

**KUELEWA REHEMA
YA
MWENYEZI MUNGU**

Kimeandikwa na:

Dkt. Mohammad Ali Shomali

Kimetarjumiwa na:

Salman Shou

Kimehaririwa na:

Ramadhani S K Shemahimbo

ترجمة

معرفة رحمة الله

تأليف

محمد علي شومالي

من اللغة الإنجليزية إلى اللغة السواحلية

**©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION**

ISBN: 978 - 9987 - 17 - 027 - 2

Kimeandikwa na:
Dkt. Mohammad Ali Shomali

Kimetarjumiwa na:
Salman Shou

Kimehaririwa na:
Ramadhani S K Shemahimbo

Kime pangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Septemba, 2013
Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: + 255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: w.w.w.alitrah.info

YALIYOMO

Neno la Mchapishaji.....	01
SEHEMU YA KWANZA:	03
Kuelewa Rehema ya Mwenyezi Mungu.....	03
Rehema ya Mwenyezi Mungu haina mpaka.....	03
Lengo la Kuwaumba Binadamu	08
Sehemu ya Pili:	26
Majina na Sifa za Mwenyezi Mungu ndani ya Qur'ani	26
Rehema ya Mwenyezi Mungu swt, kama lengo la Uumbaji wake	40
1. Kumwabudu na kumjua Yeye	40
2. Kutoa na kudhiihirisha rehema Yake	42
Sifa za Mwenyezi Mungu swt, zinazofuatana na Rehema na uwezo ...	44
SEHEMU YA TATU:	51
Maelezo Mafupi.....	51
Utangulizi	51
Sifa za Ziada za Rehema ya Allah	52
Allah swt anatuhurumia sisi na Yeye anatutarajia sisi tuhurumiane sisi kwa sisi	63
Rehema ya Allah swt, haiwezi kuzuiwa.....	64
Rehema ya Allah swt, hukunusuru wewe na adhabu.....	64
Maelezo ya ziada ya Rehema ya Allah swt, Mwenye Rehema na Mkwasi	66
Mwingi wa Rehema na Ujuzi	66
Rehema ya Mwenyezi Mungu inakizingira kila kitu	70
Allah swt, amefanya Rehema kuwa wajibu juu Yake	73
Nini maana ya 'kutubu haraka?'	78
Hitimisho	78

SEHEMU YA NNE:	81
Dhima ya Rehema ya Mwenyezi Mungu katika maisha yetu ya kidunia	81
Kuhifadhi mbingu na kuumbwa kwa nyota.....	82
Kupishana kwa mchana na usiku	83
Upopo na mvua.....	84
Wanyama	85
Usafiri ndani ya bahari ndogo na bahari kuu	86
Ulinzi Dhidi ya Mabalaa.....	87
Msaada na ulinzi katika masuala maalum.....	90
Dhima ya Rehema ya Mwenyezi Mungu katika Kumuongoza Mwanadamu	93
Kumpeleka Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kama rehema.....	93
Kumpeleka Nabii Isa kama rehema	100
Hitimisho	100
SEHEMU YA TANO:	102
Mukhtasari wa Yaliyopita	102
Mwongozo wa Mwenyezi Mungu.....	102
Vitabu vya mwongozo na rehema.....	104
Mwenyezi Mungu hutoa sheria kutokana na rehema Yake.....	112
Mwenyezi Mungu hutusaidia na kutufadhili sisi kutokana na rehema Yake.....	114
Ulinzi dhidi ya Shetani.....	114
Ulinzi dhidi ya Upotoshwaji.....	117
Ulinzi dhidi ya ushawishi wa nafsi	118
Rehema ya Mwenyezi Mungu hutakasa moyo	122
Rehema ya Mwenyezi Mungu huwazuia watu wasikate tamaa.....	123
Hitimisho	125

SEHEMU YA SITA:	126
Mukhtasari wa Yaliyopita	126
Wajibu wa rehema ya Mwenyezi Mungu katika msamaha.....	126
Kubadilisha matendo maovu kuwa matendo mema	127
Nafasi ya rehema ya Mwenyezi Mungu katika kurahisisha mambo yetu.....	129
Aina ya majibu kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu	130
Jinsi ya kupokea rehema nyingi zaidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu	134
Mwenye subira hupokea rehema za ziada	137
SEHEMU YA SABA:	143
Mukhtasari wa Yaliyopita	143
Wale wanaostahili kupokea rehema ya ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu	143
1. Wenye Subira.....	143
2. Wenye kutenda mema	143
3. Wale wanaosikiliza Qur`ani kwa makini.....	144
4. Wale wanaoswali usiku (salatul-layl) hupokea rehema za ziada	145
5. Walio Wema	146
6. Wale wanaoomba msamaha	147
7. Wale wanaoombewa na malaika	148
8. Wale wanaohama na kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu	149
9. Watifiu	152
SEHEMU YA NANE:	161
Mukhtasari wa Yaliyopita	161
Sifa za malipo ya thawabu.....	165

KUELEWA REHEMA YA MWENYEZI MUNGU

Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu watu kwa ajili ya nia zao njema na hawaadhibu kwa nia zao mbaya.....	170
Mwenyezi Mungu huzidisha thawabu kwa ajili ya matendo mema; adhabu kwa ajili ya matendo mabaya hazizidishwi	171
Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu wale wanaofanya matendo ambayo yamependekezwa ndani ya baadhi ya hadithi, hata kama hadithi hizo haziko sahihi hasa.....	174
Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu wacha-Mungu kufuatana na utendaji wao mzuri sana.....	176
Mwenyezi Mungu huwalipa wenye subira bila kipimo.....	178
Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe.....	179
Aina mbali mbali za msamaha.....	180
Mwenyezi Mungu hamuadhibu yejote kwa maovu ya mtu mwengine, lakini anaweza kumsamehe mwenye dhambi kwa tendo zuri la mtu mwengine.....	186
Mwenyezi Mungu husamehe kupitia uombezi.....	189
Mwenyezi Mungu huwasamehe wale wenye matumaini katika msamaha Wake	191
Kauli ya mwisho.....	194
Hitimisho	195

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu ulichonacho mikononi mwako ni mfululizo wa makala zilizoandikwa na mwanachuoni mahiri Dkt. Mohammad Ali Shomali wa Iran. Katika makala hizi mwandishi anazungumzia kuhusu Rehema ya Allah (s) kwa viumbe Wake

Rehema ni neema kubwa ambayo Allah amewaruzuku vi-umbe Wake wote. Hata hivyo, Allah ameigawa rehema hii katika sehemu mbili; kwanza hapa ulimwenguni kwa viumbe wote bila kujali kama wao ni waumini au la, na sehemu ya pili itakuwa ni Akhera kwa ajili ya watu wema tu. (Allah atu-jaaliye tuwe mionganoni mwa watu wema – Amin.)

Mwandishi ameelezea kwa kina kuhusu rehema na maana yake, na kwa kufanya hivyo amenukuu aya nyingi za Qur'ani Tukufu na Hadithi.

Kwa mfano mwandishi amenukuu hadithi moja kutoka kwa Imam Baqir AS aliposema kwamba Mwenyezi Mungu alimwambia Musa: "Ewe Musa! Nipende Mimi na uwafanye Watu wangu wanipende Mimi."

Musa akasema: "Mola wangu. Unajua kwamba hapana mwingine ninayempenda mimi kuliko Wewe. Hata hivyo, [niambie] nitawezaje kuwafanya watu wengine wahamasike kukupenda Wewe zaidi?"

Allah akamuambia: "Wakumbushe waja Wangu kuhusu neema na baraka Zangu kwao."

Wanadamu ni wepesi sana wa kusahau, hivyo, wanahitaji mara kwa mara kukumbushwa na ndio maana Allah akatuma Mitume wengi ili kuja kuwakumbusha wanadamu neema walijopewa na Allah. Ujaji wa Mitume ulipokoma na kuishia kwa Mtukufu Mtume Muhammad SAW, Allah akateua Maimamu Watukufu AS kwa madhumuni hayohayo na baada yao ni wanavyuoni (maulamaa) ndio ambao wamechukuwa jukumu hili. Na hili ndilo alilofanya na analoendelea kufanya mwandishi mwanachuoni huyu kutukumbusha neema za Allah juu yetu. Tunamwomba Allah atufanye ni wenye kumkumba na kushukuru neema Zake juu yetu – Amin.

Tumekiona kitabu hiki ni chenye manufaa makubwa susan wakati huu ambapo watu wana hamu kubwa ya kutaka kujuu dini yao, na upotoshaji wa historia ni vitu ambavyo havina nafasi kwa watu wa sasa.

Taasisi yetu ya Al-Itrah imeamua kuchapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni che nye manufaa makubwa kwao.

Tunamshukuru ndugu yetu Salman Shou kwa kufanikisha tarjuma ya kitabu hiki katika lugha ya Kiswahili, pia na wale wote waliosaidia kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake. Allah awalipe wote malipo mema hapa duniani na huko Akhera pia. Amin

Mchapishaji:
Al-Itrah Foundation
Dar es Salaam.

SEHEMU YA KWANZA

KUELEWA REHEMA YA MWENYEZI MUNGU

Rehema ya Mwenyezi Mungu ni sifa ya Mwenyezi Mungu Rambayo imetajwa mara nyingi sana ndani ya Qur`ani. Zaidi ya umuhimu wake wa kiteknolojia, rehema ya Mwenyezi Mungu inachukua nafasi kubwa katika mambo ya kiroho na ya kimaadili ya Kiislamu. Kujaribu kuelewa rehema ya Mwenyezi Mungu kukifuatiwa na kujaribu kuwa mwema kwa wengine huunda kiini cha safari ya kiroho na utekelezaji wa kimaadili. Katika mlolongo huu wa makala hizi, tutajaribu kuchunguza vipengele mbalimbali vya rehema ya Mwenyezi Mungu kuhusiana na sifa Zake na matendo Yake. Miongoni mwa matendo Yake tutalenga kwenye kuumbwa kwa binadamu na mpango Wake kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu. Ni dhahiri kwamba uelewa wetu wa sifa yoyote ya Mwenyezi Mungu na hususan rehema yake ni mdogo sana. Yeye ni mkubwa zaidi kuliko vile tunavyoolewa na kumuelezea.

REHEMA YA MWENYEZI MUNGU HAINA MPAKA

Rehema ya Mwenyezi Mungu haina ukomo na haikubali masharti yoyote. Ukomo pekee upo katika uelewa wetu na kwa hiyo inawezekana tushindwe kufahamu vipengele vyote

vya rehema Yake. Rehema Yake inakumbatia yote na inajumuisha yote, hakuna kitu kinachoangukia nje yake. Kwenye dua nzuri sana ambayo imependekezwa kusomwa kila baada ya swala ya kila siku, tunasema:

اللهم إِنْ مغفرتك أرجى من عملٍ

“Ee Allah! Msamaha Wako hunipa matumaini zaidi kuliko matendo yangu.”

Hata hivyo, tunapaswa kuzingatia kwamba kutenda matendo mema ni jambo linalopasa hasa. Kule kuwa na imani tu peke yake haitoshi. Imam Ali (a.s.) alisema:

لَا تَكُنْ مِّنْ يَرْجُو الْآخِرَةَ بِغَيْرِ الْعَمَلِ

“Usiwe kama yule ambaye hutaraji [furaha kamili huko] Peponi bila vitendo.”

Ili kuweza kupata hadhi iliyo bora huko Akhera, mtu anatakiwa kufanya matendo mema. Lakini suali ni kwamba: Je, ni vitendo vizuri vya mtu ndivyo vitakavyokuwa jambo kuu la kumuokoa mtu na kumnyanyua hadi kwenye viwango vya juu huko Akhera, au ni msamaha wa Mwenyezi Mungu ndiyo unaofanya hivyo? Kama tutakavyoona baadaye, ni kwa sababu ya malipo Yake yenye ukarimu ambayo kwayo ndipo vitendo vyetu vidogo vitakapokuwa vya maana sana. Ndiyo maana tunasema:

“Msamaha Wako hunipa matarajio zaidi kuliko matendo yangu.” Kwa mfano, fikiria kwamba kuna mwanafunzi ambaye anakaribia kufanya mtihani mgumu. Pamoja na kwamba amesoma sana, anajua kwamba kama mwalimu wake akisahihisha makaratasi yake bila huruma atafeli mtihani. Licha ya juhudhi yake yote, somo hilo ni gumi sana kujifunza na kujuu yote yaliyomo humo.

Halafu tunamwambia Mwenyezi Mungu:

وَإِنْ رَحْمَتُكَ أَوْسَعُ مِنْ ذَنْبِي

“Ee Allah! Hakika rehema Yako ni kubwa mno kuliko dhambi zangu.”

Hapa muombaji anakiri mbele ya Allah kwamba ametenda dhambi kubwa na mbaya mno. Lakini kwa vipi dhambi zinakuwa kubwa? Mtu anapotenda dhambi, kwa kweli huwa anamuasi Mola wa mbingu, Mola wa ardhi, na Mola wa chochote kilichomo baina yao. Kwa hiyo, hata uasi mdogo tu mbele ya Mola Mtukufu kama huyo ni mkubwa. Hii si kwa sababu mkosaji anao umuhimu wowote au kwamba uasi wake unamdhuru Allah., lakini ukweli kwamba alithubutu kumuasi Mola kama huyo, kwenyewe ni kosa na dhambi kubwa. Kwa hiyo, kwa mtazamo mmoja, inaweza kusemwa kuwa hakuna madhambi madogo. Hata hivyo, unapofanywa ulinganisho baina ya dhambi moja na nyingine, pataonekana dhambi kuu na ndogo. Kwa vyovyyote vile, ingawaje dhambi zetu ni kubwa sana, matumaini yetu yapo kwenye rehema ya Allah. ambayo ni kubwa zaidi.

Halafu tunasema:

اللَّهُمَّ إِنِّي لَمْ أَكُنْ أَهْلًا أَبْلَغُ رَحْمَتَكَ
فَرَحْمَتَكَ أَهْلَ أَنْ تَبْلُغَنِي وَتَسْعِنِي

“Ee Allah! Endapo mimi sina sifa ya kufikia rehema yako, rehema Yako ina uwezo wa kunifikia na kunikumbatia”

Si hivyo kwamba mtu mwenye matumaini ya rehema ya Allah anastahiki kuipata rehema hiyo. Lakini ni hiyo rehema Yake ndiyo yenye sifa ya kuja na kutukumbatia sisi. Kwa nini iwe hivyo?

لَأَنَّهَا وَسَعَتْ كُلَّ شَيْءٍ

“Kwa sababu rehema Yako imekikumbatia kila kitu.”

Kama asemavyo Allah Swt ndani ya Qur`ani:

وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ

“.....na rehema Yangu imekienea kila kitu.....” [7:156].

Huvezi kudhania kuwepo kitu chochote kisichonufaika kutokana na rehema Yake; vinginevyo, kusingekuwepo na kitu chochote, na hata kama ikiwa hivyo, hakuna kitu ambacho kingeendelea kuishi. Hata lile suala la kwamba Shetani ana uwezo wa kuendelea maisha yake, ni kutokana

na rehema ya Allah. Shetani alipong`ang`ania tabia yake potofu na akalaaniwa, alimuomba Mwenyezi Mungu ampe muda hadi Siku ya Ufufuo.

قَالَ رَبُّ فَانظِرْنِي إِلَى يَوْمٍ يُبَعَثُونَ

“Akasema (Iblis): Mola wangu! nipe muda mpaka siku wa-takayofufuliwa.” [15:36].

Allah akajibu:

قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِينَ إِلَى يَوْمِ الْوَقْتِ الْمَعْلُومِ

“Akasema (Mwenyezi Mungu). Hakika wewe ni katika wale waliopewa nafasi. Mpaka siku ya wakati uliowekwa.”

[15:37-38]

Hivyo, Shetani amepewa nafasi ya kuendelea kuishi. Bila shaka, hili halitaendelea kama alivyoomba hadi Siku ya Ufufuo. Itakuwa “**Mpaka siku ya wakati uliowekwa.**” Patakuwepo wakati kabla ya Siku ya Ufufuo ambapo Shetani atasimamishwa. Kwa hali yoyote ile, hata Shetani hunufaika na rehema ya Allah. Mwenyezi Mungu huwarehemu hata wale wasiomuamini au wanaothubutu kupingana Naye.

LENGO LA KUWAUMBA BINADAMU

Kama tutakavyoona baadaye, kuchunguza sifa na matendo ya Mwenyezi Mungu na kuchunguza kuumbwa kwa binadamu, kumuongoza kwa kumpelekea ujumbe kupitia Mitume Wake, na malipo Yake yenyeye wingi wa ukarimu yanaweka wazi kwamba msingi wa kila kitu umeegemea kwenye rehema Yake. Kwa kweli, kadhia yote ya uumbaji inaweza kufupishwa katika sentensi chache: Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema, alitaka kuonyesha rehema Zake. Kwa hiyo, aliumba dunia hii. Aliwapa binadamu rehema Yake ili wawe wawakilishi Wake hapa duniani na kuwa ndio njia ya rehema Yake. Hata hivyo, kwa bahati mbaya binadamu wengi walishindwa. Hawakumwakilisha Yeye ambaye ni Mwingi wa rehema. Badala yake, binadamu walio wengi walimwakilisha yule adui wa Mwenyezi Mungu. Hawa ndio "wale mashetani kutoka mionganini mwa binadamu"¹ ambao badala ya kuwa wawakilishi wa Mwenyezi Mungu, walichagua kumfuata na kumtumikia Shetani.

Hata hivyo, endapo hata kama mtu mmoja tu kwa kweli anakuwa mwakilishi wa Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema, dunia hii ingekuwa na thamani sana na kustahili kuumbwa. Mtu mmoja mkamilifu ni mzito zaidi na ni mkubwa zaidi kuzidi mamilioni ya watu wasio waadilifu. Fikiria chuo kikuu ambamo maelfu ya wanafunzi wanaweza kuchukua mafunzo hapo, lakini kwa sababu ya uchaguzi wao mbaya wanaofanya katika baadhi ya mambo, kama vile uzembe, ni Avicenna au Aristotle mmoja tu ambaye amehitim. Hivi sio bora kuendelea kuwa na chuo kikuu hiki na kuwapa

¹ Rejea Sura ya [6:112]

watu fursa na nafasi ya kuendelea na kustawi na hatimaye kuwa na angalau Avicenna au Aristotle mmoja? Kwa kiasi Allah anavyohusika, kila mtu anaweza kuwa mtu mwema. Amempa kila mtu fursa hii bila ya kuweka mpaka wowote. Kwa hiyo, kuendelea kuwepo watu wavivu au wasiotaka kuwa wema haimaanishi kwamba chuo kikuu kifiki mwisho wake. Jambo hilo hilo linatumika kwa shule, misikiti, na taasisi zingine za kielimu. Muhimu zaidi, linatumika kwa kadhia yote ya maumbile.

Bila shaka wapo wengi ambao wamekuwa wawakilishi wa Mwenyezi Mungu. Katika kipindi chote cha historia, wamekuwepo maelfu ya watu ambao walipata daraja hili. Pamekuwepo takriban Mitume laki moja na ishirini na nne elfu [124,000]. Idadi hii ni kwa nyongeza kwa warithi maasum au watu watukufu ambao wamewafuata. Kwa vyovyyote vile, Mwenyezi Mungu anataka binadamu wote wawe njia ya mkondo wa rehema Zake kwa wengine, na amewapa njia nydingi na vipaji vya kufanyia hivyo. Jambo hili halijumuishi watu tu, lakini na wanyama, mimea, au kwa kweli kila kitu katika viumbe, pamoja na maji, hewa, na udongo.

Njia moja muhimu ya kuwa mwenye huruma ni kuelewa vizuri zaidi rehema ya Mwenyezi Mungu na yote yale ambayo ametufanyia sisi. Kwa mujibu wa hadith maalum (*hadith-e Qudsi*) ambayo imesimuliwa katika vyanzo vingi na kutoka kwa Maimam mbalimbali kama vile Imam Baqir (a.s.), Imam Ridha (a.s.), na Imam Asqari (a.s.), Mwenyezi Mungu alimtengenezea Nabii Musa (a.s.) mkakati wa kuenezea ujumbe. Kwa mfano, Imam Baqir (a.s.) anasema kwamba Mwenyezi Mungu alimwambia Musa:

قال الله عزوجل: يا موسى احبني واحببني إلى خلي

**“Allah. anasema: Ewe Musa! Nipende mimi na uwafanye
water wangu wanipende mimi.”²**

Ninaamini hii inaweza kufanya kuwa sera ya jumla katika maisha yetu. Kama mtu inaweza kumpenda Allah. na kuwafanya watu wengine wampende Yeye, atapata kila kitu kilicho kizuri. Wakati wote tunapaswa kutathimini utekelezaji na maendeleo yetu kuhusu jambo hili. Watu wanatakiwa kutathimini ni kwa kiasi gani wanampenda Allah., wamewafanya kwa kiasi gani watoto wao, washirika wenzao, majirani zao, ndugu zao, na marafiki zao waweze kumpenda Allah. Kufuzu kwa mtu yeoyote kunaweza kuamuliwa kwa tathimini hii. Watu bora zaidi ni wale wampendao sana Allah. na ambao wanaweza kuwafanya wengine wajihisi kama wao. Musa alijibu:

قال يا رب إنك تعلم أنه ليس شيء أحب إلي منك فكيف لي بقلوب العباد

**“Mola wangu. Unajua kwamba hapana mwingine ninayem-
penda mimi kuliko Wewe. Hata hivyo, [niambie] nitawezaje
kuwafanya watu wengine wahamasike kukupenda Wewe
zaidi?”**

Musa alijua kwamba kwa jinsi alivyokuwa anahuksika, yeye alikuwa anampenda Allah swt kuliko mwingine yeoyote. Kwa hiyo, alichohitaji ni kuuliza namna ya kufanya hivyo na wengine. Hii ilikuwa ndio changamoto kwake. Bila shaka,

² Mishkat al-Anwar, Tabarsi, uk. 332, (Najaf: Maktaba ya Haydariyyah, 1385 I.A.H.)

kwa watu walio wengi hata kwa sehemu ya kwanza, yaani, jinsi ya kumpenda Allah swt kunaweza kuwa ni changamoto. Lakini kwa Musa, changamoto ilikuwa ni kipande cha pili cha ushauri. Hapa Allah. alimwambia Musa:

ذکر هم نعمایی و الایی

“Wakumbushe waja wangu kuhusu neema na baraka Zangu kwao.”

Kwa njia hii, Mwenyezi Mungu alimfundisha Musa kwamba yeye hakuhitaji kufanya lolote isipokuwa kuwaambia watu kuhusu mambo mazuri ambayo Allah swt amewafanyia. Mwenyezi Mungu alimtaka Musa awakumbushe watu kuhusu neema zote ambazo wamepokea kutoka Kwake.

Hili ni jambo ambalo kwa kawaida husahauliwa katika mahusiano ya mtu na mtu. Kwa mfano, fikiria kijana mdogo anakujia na kukuambia kwamba wazazi wake hawampendi. Wewe ungemwambia nini? Hungemwambia kwamba tangu siku ya kwanza alipozaliwa na hata kabla ya kuzaliwa wazazi wake walikuwa wanampenda na kumjali? Kimsingi wewe ungejaribu kumkumbusha yale yote wazazi wake walivyomfanyia, jinsi wazazi wake walivyomsaidia, walivyokuwa wanamlisha, walivyokuwa wanamvisha nguo, na walivyokuwa wanamuangalia yeye, wakampa elimu nzuri na mapenzi. Kama ukifaulu kumwelewesha atajihisi vibaya na kusikitika. Atakwambia alidhania kwamba yeye amekua mwenyewe tu.

Hivyo, Allah swt alimwambia Musa kuwakumbusha watu kuhusu mambo mazuri ambayo Yeye huwafanyia. Akamweleza Musa kwa nini anamtaka yeye afanye hivyo, Anasema:

فِإِنَّهُمْ لَا يَذَكُرُونَ مِنِّي إِلَّا حَسَنًا

**“Kwa sababu hawakumbuki chochote kutoka Kwangu
isipokuwa yale yaliyo mazuri.”**

Mwenyezi Mungu hawadhuru watu na hakuna lolote baya ambalo limekuja kwao kutoka Kwake. Kwenye dua ambayo imefundishwa na Imam Sadiq (a.s.) na ikapendekezwa kusomwa kila baada ya swala ya kila siku wakati wa mwezi wa Rajab, tunamuomba Allah swt:

يَا مَنْ أَرْجُوهُ لَكُلَّ خَيْرٍ وَآمِنْ سُخْطَهُ عِنْدَ كُلِّ شَرٍ

**“Ee ambaye Kwake ninaweza kutaraji yote yaliyo mazuri na
mimi nimesalimika kutokana na ghadhabu Yake katika kila
uovu.”**

Kama mtu anataka kupata jambo jema, lazima aweke matumaini yake kwa Allah swt Hakuna mpaka kwenye fadhlila zake, uwezo, au ujuzi. Zaidi ya hayo, hapana mwengine badala Yake. Wakati ambapo Yeye ni mpole na mpaji mkarimu ambaye anaweza kukupatia wewe kila kitu na hapana mtoaji mwengine ila Yeye, hakuna mantiki ya kutafuta mwengine tena. Yeye ni mpaji ambaye hugawa kila kitu na hakuna mtoaji mwengine. Madai yoyote ya kuwa na mpaji mwengine

ambaye ni mtu mbali na Yeye, huyo ni muongo. Kila kitu walichonacho watu kimetoka kwa Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, hatutakwenda kwa wengine na tutakuwa na matumaini Kwake tu kwa yote yale ambayo ni mazuri.

Kwa upande mwingine, endapo jambo baya litatufika sisi ni lazima ieleteweke kwamba si kwa sababu ya tatizo binafsi ambalo Allah swt analo juu yetu sisi. Haina maana kwamba ametukasirikia au kwamba hatupendi. Chukulia kwamba unaye mwalimu mwenye huruma na mwema ambaye anakupenda sana na amekufundisha yote yale unayoyajua. Ukiwa na mwalimu kama huyo, utatambua kwamba kama ukipata tatizo si kwa sababu mwalimu wako analo tatizo binafsi na wewe. Kwa kawaida watu wanapofaulu kupata alama nyingi hufikiri ni kwa sababu ya juhudhi yao, lakini wanapopata maksi za chini, hushindwa kuwajibika na humlaumu mwalimu wao. Jambo hilo hilo hujitokeza katika uhusiano wetu na Allah swt Wakati tunapofaulu katika maisha yetu, kama vile, kuwa na mwenza mzuri, watoto, elimu, au biashara yenye mafanikio, huamini kwamba kufuzu huko ni matokeo ya juhudhi zetu. Hata hivyo, pale tunapokabiliwa na tatizo, tunaweza tukalihusisha na Allah swt na pengine hata kumlaumu Yeye kwalo. Ambapo ukweli ni kinyume chake. Qur`ani inaelezea kwa uwazi kabisa kuhusu jambo hili:

مَا أَصَابَكُ مِنْ حَسَنَةٍ فَمِنَ اللَّهِ طَوْهُ وَمَا أَصَابَكُ مِنْ سَيِّئَةٍ فَمِنْ نَفْسِكَ

“Wema uliokufikia umetoka kwa Mwenyezi Mungu, na ubaya uliokufikia basi umetoka kwako mwenyewe....” [4:79]

Sawa na ule mfano kuhusu yule mwanafunzi alikuwa na deni kwa mwalimu wake kwa kupata maksi za juu, kila mmoja wetu anamtegemea Allah swt kwa lolote zuri linalomtokea. Kama yule mwanafunzi ambaye kazi yake ilikuwa ni kushukuru juhudhi ambayo ilifanywa na mwalimu wake na kufanya kazi, kila mmoja wetu anatakiwa kufanya hivyo katika uhusiano wake na Allah swt Katika mfano wetu, kama kungekuwa na kutofaulu kokote, ni wazi kwamba hilo lilikuwa ni kosa la mwanafunzi. Hivyo ndivyo ilivyo kwa Allah swt Kwa hiyo, tunapaswa kujihisi tuko salama na tujue kwamba Allah swt hatufuatilii ili atuadhibu au atusababishie matatizo.

يَا مِنْ يُؤْتَى الْكَثِيرُ بِالْقَلْبِ

“Ee ambaye hukirimu kwa wingi kwa kidogo tunachofanya”

Hakuna nafasi ya kufikiri kwamba Allah swt anaweza kumlipa mtu pungufu ya kile ambacho amefanya. Zaidi ya hayo, Yeye huwapa watu kwa wingi sana kwa mambo madogo wanayofanya. Malipo yanayotolewa kwa kiwango ambacho kila mtu atatosheka kwa ukamilifu. Kwa kweli kila mtu atashangaa pale anapolinganisha kile alichopewa na kile alichofanya. Na rehema ya Allah swt haikomei hapa. Tunatambua kwamba huiendeleza hatua nydingine mbele zaidi pale tunaposema:

يَا مِنْ يُؤْتَى مِنْ سَأْلَهُ

“Ee Wewe umruzukuye yule anayekuomba.”

Si tu kwamba Allah swt anawalipa watu zawadi nyingi kwa kile kidogo wanachofanya, bali pia huwaruzuku pale wanapoomba tu vivi hivi. Huwapa hata wale wanaomuomba tu. Rehema yake wala haiishii hapa. Tunasema vilevile:

يَا مَنْ يُؤْتِي مِنْ لَمْ يَسْأَلُهُ وَمَنْ لَمْ يَعْرِفْهُ

“Ee Wewe ambaye humruzuku ambaye hakukuomba na ambaye hakutambui Wewe.”

Maneno haya yanarejelea kwenye ile hatua ya tatu amba po Mwenyezi Mungu huwapa watu hata kama hawajamumba na amba o wala hawamjui Yeye.

Endapo kuna uhaba wa kazi na kipato kwenye jiji fulani. Watawala wanalazimika kuhakikisha kwamba chakula kipo kwa ajili ya watu wote kwa kupunguza bei. Mathalani, wanaweza kuwapa watu paketi za chakula kwa bei ya pauni moja [tuchukulie mfano wa shillingi elfu tano 5,000/=] tu. Hali hii itawaridhisha watu, kwa vile kwa bei ya shillingi elfu tano tu wamepata chakula walichokuwa wanahitaji. Baada ya muda, kama watu watakuwa wameishiwa fedha, baadhi hawatasita kuendelea kuomba chakula. Wahusika wa kugawa chakula itwalazimu wawakubalie na kuwapa chakula bure. Hata hivyo, wapo watu amba o, kwa sababu fulani, hawataombwa chakula. Kama wahusika wa kugawa chakula watakuwa watu wenye huruma watawatafuta na kuwapa chakula. Watafanya hivyo kwa sababu hawataki watu hao wafe njaa. Kama watu hawaji kutuombwa msaada, tunatakiwa kuwatafuta na kuwapa msaada.

Allah huwakirimu watu sana kwa kile kidogo wanacho-

fanya. Pia huwapa kwa wingi sana wanapomuomba. Hata hivyo, wapo watu wengi ambao hawamuombi na wala hawamjui Allah swt Lakini bado, Allah swt hawazulii kutoka kwenye rehema Yake na huendelea kuwaruzuku kutoka kwenye neema Zake. Kwa kweli, wakati mwingine Mwenyezi Mungu anaweza kuwapa wasioamini neema za kidunia zaidi ya anavyowapa walioamini, kwa sababu dunia hii tu ndio kitu wanapendezewa nacho. Kufuatana na Qur`ani, kama isingekuwa baadhi ya waumini kuweka shaka katika ukweli wa imani yao, Mwenyezi Mungu angewapa kwa wingi sana wasioamini hivyo kwamba wangeweza kutengeneza dari za nyumba zao kwa dhahabu na fedha. Kwa uzuri sana Qur`ani inasema:

وَمَنْ أَرَادَ الْآخِرَةَ وَسَعَى لَهَا سَعْيَهَا وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَأُولَئِكَ كَانُ سَعْيُهُمْ مَشْكُورًا

“Na aliyetaka Akhera na akaifanyia juhudini, inayoipsa, naye ni mwenye kuamini, basi hao ndio juhudini yao itakubaliwa.” [17:19]

Mojawapo ya majina ya Allah ni ‘Shakur’ [Mwenye Kushukuru Sana]. Ni muhimu kweli kutafakari juu ya hali ya kushukuru ya Mwenyezi Mungu. Mathalani, jambo moja la kuvutia ni kwamba Allah huwashukuru wale wanaotenda mema na kufanya kazi kwa ajili ya Akhera yao bila kunufaika kutokana na vitendo vyao wanavyofanya. Wao ni wapokeaji tu wa neema Zake. Na bado huwashukuru na kuyatakabalia matendo yao. Hii ni kwa ajili ya watu wanaojituma kwa ajili ya Akhera. Hata hivyo, Allah swt anasema kwamba hata watu wanojituma kwa ajili ya dunia hii pia wamejumuishwa

kwenye rehema Yake. Hufanya hivyo kwa kuwasaidia wapate kile wanachotaka.

مَنْ كَانَ يُرِيدُ الْعَاجِلَةَ عَجَّلْنَا لَهُ فِيهَا

“Anayetaka (dunia hii) ipitayo upesi, tutamharakisha humo....” [17:18]

كُلَّا نُمُدُ هُولَاءِ وَهُولَاءِ مِنْ عَطَاءِ رَبِّكَ وَمَا كَانَ عَطَاءُ رَبِّكَ مَحْظُورًا

“Wote tunawasaidia hawa na hawa katika kipawa cha Mola wako, na kipawa cha Mola wako hakizuiliki (kumfikia mja wake).” [17:20]

Hii ni kama vile mtu anapowasaidia watoto wake ingawaje wao inawezekana wasimpende yeye. Bila shaka, yeye hawezi kuwasaidia katika mambo maovu; bali huwasaidia katika njia ambayo itawafanya watimize malengo yao mazuri na wakati ule ule akiwaambia kwamba kila mmojawao atahusika na matendo yake na wanawajibika kutenda matendo mema.

Kwa hiyo, Allah swt huwaruzuku wale ambao wametenda mema kidogo, wale ambao humuomba, wale ambao wala hawamuombi, na muhimu zaidi, wale ambao hata hawamtambui Yeye. Sasa tumeelewa sehemu hii ya dua ambayo impendekezwa kutumika mwezi wa Rajab, ambayo inasomeka ifuatavyo:

يَا مَنْ يُؤْتَى مِنْ سَأْلَهُ يَا مَنْ يُؤْتَى مِنْ لَمْ يَسْأَلْهُ وَمَنْ لَمْ يَعْرِفْهُ تَحْنَنَا مِنْهُ وَرَحْمَةٌ

“Ee Wewe unayemruzuku yule anayemuomba. Ee Wewe unayemruzuku yule asiyemuomba Yeye na hamjui Yeye lakini unafanya hivyo kutokana na huba na huruma yako”

Kuendelea na Du'a hiyo tunasema:

أعطني بمسئلتي إياك جميع خير الدنيا وجميع خير الآخرة ، واصرف عني بمسئلتي إياك جميع شر الدنيا وشر الآخرة

“Naomba uniruzuku, kile ambacho nimekiomba kutoka Kwako, mazuri yote ya dunia hii na yote mazuri ya Akhera. Niepushe na maovu yote ya dunia hii na ya Akhera, am-bayo nimekuomba Wewe.”

Tunapofika hapa swali linajitokeza: Mtu anawezaje kuwa na matarajio kama haya? Kumuomba Allah swt mazuri yote ya duniani na Akhera na kuyaondoa yote maovu ya duniani na yote maovu ya Akhera inaweza kuonekana kama vile yamezidi mno na ni tamaa ya makuu mno. Jibu linakuja kama ifuatavyo:

فانه غير منقوص ما أعطيت

“Kwani kwa kweli, hakikupunguzii chochote kile unachokitoa kwetu.”

Isije ikafikiriwa kwamba ombi hili ni kubwa mno. Allah swt anapotoa kitu hakisababishi upungufu wowote katika

ukwasi Wake. Kufuatana na viwango vyetu ni kubwa mno lakini kwa Allah swt si chochote, hakuna kilichopungua. Tofauti na mtu anapotoa fedha kwa mwingine na fedha ya mtoaji hupungua, Allah swt anapotoa hakumpunguzii kile alichonacho. Hii ni kama vile unapomfundisha rafiki yako kitu, sio tu kwamba hupunguzi chochote katika ujuzi wako, lakini ujuzi wako unaweza pia kuongezeka. Tukiwa tunajua hili, tunamuomba Allah swt:

وزدني من فضلك

“Nakuomba uniruzuku zaidi kutoka kwenye fadhila zako.”

Sehemu hii ya dua inashangaza sana. Baada ya kumuomba Allah atupe mema yote ya dunia hii na Akhera na kutuepusha na yote maovu ya duniani na Akhera, bado tunamuomba aturuzuku zaidi. Inawezekana labda yapo mambo fulani ambayo kamwe hatujayafikiria na kwa hiyo wala tusingeomba. Tunamuomba Allah swt asiziwekee mpaka fadhila Zake kwenye matarajio yetu. Tunamuomba Allah swt kutupatia kila chochote kile Alichonacho cha kutoa na sio kile tunachohitaji au kuomba tu. Hii ni sawa na vile Qur`ani inavyoeleza kuhusu watu wa Peponi. Watapewa chochote wanachokipenda, chochote wanachokitaka, na hata zaidi:

وَفِيهَا مَا تَشْتَهِيهُ الْأَنْفُسُ وَتَلَذُّ الْأَعْيُنُ

“..... na vitakuwamo ambavyo nafsi zinavipenda na macho yanafurahia,” [43:71]

Na:

لَهُمْ مَا يَشَاءُونَ فِيهَا وَلَدَيْنَا مَرْيَدٌ

“Humo watapata chochote wakitakacho, na kwetu kuna zaidi.” [50:35]

Mtu anapokitamani kitu ina maana kwamba amekielewa kwanza. Tunatambua kwamba uelewa wetu una mipaka. Kwa hiyo, hata kama tunatamani kile tunachokijua, bado yapo mambo ambayo hatuyajui. Mwenyezi Mungu anawaruzuku watu wa Peponi chochote wanachotaka pamoja na kile ambacho hawakijui. Fikiria kwamba unaye mtoto wa miaka mitatu. Unamwambia akuombe chochote ana-chokitaka. Atakuomba nini? Atakuomba kitu ambacho kwa kawaida watu wa umri mkubwa wanakiona ni kitu kisicho na maana: chokoleti chache, biskuti, au wanasesere kad-haa, kwani hivi ndivyo vyote ambavyo anaweza kuvififikiria. Mtoto wa umri wa miaka mitatu hawezi kamwe kuomba ny-umba au fedha za karo ya shule kwa ajili ya elimu yake ya juu.

Sisi binadamu ni kama mtoto huyu mbele ya Allah swt Matakwa yetu ni madogo sana yakilinganishwa na kile alichonacho Yeye. Maombi yetu hayakuwekewa mpaka kwenye neema Zake. Huko Peponi, kila mtu anapoomba yote yale anayotaka, Allah swt hufanya ifahamike kwamba bado ana-vyo zaidi. Vipo vitu ambavyo anavijua Allah swt peke Yake tu. Tunawezaje kuelewa furaha ambayo Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alikuwa akiipata wakati akiswali sala zake? Furaha

kubwa sana tuliyonayo katika maisha yetu ni ndogo sana ikilinganishwa na ile furaha aliyokuwa anaipata Mtukufu Mtume (s.a.w.w.). Wakati mwingine tunapohisi kuridhika na swala zetu, na tunadhani kwamba swala ya Mtume (s.a.w.w.) lazima iwe sawa na ile ya kwetu lakini inazidi kidogo kwa ubora. Hatuwezi kuelewa zaidi ya pale. Ni Mtume (s.a.w.w.) peke yake ndiye anaweza kuelewa hilo. Yapo mambo mengi mno ambayo kamwe sisi hatujawahi kuyafikiria.

Peponi, watu wanaweza kuwa na vitu kama vile walivyokua navyo hapa duniani. Kama wakitaka matunda ya tufaha, tini, au zeituni, wanaweza kuyapata. Bila shaka yatakuwa na sifa za Peponi. Qur`ani inasema:

وَبَشِّرِ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ جَنَّاتٍ تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا
الْأَنْهَارُ كُلُّمَا رُزِقُوا مِنْ ثَمَرَةٍ رُزْقًا لَا قَالُوا هَذَا الَّذِي رُزِقْنَا مِنْ قَبْلُ
وَأَنُوا بِهِ مُتَشَابِهًاتٍ وَلَهُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُطَهَّرَةٌ وَهُمْ فِيهَا خَالِدُونَ

“Na wabashirie walioamini na kutenda vitendo vizuri, kwamba watapata Mabustani yapitayo mito chini yao, kila mara watakapopewa matunda humo kuwa riziki, watasema: Haya ndiyo tuliyopewa zamani, nao wataletewa yenye kufanana, na humo watapata wake waliotakasika, nao watakuwa humo milele.” [2:25].

Kwa hiyo, kuhusu baadhi ya neema, kama vile matunda watu watasema kwamba yanafanana na yale waliyopewa zamani. Lakini pia huko Peponi kuna vitu ambavyo kamwe hakuna jicho ambalo limewahi kuviona, hakuna sikio ambalo limewahi kusikia, hakuna moyo ambaao umewahi kuvifikiria. Vipo vitu ambavyo Allah swt amevificha kama kishtukizo

kwa wenyewe haki. Mathalani, kuhusu wale wanaoswali Swala za Usiku (*salat al-layl*), Qur`ani inasema:

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَا أُخْفِيَ لَهُمْ مِنْ قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Nafsi ye yote haijui walichofichiwa katika hayo yanayofurahisha macho, ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyafanya.”

[32:17]

Kuna maelezo mengine ya mazungumzo baina ya Allah swt na Nabii Musa (a.s.) ambamo kuna mwishilizio wa ziada baada ya Musa kuambiwa awakumbushe watu kuhusu neema Zake ili kwamba waweze kumpenda Yeye. Kufuatana na mazungumzo haya ya kina, Imam Askari (a.s.) anasimulia kutoka kwa Imam Sajjad (a.s.) kwamba Mwenyezi Mungu al-imwambia Musa:

فَلِإِنْ تَرَدَّ أَبْقَا عَنْ بَابِيْ ، أَوْ صَلَا عَنْ فَنَائِيْ أَفْضَلُ لَكَ مِنْ عِبَادَةِ مَائَةٍ
سَنَةٌ بِصِيَامِ نَهَارَهَا وَقِيَامِ لَيْلَهَا .

“Kama ukimrejesha Kwangu mja Wangu ambaye ametoroka kutoka Kwangu au mtu ambaye amepotea njia ni bora zaidi kwako kuliko miaka mia moja ya ibada ambapo unafunga saumu kila siku na kuswali kila siku usiku.”

Allah swt hamhitajii mtu ye yote, lakini bado, kwa rehema Zake, hamtakii hata mtu mmoja kupotea. Halafu Musa (a.s) akauliza:

وَمَنْ هُذَا أَعْبُدُ إِلَّا بَنِيَّهُ؟

“Ee Allah! Ni mja wako yupi ambaye ametoroka?”

Allah swt akajibu:

العاصي المتمزد

“Yule anayeniasi Mimi na hanisikilizi Mimi”

Allah anawataka watenda dhambi watubie dhambi zao na warejee Kwake. Kwenye hadithi Qudsi tunasoma:

لَوْ عَلِمَ الْمُدْبِرُونَ كَيْفَ اسْتَبَاقَيْ بِهِمْ لَمَاتُوا شَوْقًا

“Kama watu ambao wameniasi wangejua ninawapenda kiasi gani, na wakarejea, wangekufa kwa kufurahi sana.”

Inaweza kueleweka kutoka kwenye riwaya hii kwamba wakati wowote mtu anapokuwa na tatizo linalohusiana na Allah swt tunatakiwa kujaribu kuwasuluhisha. Allah swt ametupatia mamlaka ya kuwalingania warudi Kwake. Kamwe tusiache mfarakano baina ya mja na Allah swt kuwa mkubwa zaidi kwa kumwambia mhusika wewe huna matumaini huna nafasi ya kurudi Kwake. Kwa bahati mbaya baadhi ya watu wamekuwa wakifanya hivi. Kama mtu ana tatizo dogo wao hulifanya kuwa baya zaidi. Kwa kawaida hali hii hujitokeza kwa sababu ya mtu kujivunia vitendo vyake vyema na ku-

kadiria kwa upungufu sifa nzuri na vitendo vizuri ambavyo mtu mwingine anaweza kuwa navyo. Kila mtu anatakiwa kujaribu kuwatia moyo na kuwahimiza watu wamrudie Allah swt na awafikirie kwamba hatimaye watu hao wanawenza kuwa bora zaidi kuliko yeye machoni kwa Allah swt Si vema mtu kuanza kujifurahia yeye mwenyewe, kwani mtu ambaye anaweza kuwa mwema na karibu sana na Allah swt leo; lakini pia si jambo la kushangaza baadaye akaishia kuwa mtu muovu mbele ya Allah swt

Halafu Musa (a.s.) akauliza:

فمن الضال عن فنا ؟

“Ni mja yupi yule ambaye amepotea njia inayoelekea Kwako?”

Mwenyezi Mungu akajibu:

الجاهل بِإِيمَانِ زَمَانِهِ تَعْرُفُهُ، وَالغَائِبُ عَنْهُ بَعْدَمَا عَرَفَهُ، الْجَاهِلُ
بِشَرِيعَةِ دِينِهِ ، تَعْرُفُهُ شَرِيعَتُهُ، وَمَا يَعْدُ بِهِ رَبُّهُ ، وَيَتَوَصَّلُ بِهِ
إِلَى مَرْضَاتِهِ.

“Yule asiyemjua Imam wa zama zake, mtambulisse Imam wake Kwake. Na kwa yule aliye kuwa anamjua Imam wa zama zake, lakini alimkosa. Na kwa yule asiye jua sheria na kanuni za dini yake mwenyewe, mfundishe yeye sheria na kanuni na vitendo ambavyo kwavyo anaweza kumwabudu Mola Wake na kutafuta radhi Zake.”

Kwa hiyo, kila mmoja anatakiwa kujaribu kuwatambuli-sha watu kwa Imam Mteule wa Mwenyezi Mungu zama zao. Hii ni muhimu na la maana zaidi kuliko kumtambulisha mtu kwa baba au mama yake aliyepotea. Pia kila mtu anatakiwa kujaribu kuwasaidia watu kujifunza dini yao na wajibu wao wa kidini.

Kwa hiyo, sera sahihi na nzuri katika mazungumzo yoyote kuhusu Mwenyezi Mungu ni kuwasaidia watu wazielewe zaidi na kuzikumbuka neema Zake na kumpenda Yeye zaidi. Kama, kwa sababu yoyote ile, uhusiano wao na Mwenyezi Mungu umetetereka, wanatakiwa kutiwa moyo wamrudie Yeye. Sio sahihi kusababisha utengano baina ya watu na Mwenyezi Mungu au kumwelezea Mwenyezi Mungu kwa njia ambayo inawatia watu woga. Wakati mwingine baadhi ya watu wan-apozungumza na watoto wao kwa lengo la kuwahimiza watekeleze vitendo fulani vya kidini, hutumia lugha na mantiki ya kutisha. Kwa mfano, wanawaonya watoto wao kwamba kama hawaswali au kuvalaa hijabu, Mwenyezi Mungu atawatupa Jahannam. Watoto wakisikia maneno haya kutoka kwa wazazi wao, wataanza kufikiri kwamba Mwenyezi Mungu anaweza kukasirika kwa urahisi sana na kukimbilia kutoa adhabu kali kwa watu. Inaonyesha kwamba huu si mwelekeo mzuri wa kufaa. Badala yake, wazazi wanatakiwa wazalishe mapenzi na shukurani juu ya Allah swt katika nyoyo za watoto wao ili watoto waweze kuhisi wanao wajibu na wafanye mambo kwa hiari zao na kwa furaha kumridhisha Mwenyezi Mungu.³

³ Mustadrak al-Wasail, Muhadithi Nuri, Juz. ya 12, uk. 240, (Qum: Ahlul Bayt Institute, 1408 L.A.H.).

SEHEMU YA PILI

MAELEZO MAFUPI KUHUSU SEHEMU YA KWANZA

Mada kuu mbili zilizungumziwa katika Sehemu ya Kwanza: rehema ya Mwenyezi Mungu ambayo haina ukomo na kujumuishwa kwake juu ya kila kitu, na uhusiano wa rehema ya Mwenyezi Mungu na dhati Yake. Sehemu ya Pili inatoa maelezo ya kina zaidi kuhusu rehema ya Mwenyezi Mungu kama ilivyoonyeshwa kwenye Qur`ani Tukufu. Matumizi na umuhimu wa sifa za Mwenyezi Mungu, kama vile *al-Rahman*, *al-Rahim*, na *Khayr al-Rahimin*, na sifa Zake zinazofaa za rehema na nguvu zimezungumziwa kwa kuhusishwa na lengo la Mwenyezi Mungu katika uumbaji wa Ulimwengu. Rehema ya Mwenyezi Mungu - sifa ambayo imetajwa mara nyingi sana ndani ya Qur`ani - itaonyeshwa kuwa ndiyo sababu ya uumbaji wakati huo huo ikizingatiwa kwamba hiyo si ishara ya udhaifu. Mwenyezi Mungu ni Mwenye Rehema na Mwenye nguvu zote.

MAJINA NA SIFA ZA MWENYEZI MUNGU NDANI YA QUR`ANI

Kwa sababu ya uelewa wetu mfinyu, hatuwezi kuelewa kwa usahihi Yeye ni nini. Qur`ani inasema kwamba hapana awezaye kumwelezea Yeye kwa usahihi:

سُبْحَانَ اللَّهِ عَمَّا يَصِفُونَ إِلَّا عِبَادَ اللَّهِ الْمُخْلَصِينَ

“Mwenyezi Mungu Yu mbali na sifa wanazompa. Isipokuwa waja wa Mwenyezi Mungu waliosafishwa.” [37:159-160]

Imam Ali (a.s.) anasema ndani ya *Nahj al-Balaghah* kwamba kama ukimuuliza mchwa amwelezee Mwenyezi Mungu, atasema Mwenyezi Mungu yu kama mchwa mkuu; kiumbe anayefanana na yeye lakini mkubwa zaidi yake. Hiki ndio kiwango cha juu kabisa cha upeo wa fikira ya mchwa. Sisi binadamu humfikiria Mwenyezi Mungu kama mchwa anavyomfikiria. Tunamfikiria Mwenyezi Mungu ni kitu kinachofanana na sisi, lakini chenyewe ni kikubwa sana zaidi yetu, chenyewe uwezo mkubwa sana zaidi yetu, ingawaje Mwenyezi Mungu si mtu mwenye uwezo kupita kiasi, au mchwa mkubwa sana au kitu kingine kikubwa sana. Mwenyezi Mungu kabisa anavuka mipaka ya uwezo wa kibinadamu, na Yu tofauti na kulingana na Qur`ani, watu pekee ambao wanawenza kumwelezea Mwenyezi Mungu ni wale tu waliotakaswa. Bila shaka, maelezo yao bado si kamili hasa ingawa yanakubalika. Kwa hiyo, njia nzuri na ya kuaminika ya kuelewa sifa za Mwenyezi Mungu ni kurejelea kwenye maneno Yake Mwenyewe, yaani Qur`ani na maneno ya waja wake waliotakaswa yaani Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na watu wa nyumbani kwake (a.s.), ambao utakaswaji wao umethibitishwa ndani ya Qur`ani na Mwenyezi Mungu Mwenyewe:

إِنَّمَا يُرِيدُ اللَّهُ لِيُذْهِبَ عَنْكُمُ الرِّجْسَ أَهْلَ الْبَيْتِ وَيُطَهِّرَكُمْ تَطْهِيرًا

“Hakika Mwenyezi Mungu anataka kuwaondolea uchafu, enyi watu wa nyumba ya Mtume, na kuwatakasa kabisa kabisa.” [33:33].

Kufuatana na baadhi ya uchunguzi , sifa zinazohusiana na rehema Yake kwa wazi zimetumika takriban mara mia sita ndani ya Qur`ani na hii ni mbali na vile vitu vinaashiria tu rehema Zake, kwani kama tukivihesabu navyo pia, vitakuwa ni maelfu.⁴ Kwa hiyo Mwenyezi Mungu anajieleza Yeye kama Mwenye Rehema kama mara mia sita hivi kwenye Qur`ani na halafu sifa zingine za Mwenyezi Mungu zimetajwa mara chache. Mathalani, ujuzi wa Mwenyezi Mungu ni sifa ambayo imesisitizwa ndani ya Qur`ani pamoja na kwamba imetumika mara mia mbili. Sifa kama uwezo na uadilifu zote zinafuata baadaye.

Majina ya *Rahman*, *al-Rahim*, *Khayr al-Rahimin*, *Arham al-Rahimin*, *Dhu'l-Rahmah*, na *Dhu Rahmat-in Wasi`ah* ni majina kadhaa ya Mwenyezi Mungu ambayo yanarejelea kwenye rehema Yake, na kuifanya ndio sifa inayotajwa mara nyingi sana ndani ya Qur`ani.

⁴ Taz. “Image of God in the Qur’ani,” (Sura ya Mwenyezi Mungu ndani ya Qur’ani) katika kichwa: *God; Existence na Attributes* (Uwepo na Sifa) cha Mohammad Shomali Ali na Mahnaz Hedapuur, kilichohaririwa na M.A. Shomali, London, 2008 Islamic Centre of England.

Al-Rahman

Sifa ya *al-Rahman* (Mwingi wa Rehema) imetajwa mara 122 ndani ya Qur`ani pamoja na sifa zingine ambazo zikijumuishwa na zile mara 49 ambazo zimetajwa tofauti itakuwa sifa hii imetajwa mara 171. Inapaswa kuzingatiwa pia kwamba *al-Rahman* inatumika kama Jina mbadala la Allah. Mwenyezi Mungu anazo nomino sahihi mbili ndani ya Qur`ani: *Allah* na *al-Rahman*. Mwenyezi Mungu Anasema:

فُلِّ ادْعُوا اللَّهَ أَوْ ادْعُوا الرَّحْمَنَ مَثَيِّأً مَا تَدْعُوا فَلَهُ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ

“Sema: Muombeni Mwenyezi Mungu au muombeni Rahmani kwa jina lolote mnalomwita, kwani ana majina mazuri.”
[17:110].

Palikuwepo na mgogoro wakati wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) wa iwapo kama iruhusiwe au isiruhusiwe kumuita Mwenyezi Mungu `Allah`, `al-Rahman, `au jina lingine. kwenye aya hii, Mwenyezi Mungu ametupatia uchaguzi wa kumwita; ni lazima iwe ni kati ya majina hayo mawili. Hii inaashiria kwamba mionganini mwa majina yote ya Allah, katika mfuatano wao ni la *al-Rahman* tu ndilo linalofuata baada ya Allah na majina mengine yanakuja kwa umuhimu pungu-fu na hurejelea kwenye baadhi ya sifa za Mwenyezi Mungu badala ya kurejelea kwenye uhalisia Wake wote.

Huko nyuma imetamkwa kwamba wakati mwiningine *al-Rahman* ni sifa ambayo imetumika pamoja na sifa zingine au

majina mengine. Mathalani, *al-Rahman* imetumika pamoja na *Allah* na *al-Rahim* mara 114 ndani ya Qur`ani kama inavyoonekana kwenye aya:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

**“Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwene
nye Kurehemu.”**

Kila Sura ndani ya Qur`ani hufunguliwa na maneno hayo isipokuwa Sura ya Tisa (*Tawbah*). Hata hivyo, kwa sababu kifungu hiki cha maneno kimetumika mara mbili katika Sura ya 27 (*an-Naml*: Mchwa) maneno haya yamerudiwa sawa na idadi ya Sura zote ndani ya Qur`ani, yaani mara 114.

Kufuatana na Madhehebu ya Ahlul Bayt (a.s.), kuju-muishwa kwa maneno haya mwanzoni mwa Sura ina maana kwamba inahesabiwa kuwa ni sehemu yake. Vinginevyo ingemaanisha kwamba hayakuwa sehemu ya Sura hizo na kwamba yalifunuliwa mara moja na yakawavutia watu, au Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) alisema maneno hayo yalikuwa mazuri na hivyo yawekwe mwanzoni mwa kila Sura. Kwa mujibu wa Madhehebu ya Ahlul Bayt (a.s.) aya hii iliterem-shwa na kila Sura isipokuwa Sura ya *Tawbah*. Hii inaonyesha umuhimu wake; Mwenyezi Mungu aliiteremsha aya hii mara 114 kwa lengo la kusisitiza ujumbe uliomo. Katika riwaya kutoka kwa Imam Sadiq (a.s.), ni kwamba aya hii imetambulishwa kama aya muhimu sana ya Qur`ani (*a`dham ayat*) am-bayo kwa bahati mbaya Shetani ameweza kuiiba kutoka kwa

watu na hapo ndipo wanapoacha kuisoma wanaposoma Sura ya pili katika kila swala.

Hata hivyo, maneno haya yanaonyesha kwamba miongoni mwa sifa zote mbalimbali na majina ya Mwenyezi Mungu ambayo ni zaidi ya elfu moja (1000), Mwenyezi Mungu amependelea kuelezewa kwa namna hii: *al-Rahman al-Rahim*. Angeweza kutumia sifa nyinginezo nyingi, kwa mfano `Mwingi wa Kusamehe,` `Muweza wa Yote` lakin rehema Zake zinazidi sifa zingine kwani zipo karibu mno na dhati Yake halisi. Inapaswa izingatiwe kwamba hata mwanzoni mwa Sura ya Tisa ambapo msisitizo wa rehema ya Mwenyezi Mungu haiwezi kukidhi lengo la kuwaonya wapagani, Mwenyezi Mungu hafurahi Yeye ku-jitambulisha kwa njia tofauti kwa kutaja majina mengine isipokuwa *al-Rahman al-Rahim*. Hii inapendekeza kwamba ama Mwenyezi Mungu hujitambulisha Yeye kama Mungu ambaye ni *al-Rahman al-Rahim* au hupendelea kutokusema chochote.

Sura ya al-Fatihah (Kifunguzi), ambayo ni Sura muhimu sana hivyo kwamba Waislamu hawawezi kumuomba Mwenyezi Mungu bila kuisoma katika kila swala wanazosali mara tano kila siku, sio tu mwanzo wa Qur`ani bali kwa namna fulani ni mukhtasari wa Qur`ani yote.⁵ Kwenye sura fupi

⁵ Kwa mujibu wa hadithi nyingi za kuaminika, hapawezo kuwepo na swala ya kila siku bila ya kusoma Sura ya Kwanza. Mathalani, tunasoma kwenye baadhi ya hadithi (maneno ya Kiarabu). Ikielezea hukumu kuhusu usomaji wa Sura za Qur`ani wakati wa swala. Ayatollah Khomeini ameandika hivi kwenye kitabu chake kiitwacho "*Tahrir al-Wasilah*" Juz. ya 1. uk. 147:

Mas'ala ya kwanza: Ni wajibu wa lazima kusoma *Surat al-Fatihah* (Sura ya 1 ya Qur`ani) halafu ndiyo zisomwe Sura zingine kamili kwenye Rak`at (Rakaa) ya kwanza na ya pili za swala za faradhi za kila siku.

kama hiyo Mwenyezi Mungu anataka kutupatia ufupisho wa yote yale tunayoyahitaji katika maisha yetu: mukhtasari wa Uislamu na mukhtasari wa Qur`ani. Inaanza hivi:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ الرَّحْمَنُ الرَّحِيمُ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, Mola wa viumbe. Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu.....”

Sura al-Fatiha 1:1-3

Wakati wowote inapotokea ufinyu wa nafasi kwa kawai-da mhusika hujaribu kuepuka kurudia mambo. Hata hivyo, kwenye mpito mfupi kama huu, ni muhimu sana kwamba Mwenyezi Mungu anaona ni muhimu kukirudia kifungu hicho cha maneno `Mwingi wa rehema, Mwenye kurehemu` kwa sababu kama mtu hakumbuki kwamba Yeye (Mwenyezi Mungu) ni Mwingi wa kurehemu, basi huyo

Katika mzingira fulani mtu anaruhusiwa kutokusoma Sura nyingine baada ya kusoma Sura ya Kwanza. Bali hilo ni wajibu endapo muda wa swala ni mfupi au kama kuna hofu au jambo lolote mithli ya hayo ambalo ni mionganoni mwa masuala muhimu ...

Mas'ala ya Pili: Ni faradhi kusoma *Surat al-Hamd* kwenye swala za zaidi ya kiwango (*supererogatory*) kama ilivyo kwenye swala za faradhi za kila siku, kwa hali ya kuwa ni sharti la usahihi wake. Kuhusu kusoma Sura ya pili (kwenye sala za zaidi ya kiwango), si faradhi, isipokuwa pale swala inapokuwa ya faradhi kwa sababu zingine kama nadhiri au kitu kinachofanana na hicho. Bila shaka, kuhusu baadhi ya swala za kuzidi kiwango ambamo baadhi ya Sura maalum zimetajwa, kusomwa kwa Sura hizo maalum itakuwa ni sharti la kukamilika kwa kiapo, lakini lazima ifahamikke kwamba kusomwa kwao ni sharti la ukamilifu wa kiapo, lakini si kama faradhi ya kidini, au kwa ajili ya usahihi wake.

atakuwa hawezi kuelewa sawasawa jinsi Mwenyezi Mungu anavyotekeleza Mamlaka Yake hapa duniani na Akhera. Kwa hiyo, katika Sura hii, Mwenyezi Mungu kwanza ametaja rehema Yake mara mbili halafu amezungumzia kuhusu Mamlaka Yake hapa duniani. Halafu tena anataja rehema Yake mara mbili halafu ndiyo anazungumzia ufalme Wake huko Akhera. Kwa hiyo, kabla na baina ya kutukumbusha sisi kuhusu Mamlaka Yake hapa duniani na ufalme Wake huko Akhera, Allah swt anatukumbusha sisi kuhusu rehema Yake.

Al-Rahman na *al-Rahim* ni sifa zinazoonekana pamoja kwenye Sura zingine pia, kama Sura ya Fussilat [41], aya ya 2, Sura ya Baqarah [2] ,aya ya 163 na Sura ya Hashr [59], aya ya 22. Pia imetajwa pamoja na *al-Mustā`an* (yule ambaye msaada wake unatafutwa) [29:112]. Kwenye Sura ya Naba` [78], aya ya 37, Mwenyezi Mungu ametumia *al-Rahman* pamoja na *Rabb*, yaani Mola.

رَبُّ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَمَا بَيْنَهُمَا الرَّحْمَنُ

“Mola wa mbingu na ardhi na vilivyomo kati yake, Mwingi wa rehema.....” [78:37]

Hivyo, kila kitu katika dunia hii kilianza kwa rehema Yake. Viumbe na mwendelezo wao, na Akhera vyote vinategemea hiyo. Sura ya Hamd yenye we ni ushahidi mkubwa kuhusu umuhimu wa rehema ya Mwenyezi Mungu.

Al-Rahim

Jina linalofuata ni *al-Rahim* [au kwa urahisi Mwenye Rehma]. Jina hili limetajwa mara 227 ndani ya Qur`ani. Limetumika mara 226 kama jina la Mwenyezi Mungu na kwa Mtume Muhammad (s.a.w.w.) limetumika mara moja. Katika lugha ya Kiarabu, *Rahim* na *al-Rahman* yote mawili ni vivumishi na yamechukuliwa kutoka kwenye kiini kimoja ‘rahmah.’ Kwa hiyo swalii linajitokeza: Kuna tofauti gani baina ya *al-Rahman* na *Rahim*? Tukitumia Qur`ani na hadithi kuwa ndiyo vyanzo vyake, wanazuoni wa Kislamu wanatuhakikishia kuwa *al-Rahman* limetumika kama kivumishi na nomino sahihi kwa Mwenyezi Mungu. Linapotumika kama kivumishi, lina rejelea kwenye rehema ambayo inakusanya kila kitu: yaani wanaoamini na wasioamini, binadamu, na viumbe vinginevyo hapa duniani na Akhera. Hata hivyo, *Rahim*, linaashiria rehema maalum ya Mwenyezi Mungu kwa watu wema.

Kwa njia hii, tunaelewa kwamba Mwenyezi Mungu anazo aina mbili za rehema; aina moja inakumba kila kitu na kila mtu hata wale ambao ni watenda maovu, na rehema ya pekee iliyotengwa kwa ajili ya watu wanaoamini kutegemea na wema wao na sifa zao. Kwa hiyo, watu wema na waovu havwako sawa pamoja na kwamba wote wanapata rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu bila ya rehema yake Mwenyezi Mungu, hakuna kinachoweza kuwepo.

Kwa kawaida fungu la maneno, بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ hutafisiriwa “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa huruma, Mwenye kurehemu” au “Mwingi wa ukarimu, Mwenye rehema. Hata hivyo, kwa kuwa hizi sifa mbili zote zimechukuliwa kutoka kwenye asili moja, ili kuwa sahihi, tunaweza kutafsiri

ifuatavyo: "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye rehema, Mwenye kurehemu mno." Na kuwa sahihi zaidi vilevile tunaweza kusema "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, ambaye ana rehema juu ya kila kitu na anayo rehema maalum kwa ajili ya watu wema."

Khayr al-Rahimin

Kwenye aya ya 109 na 118 Sura ya 23, Mwenyezi Mungu ameelezewa kama *Khayr al-Rahimin*. Kwa mfano, Mwenyezi Mungu anasema:

وَقُلْ رَبِّ اغْفِرْ وَارْحَمْ وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ

"Na sema: Mola wangu! Samehe na Rehemu, nawe ndiye Mbora wa wanaorehemu." [23:118]

Kwa mfano, unaweza kufikiria akina mama walivyo na huruma ingawaje hapana hata mmojawao anayeweza kul-iganishwa na Mwenyezi Mungu, ambaye huruma yake imezidi huruma ya kila mtu. Ukimchukulia mama ambaye anahuruma sana hapa duniani ikilinganishwa na huruma ya Mwenyezi Mungu hali yake hiyo inafananishwa na tone moja likilinganishwa na bahari.

Inawezekana umewahi kusikia kisa cha mtu mmoja katika kipindi cha Nabii Musa (a.s.) ambaye alikuwa na mama yake ambaye alikwisha kuwa mzee sana na akawa amem-choka. Hatimaye, aliamua kumuondoa kwa kumpeleka mlimani na kumuacha huko ili asiweze kurudi tena nyumbani.

Pamoja na huruma na upendo aliopata mtu huyo kutoka kwa mama yake lakini yeye hakumhurumia mama yake, akamfanyia hivyo alivyofanya. Alipokuwa anaondoka pale mlimani giza lilikwishaanza. Mwenyezi Mungu alimfahamisha Nabii Musa (a.s.) kuhusu mama kizee huyo na akamuamuru aende kumtembelea. Wakati Nabii Musa (a.s.) alipokaribia alipokuwa mama huyo alimsikia akiomba, "Ewe Mwenyezi Mungu! Giza linaingia ambapo mwanangu anarudi nyumbani. Tafadhali nakuomba umlinde asije akapata matatizo." Mama ambaye alinyanyaswa na mwanawe bado alimwombea mwanawe huyo badala ya kumlaani. Halafu Mwenyezi Mungu alimfahamisha Nabii Musa (a.s.) kwamba upendo Wake kwa waja wake ni mkubwa zaidi kuliko ule wa yule mama kwa mwanawe.

Kwa hiyo, kamwe tusije tukafikiria kwamba Mwenyezi Mungu anapowaadhibu waovu ni kwa sababu ya ghadhabu Zake au tamaa ya kutosheleza hasira Yake kulipa kisasi. Hapana! Hata adhabu Yake huweza kutokana na huruma Yake. Kwa kweli, si Mwenyezi Mungu anayehusika na adhabu tunazopata. Adhabu zinatokana na kujikosea sisi wenyewe. Huruma ya Mwenyezi Mungu ni kubwa zaidi kuliko ya yeyote yule awaye.

Kwenye riwaya nyingine, upendo wa baba umelinganishwa na upendo wa Mwenyezi Mungu. Nabii Yakub (a.s.) alikuwa na watoto kumi na mbili na yeye kama Mtume ali-jua kwamba alitakiwa kuonyesha mapenzi sawa kwa watoto wake wote. Hata hivyo, moyoni mwake, Yakub alikuwa na mapenzi ya pekee kwa Yusuf, kwani Yusuf alikuwa mtoto maalum. Yusuf hakuwa mwanawe tu. Alikuwa mja mteule wa Mwenyezi Mungu. Yakub hakumpenda kama mwanawe

tu. Alimpenda Yusuf sana hivyo kwamba Yusuf alipoondolewa kutoka kwake alipatwa na upofu wa macho. Qur`ani inasema:

وَتَوَلَّ إِنْهُمْ وَقَالَ يَا أَسَفَىٰ عَلَىٰ يُوسُفَ وَابْيَضَتْ عَيْنَاهُ مِنَ الْحُزْنِ فَهُوَ
كَطِيمٌ قَالُوا تَالَّهِ تَقْتُلُنَا تَذْكُرُ يُوسُفَ حَتَّىٰ تَكُونَ حَرَضاً أَوْ تَكُونَ مِنَ الْهَالَكِينَ
قَالَ إِنَّمَا أَشْكُو بَثِّي وَحُزْنِي إِلَى اللَّهِ وَأَعْلَمُ مِنَ اللَّهِ مَا لَا تَعْلَمُونَ

“Na akajitenga nao, na akasema; Ah majonzi yangu juu ya Yusuf, na macho yake yakawa meupe kwa huzuni ali-yokuwa akiizua. Wakasema: Wallahi, hutaacha kumkumbuka Yusuf hata utakuwa mgonjwa au utakuwa mionganini mwa wenyewe kuangamia. Akasema: Hakika mimi nashitakia masikitiko yangu na huzuni yangu kwa Mwenyezi Mungu, na ninajua kwa Mwenyezi Mungu msiyoyajua.”

[12:84-86]

Akiwa Nabii wa Mwenyezi Mungu, Yakub alikuwa na uvumilivu mkubwa na alipoambiwa na kaka zake Yusuf kwamba Yusuf ameuawa na mbwa mwitu alisema atakuwa na “subira nzuri sana.” Lakini bado alikuwa na machungu makubwa sana hivyo kwamba mwili wake haukuweza kuvumilia na akawa kipofu. Hadithi inasema kwamba mapenzi ya Mwenyezi Mungu kwa waja Wake ni mara sabini (70) zaidi ya yale ya Yakub. Inapasa izingatiwe kwamba sabini hapa haimukaanishwa kuwa ni tarakimu tu. Kwa Kiarabu, tarakimu saba (7) na sabini (70) mara nyingi hutumika kuashiria wingi wa ziada. Kwa hiyo, huwezi kulinganisha huruma Yake na huruma ya mwingine yejote hata kama ni baba kama Yakub. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qur`ani **“Nawe ndiye Mbora wa wanaorehemu” [23:118]**

Arham al-Rahimin

Katika aya nyingine nne Mwenyezi Mungu anasema kwamba Yeye ni *Arham al-Rahimin* ambayo maana yake ni kwamba mwenye huruma zaidi sana miongoni mwa wote wenyе huruma. Kwa hiyo, si tu kwamba Yeye ni mbora wa wenyе huruma wote, Yeye ni mbora zaidi kabisa wa wenyе huruma. Kwa mfano, Qur`ani inasema:

قَالَ رَبُّ اغْفِرْ لِي وَلَاخِي وَأَدْخِلْنَا فِي رَحْمَتِكَ ۖ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ

“Akasema (Musa) Mola wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu, na utuingize katika rehema yako, wewe ndiyе Mwenye kurehemu zaidi kuliko wenyе kurehemu.” [7:151]

وَأَئِيوبَ إِذْ نَادَى رَبَّهُ أَنِّي مَسَنِيَ الظُّرُورُ وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ

“Na Ayubu, alipomwita Mola wake ya kwamba imenigusa dhara nawe ndiyе unayerehemu zaidi kuliko wanaorehemu.” [21:83]

Tukitafakari juu ya haya majina mawili yaani Mbora wa wanaorehemu na Mwenye kurehemu zaidi kuliko wenyе kurehemu, tunatambua kwamba kuhusu huruma, ili iwe bora zaidi inatakiwa kuonyesha kivitendo huruma zaidi. Hii haihusu sifa au vitendo vingine. Kwa mfano, hatuwezi kusema kwamba mama bora zaidi ni yule ambaye ni mama zaidi

au ambaye anao watoto wengi zaidi au kwamba mwandishi bora ni muhimu awe ni yule anayeandika zaidi.

Dhu `l-Rahmah na Dhu Rahmat-in Wasi`ah:

Mwenyezi Mungu ameelezewa kwenye Qur`ani mara mbili kama *Dhu `l-Rahmah* ikiwa na maana ya Mmiliki au Mgawaji wa rehema:

وَرَبُّكَ الْغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ إِنْ يَشَاءُ يُذْهِبُكُمْ وَيَسْتَخْلِفُ مِنْ بَعْدِكُمْ مَا يَشَاءُ كَمَا أَنْشَأَكُمْ مِنْ ذُرِّيَّةٍ قَوْمٍ آخَرِينَ

“Na Mola wako ndiye Mkwasi, Mwenye rehema. Kama akita-ka atakuondoeni na kuweka wengine awatakao baada yenu kama vile alivyokuumbeni katika uzazi wa watu wengine.”

[6:133]

وَرَبُّكَ الْغَفُورُ ذُو الرَّحْمَةِ صَلَوْ يُؤَاخِذُهُمْ بِمَا كَسَبُوا لَعَجَلَ لَهُمُ الْعَذَابَ بَلْ لَهُمْ مَوْعِدٌ لَنْ يَجِدُوا مِنْ دُونِهِ مَوْئِلاً

“Na Mola wako ndiye Mwingi wa kusamehe, Mwenye kure-hemu, kama angewatesa kwa sababu ya yale waliyoyachuma, bila shaka angewapa adhabu upesi upesi, lakini wanayo mia-di ambayo hawatapata kimbilio kuepukana nayo.” [18:58]

Pia Mwenyezi Mungu ameelezewa mara moja kwenye Qur`ani kama *Dhu Rahmat-in Wasi`ah* ikiwa na maana ya ‘Mmiliki na Mgawaji wa rehema kwa viumbe vyote.’ Qur`ani inasema:

فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ رَبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَاسِعَةٍ وَلَا يُرَدُّ
بَأْسُهُ عَنِ الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ

“Kama wakikukadhibisha, basi waambie! Mola wenu ni
Mwenye rehema nyingi na adhabu yake haizuiliwi kwa
watu waovu.” [6:147]

**Rehema ya Mwenyezi Mungu (swt), kama lengo la
Uumbaji Wake:**

Ndani ya Qur`ani, Mwenyezi Mungu anataja leng o Lake
la kuumba ulimwengu. Sababu hizi zinaweza kuelezeza ka-
tika mpangilio wa mfumo wa tabaka:

1. Kumwabudu na kumjua Yeye: Qur`ani inasema:

وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّا وَالْإِنْسِنَ إِلَّا لِيَعْبُدُونَ {56}
ما أَرِيدُ مِنْهُمْ مِنْ رِزْقٍ وَمَا أَرِيدُ أَنْ يَطْعَمُونَ

“Na sikuumba majinni na watu ila wapate kuniabudu.
Sitaki kwao riziki wala sitaki wanilishe.” [51:56-57]

Yeye hataki kuabudiwa kama watu walivyokuwa wa-
naabudia masanamu. Walikuwa na desturi ya kutoa maka-
fara (tambiko) au chakula kwa miungu yao. Mwenyezi
Mungu hahitajii ibada yetu. “Kuniabudu Mimi” maana yake
ni “muweza kunijua Mimi” na hatimaye “kuwa karibu Nami.”
Kama Imam Sadiq (a.s.) alivyo mnukuu Imam Husayn (a.s.)
amesema:

أيها الناس ان الله جل ذكره ما خلق العباد الا
ليعرفوه ، فاذا عرفوه عبده ، فاذا عبده استغنو
عبادته عن عبادة ماسواه

“Kwa hakika Mwenyezi Mungu Muweza wa Yote hakuwaumba waja Wake isipokuwa kwa ajili ya kumjua Yeye hivyo kwamba wakishamjua Yeye watamwabudu Yeye. Watapomwabudu Yeye hawatahitaji kumwabudu mwingine yeote yule. [Al-Mizan, Juz. 18, uk. 390]

Mahali pengine, Qur`ani inataja ukweli kwamba Mwenyezi Mungu ameuumba ulimwengu ili umtambue Yeye:

اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ وَمِنَ الْأَرْضِ مِتْهَنٌ
يَنَزِّلُ الْأَمْرَ بَيْنَهُنَّ لِتَعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ
قَدِيرٌ وَأَنَّ اللَّهَ قَدْ أَحَاطَ بِكُلِّ شَيْءٍ عِلْمًا

“Mwenyezi Mungu ni yule ambaye ameziumba mbingu saba na ardhi mfano wa hizo, amri zinashuka baina yao, ili mjue kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu, na kwamba Mwenyezi Mungu amekizunguka kila kitu kwa elimu.” [65:12]

Katika aya hii, elimu na uwezo wa Mwenyezi Mungu ni sifa zinazotajwa pamoja. Kuweza kuwa Mola wa ulimwengu, Mwenyezi Mungu anahitaji uwezo na elimu. Kama Yeye si mwenye elimu na uwezo, Hawezi kuendesha dunia.

2. Kutoa na kudhihirisha rehema Yake:

Qur`ani inaonyesha hoja nzuri sana kuhusu utoaji wa rehema. Mwenyezi Mungu aliumba ulimwengu kwa sababu anataka kugawa rehema Yake:

وَلَوْ شَاءَ رَبُّكَ لَجَعَلَ النَّاسَ أُمَّةً وَاحِدَةً^{صَطَّ} وَلَا يَزَالُونَ
مُخْتَلِفِينَ إِلَّا مَنْ رَحِمَ رَبُّكَ وَلِذَلِكَ خَلَقُهُمْ قَدْ^{قَدْ} وَتَمَّ
كَلِمَةُ رَبِّكَ لَأَمْلَأَنَّ جَهَنَّمَ مِنَ الْجِنَّةِ وَالنَّاسِ أَجْمَعِينَ

**“Na kama Mola wako angelipenda bila shaka angeliwafanya
watu kuwa umati mmoja, na wataendelea kukhitilafiana.
Isipokuwa yule ambaye Mola wako, amemrehemu, na kwa
(rehema) hiyo amewaumba. Na limetimia neno la Mola
wako, lazima nitajaza Jahannam kwa majinni na watu.”**

[11:118-119]

Mara nyingi watu hupoteza muda na nguvu zao kwa kupingana wao kwa wao isipokuwa wale ambao wamepokea rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Watu hawa wameitambua haki na hawapingani kuhusu hilo. Wanachofanya wao ni kujikita kwenye haki hiyo na kama watu wote tungefanya hivyo, hapangekuwepo na haja ya migogoro kama Mwenyezi Mungu asemavyo kwamba Ametuumba sisi ili aturuzuku rehema.

Jifikirie wewe kama mwalimu bora na unaipenda kazi yako na hutaki kuwafundisha wale tu ambao wanakuja kwa-koko na kukuomba uwafundishe. Wewe ungetoka uende kuwatafuta watu na kuwapa ujuzi wako. Ungejaribu kuwapata wanafunzi hata kama hawangekuwa na mvuto wa kujifunza.

Ungesema kwamba ultaka kuwafundisha si kwa sababu ultaka kipato isipokuwa kwa sababu wewe unapenda kufundisha. Au tuchukulie kwamba wewe ni daktari bora na mwenye kuwajibika ambaye anapenda kazi yake na hafanyi kazi hiyo kwa sababu ya kupata fedha tu. Ungetoka na kuwatafuta wagonjwa hata kama walikuwa hawajitambui wao wenyewe binafsi, au wanaona haya kukujia kwa ajili ya matibabu, au kwa sababu hawana fedha za kukulipa wewe. Mambo hayo yote wewe usingeyajali. Ungeendelea kuwatafuta na kuwapa huduma ya matibabu kwa sababu unataka kuwasaidia. Tena, fikiria kwamba wewe ni mtu tajiri na mkarimu ambaye unataka kusaidia. Usingengojea watu waje kwako kukuomba. Badala yake wewe ungetoka na kuwatafuta watu wenyewe kuhitaji msaada ili uwasaidie.

Mwenyezi Mungu alituumba sisi sio kwa sababu sisi tulistahili kuumbwa. Pale ambapo mtu hayupo basi huwa hastahili chochote. Hatukuwa na haki yoyote Kwake ya kutufanya sisi tudai kwamba lazima tuumbwe Naye. Lakini Yeye haangalii tu kile sisi tunachostahili. Anaweza kuturuzuku na ni Mwingi wa kurehemu. Hivyo, Yeye hutengeneza furssa kudhihirisha ukarimu na alituumba sisi kwa sababu Yeye ni mrehemevu na mkarimu sana. Kama Mwenyezi Mungu asingetuumba sisi kusingekuwa na maelezo yoyote kuhusu kwa nini hatukuumbwa. Na hiyo haingekuwa kwa sababu tulistahili; kwa usahihi zaidi, ingekuwa kwa sababu hatutrajji Mwenyezi Mungu mwengine kama Yeye mwenye tabia ya huruma kama Yeye, mwenye ukarimu kama huu, mwenye uwezo kama huu, na mwenye ujuzi kama huu asiumbe. Kama daktari bora ambaye haendi kutoa msaada wake wa matibabu, mwalimu bora ambaye hatoki kwenda kutoa

mafunzo. Hili ni jambo la kishangaza lakini kama wakifanya wanayopaswa kufanya si jambo la kushangaza. Hivyo, kama Mwenyezi Mungu asingetuumba sisi, hatungekuwa na uwezo wa kumpa Yeye changamoto lakini tungestaa jabu kwamba kwa nini hakuumba. Hivyo alituumba sisi.

Imam Sadiq (a.s.) aliulizwa swal na Abu Basir kuhusu maana ya aya za 118-119 za Sura ya 11 na Imam alijibu:

خَلْقَهُمْ لِيَفْعُلُوا مَا يَسْتَوْجِبُونَ بِهِ رَحْمَتِهِ فَيْرَحْمَهُمْ

Mwenyezi Mungu aliwaumba wanadamu ili wafanye kitu cha kuwafanya wastahili rehema Yake na halafu angewapa rehema Yake. [Al-Tawhid cha Saduq, uk. 404]

Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu alitaka kuwapa watu fursa ya kufanya matendo mema ili waweze kustahili rehema za ziada kutoka Kwake.

Sifa za Mwenyezi Mungu swt zinazofuatana za Rehema na uwemo:

Qur`ani inasema kwamba pamoja na rehema ya Mwenyezi Mungu, Yeye anao uwemo wa kufanya yote yale anayoyataka. Baadhi ya watu ni wenyewe huruma wanapokuwa hawana uwemo; lakini wanapokuwa na uwemo wanakuwa hawana huruma tena. Kwa kweli, mojawapo ya njia za kupima uaminifu wa mtu ni kuona atafanya nini anapokuwa tajiri au mwenye mamlaka. Madhali mtu ni fukara na mnyonge, anaweza kuwa na tabia ya urafiki lakini akishakuwa ameimarika anaweza kusahau. Mwenyezi Mungu ni mwenye rehema na mwe-

nye nguvu. Nguvu Zake hazimbadili Yeye na hana huruma kwa sababu ya unyonge. Katika aya kumi na tatu za Qur`ani, Mwenyezi Mungu anajielezea kwamba Yeye ni Muweza wa Yote (*al-Aziz*) na Mwingi wa Rehema (*al-Rahim*). Kwa mfano tunasoma:

وَإِنَّ رَبَّكَ لَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ

“Na hakika Mola wako Yeye ndiye Mwenye nguvu, mwenye kurehemu.” [26:9, 68, 104, 122, 140, 159, 175 & 191]

Kwenye msamiati wa Kiarabu cha leo maana ya `aziz ni; mpendwa, lakini kwa asili maana yake ni mwenye nguvu na asiyeshindwa kunakosababisha upenzi Wake na kuheshimika Kwake. Hapa msisitizo ni kwenye ukweli kwamba Mwenyezi Mungu anao uwezo wa kufanya atakavyo Yeye. Anapotaka kukuruzuku wewe rehema, hakuna awezaye kumzuia Yeye. Ana uwezo wa kukuruzuku wewe rehema katika hali na mazingira yoyote, ama watu wapende au wasipende. Katika Sura hiyo hiyo, Mwenyezi Mungu anasema:

وَتَوَكَّلْ عَلَى الْعَزِيزِ الرَّحِيمِ

“Na umtegemee Mwenye nguvu, Mwenye rehema.” [26:217]

Kama mtu anataka kumwamini mtu mwengine, ye ye ana hitaji kujua iwapo kama mtu huyo anayetaka kumwamini ni mwenye msaada na mwenye uwezo wa kusaidia. Hatuwezi

kumwamini mtu asiye na uwezo kufanya tunavyotaka sisi. Zaidi ya hayo, kama anao uwezo lakini hana upendo na huruma hakuna haja ya kumwamini. Kwani hatanifanyia chohote. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu ni mwenye uwezo na mwenye kurehemu pia na sisi tunapata kila sababu ya kumwamini Yeye. Ndiyo maana Qur`ani inasisitiza kuhusu ukweli kwamba wale wanaotaka kumwamini yeyote yule lazima waweke imani zao juu ya Mwenyezi Mungu. Mathalani, Mtume Yakub amenukuliwa akisema:

وَقَالَ يَا بَنِيَّ لَا تَدْخُلُوا مِنْ بَابٍ وَاحِدٍ وَادْخُلُوا مِنْ
أَبْوَابٍ مُتَفَرِّقَةٍ وَمَا أَغْنِي عَنْكُمْ مِنْ اللَّهِ مِنْ شَيْءٍ
إِنَّ الْحُكْمُ إِلَّا لِلَّهِ عَلَيْهِ تَوَكَّلْتُ وَعَلَيْهِ فَلَيَتَوَكَّلَ
الْمُتَوَكِّلُونَ

“Na akasema: Enyi wanangu! msiingie katika mlango moja bali ingieni katika milango mbalimbali, wala sikufaeni chohotembele ya Mwenyezi Mungu. Haiko hukumu ila kwa Mwenyezi Mungu tu, kwake nimetegemea, basi wategemeao na wategemee kwake.” [12:67]

Angalia pia sura 14:12 na 39:38. Qur`ani inafafanua kwamba waumini ni wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu:

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ إِذَا ذُكِرَ اللَّهُ وَجِلَتْ قُلُوبُهُمْ
وَإِذَا تُلَيَّتْ عَلَيْهِمْ آيَاتُهُ زَادَتْهُمْ إِيمَانًا وَعَلَى رَبِّهِمْ
يَتَوَكَّلُونَ

**“Hakika wenye kuamini ni wale ambao anapotajwa
Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu, na wanaposome-
wa aya zake huwazidishia imani, na wakamtegemea Mola
wao tu.” [8:2]**

Kwa kawaida, watu hawana tabia ya kuwaamini wale am-bao wamekuwa na mazoea ya maingiliano hasi nao, kama vile kuonyesha ulafi wa mali, usaliti au kusimama tu waka-ti unapohitajika msaada. Hata hivyo, hapana hata tabia mojawapo katika hizi ambayo ni sahihi kuhusu Mwenyezi Mungu. Yeye swt anakulinda na kukupenda kwa uwezo na ujuzi Wake. Hakuna sababu kwa nini tusimwamini Yeye, hu-susan tunapokumbuka yale ambayo tayari ametutendea:

وَمَا لَنَا أَلَا نَتَوَكَّلُ عَلَى اللَّهِ وَقَدْ هَدَانَا سُبُّلَانَا
وَلَنَصِرَنَّ عَلَىٰ مَا آذَيْنَا وَعَلَى اللَّهِ فَلَيَتَوَكَّلِ
الْمُتَوَكِّلُونَ

**“Na tuna nini tusimtegeme Mwenyezi Mungu na hali
tukiona kwamba ametuonyesha njia zetu? Na lazima tutaya-
vumilia mnayotuudhi, basi kwa Mwenyezi Mungu watege-
mee wenye kutegemea.” [14:12]**

Kama ilivyotajwa mapema, hapana chochote kinachowenza
kumzuia Mwenyezi Mungu anapotaka kutoa rehema:

مَا يَفْتَحُ اللَّهُ لِلنَّاسِ مِنْ رَحْمَةٍ فَلَا مُمْسِكَ لَهَا إِلَّا
يُمْسِكَ فَلَا مُرْسِلٌ لَهُ مِنْ بَعْدِهِ وَهُوَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Rehema anayoifungua Mwenyezi Mungu kwa watu, haku-na wa kuizuia, na aizuiayo hakuna wa kuipeleka isipokuwa Yeye, Naye ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima.” [35:2]

Mwenyezi Mungu anao udhibiti kamili. Pale Mwenyezi Mungu alipotaka kumsaidia Musa, pamoja na uwezo wote aliokuwa nao Firaun, hakuweza kumzuia Musa asizaliwe au asiuliwe wakati Musa alikuwa anakua. Wakati Musa alikuwa bado hana hata uwezo wa kujilinda mwenyewe, Mwenyezi Mungu alimsaidia na akamshinda Firauni, ambaye alichangia kushindwa kwake kupitia vitendo vyake mwenyewe. Ni wazi kwamba, hili hujirudia katika historia: kwani wafalme, masultani au watawala wa mabavu, madikteta; wao wenyewe ndiyo husababisha kushindwa kwao Mwenyezi Mungu anapotaka kuwapindua kama matokeo ya vitendo vyao viovu. Mwenyezi Mungu hahitaji kusimama dhidi yao na kupigana. Kwa sababu ya vitendo vyao, Mwenyezi Mungu huwanyang`anya hekima na uelewa wa ziada na halafu wanajiangamiza wenyewe. Huu ni mpangilio wa jumla. Yeyote ambaye hastahili zawadi ya Mwenyezi Mungu ya uelewa na hekima huishia katika kuijangamiza mwenyewe. Hili linaweza kutokea kwa watu binafsi, jamii ya watu, baadhi ya ustaarabu. Jambo lisilo kifani, wakati wa uhai wa Musa, Mwenyezi Mungu alimfanya adui wa Musa amuokoe Musa, na ndani ya kasri ya Faraoh, Musa alipata malezi na matunzo yote aliyoyahitaji, zaidi ya vile ambavyo wazazi wake wangemfanyia. Hata hivyo, haya hayakutokea kwa Musa tu. Inatumika kwa wote wale wanaojitahidi katika njia ya Mwenyezi Mungu, ambaye hatimae badala yake Yeye huwasaidia.

وَلَئِنْ سَأَلْتُهُمْ مَنْ خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ لَيَقُولُنَّ اللَّهُ ۚ قُلْ
 أَفَرَأَيْتُمْ مَا تَدْعُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ إِنْ أَرَادَنِيَ اللَّهُ بِضُرٍّ هَلْ هُنَّ
 كَاشِفَاتُ ضُرِّهِ أَوْ أَرَادَنِيَ بِرَحْمَةِ هَلْ هُنَّ مُمْسِكَاتُ رَحْمَتِهِ ۚ
 قُلْ حَسْبِيَ اللَّهُ ۖ عَلَيْهِ يَتَوَكَّلُ الْمُتَوَكِّلُونَ

“Na ukiwaliza: Ni nani aliyeziumba mbingu na ardhi? Bila shaka watasema: Mwenyezi Mungu. Sema: Je, mnawaon-aje wale wanaowaomba kinyume cha Mwenyezi Mungu, kama Mwenyezi Mungu akitaka kunidhuru, wao wanaweza kunirehemu, je, wao wanaweza kuzuia rehema Yake? Sema: Mwenyezi Mungu ananitosha, kwake wategeme wa-naotegemea.” [39:38]

Katika Sura ya al-Ahzab, kuonyesha zaidi rehema na ulinzi wa Mwenyezi Mungu, tunasoma:

قُلْ مَنْ ذَا الَّذِي يَعْصِمُكُمْ مِنَ اللَّهِ إِنْ أَرَادَ بِكُمْ سُوءًا
 أَوْ أَرَادَ بِكُمْ رَحْمَةً ۗ وَلَا يَجِدُونَ لَهُمْ مِنْ دُونِ اللَّهِ
 وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا

“Sema: Ni nani ambaye aweza kukulindeni na Mwenyezi Mungu kama (Mwenyezi Mungu) akikutakieni uovu, na akikutakieni rehema? Wala hawatapata mlinzi wala msaidizi kinyume cha Mwenyezi Mungu. [33:17]

Mwenyezi Mungu anatuambia kwamba Yeye ni Mwingi wa rehema na wakati huo huo rehema Yake si kwa sababu ya udhaifu Wake. Kwa kweli, Yeye ni Mwenye nguvu sana.

Anaweza kuturuzuku rehema Yake au anaweza akatunyima rehema Yake. Hapana yejote anayeweza kumlazimisha au kumzuia. Lakini mwishoni Yeye anataka kuturuzuku sisi rehema. Kama mtu hataki kukubali kupokea rehema Yake, hilo litakuwa ni tatizo lake. Hata hivyo, kwa kiasi Mwenyezi Mungu anavyohusika, Yeye hutoa. Na ametuumba sisi ili aturuzuku. Anasema kwamba Yeye hakuwa na sababu nyingne yoyote ya kutuumba sisi bali kutuonyesha sisi rehema. Yeye ni Mwenye rehema na wakati huo huo akiwa na udhibiti kamili na uwezo.

SEHEMU YA TATU

MAELEZO MAFUPI

Sehemu ya pili ya mfululizo ya makala hizi imetoa mael-ezo ya maana za sifa za Allah swt, kama vile *al-Rahman* na *al-Rahim*, ikiwa ni pamoja na zile sifa Zake zenye kuendelea kuwepo za rehema na uwezo zenye uhusiano na lengo la Allah swt katika kuumba Kwake. Ndani ya sehemu hii, sifa kama vile ukarimu Wake, kusamehe, na upole zinaelezewa pamoja na ufanuzi wa undani zaidi wa rehema Yake ikihussisha na ujuzi na ukwasi Wake.

Rehema ya Mwenyezi Mungu imejumuisha kila kitu kwani Allah swt amejilazimisha rehema kuwa wajibu juu Yake; rehema hii haiwezi kuzuiliwa na chanzo chochote na inaweza kuwakomboa watu kutokana na adhabu ya Mwenyezi Mungu. Allah swt amesitiza sana juu ya rehema Yake sio kwa sababu nyingine yoyote zaidi ya sisi kufuzu kupokea rehema zaidi na hatimaye tuwe makhalfa Wake.

UTANGULIZI

Ndani ya sehemu ya pili ya mfululizo wa makala hizi, tuliona kwamba mionganini mwa tabia na sifa za Mwenyezi Mungu zilizoonyeshwa kwenye Qur`ani, rehema Yake zaidi sana ndio imetajwa mara nyingi na kusisitizwa sana. Tayari tume-kwisha chunguza zile ambazo zinachukuliwa kutoka kwenye

kiini '*Rahman*', kama vile '*al-Rahman*', *al-Rahim*, *Arham al-Rahimin*, *Khayr al-Rahimin*, *Dhu al-Rahmah*, na *Dhu Rahmat-in Wasi`ah*. Tabia ya Allah swt kuwa Mwema, Mkarimu, Mwingi wa huruma, Mwingi wa kusamehe, Aliyetukuka, na nyingine zinatolewa kwenye sehemu hii. Zaidi ya haya, maelezo ya rehema Yake kama ilivyouniganishwa na elimu na ukwasi wake pia imeelezewa. Kwa kuzingatia sifa zilizotajwa hapo juu, Mwenyezi Muangu anawaelekeza watu kuhurumiana wao kwa wao.

SIFA ZA ZIADA ZA REHEMA YA ALLAH

al-Wadud

Mojawapo ya majina ya Mwenyezi Mungu ndani ya Qur`ani ni *Waduud*. Linatoka kwenye kiini '*wudd*' ambalo maana yake ni upendo; kwa hiyo, *Waduud* maana yake ni Mwingi wa upendo. Hili limetajwa mara mbili ndani ya Qur`ani: "Naye ni Mwingi wa kusamehe, Mwenye mapenzi." [85:14] "Na ombeni msamaha kwa Mola wenu, kisha tubuni kwake. Hakika Mola wangu ni Mwenye kurehemu, Mwenye kuwapenda." [11:90]

al-Akram

Jina lingine ni *al-Akram*. Hili limetajwa kwenye Qur`ani mara moja: "Soma na Mola wako ni Mkarimu mno." [96:3]. Hii ni mojawapo ya aya zile hasa ambazo ziliteremshwa mwanzoni mwa Uislamu.

Khayr-un Thawaab-an

Jina hili lina maana ya kwamba Mwenyezi Mungu ni mbora sana wa kutoa malipo (thawabu). Hivyo kama ukifanya kazi kwa ajili Yake, atakuwa Yeye ndiye bora wa kukulipa wewe kwa wingi. Hili limetumika mara moja ndani ya Qur`ani: "Huko ufalme ni wa Mwenyezi Mungu, Mkweli, Yeye ni Mbora kwa malipo na Mbora kwa kuleta matokeo." [18:44]

Ghaffar

Jina hili maana yake ni; Allah swt ni Mwingi wa kusamehe. Hili limetumika mara tano ndani ya Qur`ani kwa ajili ya Allah swt: "..... Ombeni msamaha kwa Mola wenu, hakika Yeye ni Mwingi wa kusamehe." [71:10]

Ahl al-Maghfirah

Jina hili maana yake ni; Allah swt ni yule ambaye tabia asilia yake ni kuwasamehe wale ambao wanastahili kusamehewa. Hili limetajwa mara moja ndani ya Qur`ani: "Na hawatakumbuka isipokuwa apende Mwenyezi Mungu, yeye ndiye Mwenye kuogopwa na Mwenye kusamehe." [74:56].

Wasi`al-Maghfirah

Jina hili lina maana kwamba Allah swt ni Mwenye ukunjufu mkubwa katika kusamehe Kwake. Hapana kitu kilichopo nje ya mipaka ya msamaha Wake. Kila jambo linaweza kusamehewa endapo mtu anaomba msamaha kwa ukweli kabisa. Hili limetajwa mara moja ndani ya Qur`ani: "Ambao wanajiepusha na madhambi makuu na vitendo vibaya isipokuwa makosa hafifu, bila shaka Mola Wako ndiye Mwenye msamaha mkubwa." [53:32]

Khayr al-Ghafirin

Yeye ni Mbora wa wale wanaosamehe. Jina hili limetajwa mara moja ndani ya Qur`ani: "Na Musa akawachagua watu sabini katika kaum yake kwa miadi yetu, na lilipowashika tetemeko (la nchi) akasema: Mola Wangu! Kama ungetaka ungelilaangamiza wao na mimi zamani. Je, unatuangamiza kwa sababu ya yale waliyoyafanya wapumbavu katika sisi? Hayakuwa haya ila ni mtihani wako kwetu, kwayo hum-poteza umtakaye na humuongoza umtakaye, Wewe Ndiye Kiongozi wetu, basi tusamehe na uturehemu, na wewe ndiye Mbora wa kusamehe." [7:155]

Kariim

Mwenye ukarimu au utukufu. Jina hili limetajwa mara mbili ndani ya Qur`ani kuhusiana na Allah swt: mara moja kama sifa ya Allah Mwenyewe: "Ewe Mwanadamu ni nini kikudanganyacho na Mola wako Mtukufu." [82:6] na lingine kama sifa ya Ufalme wake: "Basi ametukuka Mwenyezi Mungu, Mfalme wa haki, hakuna aabudiwaye ila yeye tu, Mola wa Arsh yenyeheshima." [23:116] ambapo inaweza kutafsiriwa kama 'Mwema'.

Ghafir al-Dhanb

Ni Mwenye Kusamehe dhambi. Jina hili limetumika mara moja ndani ya Qur`ani kwa ajili ya Allah swt: "Mwenye kusamehe madhambi na Mwenye kupokea toba, Mkali wa kuadhibu, Mwenye ukarimu, hakuna aabudiwaye ila yeye tu, marejeo ni kwake." [40:3]

Qabil al-Tawb

Yeye ni Mwenye kupokea toba. Jina hili limetumika mara moja kwenye Qur`ani kwa ajili ya Allah swt: “....na Mwenye kupokea toba.....” [40:3]

Dhi al-Tawl

Mwenye ukarimu. Jina hili limetumika mara moja ndani ya Qur`ani kwa ajili ya Allah swt “..Mwenye ukarimu....” [40:3]

Dhu al-Jalal wa al-Ikram

Yeye ni Mmiliki wa utukufu na ukarimu (au uadilifu). Jina hili limetajwa mara mbili ndani ya Qur`ani, mara moja kwa ajili ya Allah Mwenyewe na mahali pengine kwa ajili ya Uso Wake (*wajh*). Kuhusu Allah Mwenyewe Qur`ani inasema, “Limetukuka jina la Mola wako Mwenye utukufu na Ukarimu.” [55:78]. Hapa umetajwa mchanganyiko wa sifa mbili: ukarimu na utukufu. Sifa iliyotajwa mwanzo inahusu rehema ya Allah swt na ya mwisho kutajwa inahusu utukufu Wake.

Tawwab

Jina hili linarejelea yule ambaye humrudia Allah swt mara kwa mara. Linapotumika kwa wanadamu maana yake ni wale wanaorejea kwa Allah swt mara kwa mara kutubia, lakini linapotumika kwa Allah swt maana yake ni kwamba Yeye Allah swt hurudi kwa waja wake mara kwa mara. Kwanza huwatayarisha kwa ajili ya toba, na halafu hukubali toba hiyo wanaporudi na kutubu. Hili limetajwa kwa ajili ya Allah swt mara 11 ndani ya Qur`ani, mojawapo linasema, “...kisha

akawaelekea ili wapate kutubu, hakika Mwenyezi Mungu ndiye apokeaye toba, Mwenye kurehemu." [9:118]

Dhu al-Fadl al-Azim

Allah swt ni Mmiliki wa fadhila kubwa. Jina hili limetajwa ndani ya Qur`ani mara tatu. Kwenye mojawapo ya aya hizi, Allah swt anasema:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ تَتَقَوَّلَ اللَّهُ يَجْعَلُ لَكُمْ فُرْقَانًا
وَيُكَفِّرُ عَنْكُمْ سَيِّئَاتُكُمْ وَيَعْفُرُ لَكُمْ ۚ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ
الْعَظِيمِ

"Enyi mliaoamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atawapeni kipambanuzi na atawafutieni makosa yenu na kuwasameheni, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa."

[8:29]

Ra ùf

Allah swt ni Mpole sana. Jina hili limetajwa mara kumi ndani ya Qur`ani kwa ajili ya Allah swt Mathalani, Allah swt anasema:

هُوَ الَّذِي يُنَزِّلُ عَلَى عَبْدِهِ آيَاتٍ بَيِّنَاتٍ لِيُخْرِجَكُمْ
مِّنَ الظُّلُمَاتِ إِلَى النُّورِ ۝ وَإِنَّ اللَّهَ بِكُمْ لَرَءُوفٌ
رَحِيمٌ

“Yeye ndiye anayeteremsha Aya zilizo wazi juu ya mja wake, ili kukutoeni katika giza mwende kwenye nuru, na bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mpole kwenu, Mwenye kurehemu.” [57:9]

Ghafuur

Allah swt ni Mwingi wa rehema. Jina hili limetajwa mara 91 ndani ya Qur`ani. Mathalani, Qur`ani inasema:

وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ كَتَبَ
رَبُّكُمْ عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ أَنَّهُ مَنْ عَمِلَ مِنْكُمْ سُوءًا
بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابَ مِنْ بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Na wanapokufikia wale wanaoamini Aya zetu, basi waambie: Amani iwe juu yenu, Mola wenu amejilazimisha rehema, kwamba atakayefanya uovu kwa ujinga miongoni mwenu, kisha akatubu baada yake na akafanya wema, basi yeye ndiye Mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.” [6:54]

Dhu Maghfirah

Allah swt ni Mwingi wa kusamehe. Jina hili limetajwa mara mbili ndani ya Qur`ani:

وَيَسْتَغْلُونَكَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ وَقَدْ خَلَتْ مِنْ قَبْلِهِمْ
الْمُثُلَاثُ وَإِنَّ رَبَّكَ لَذُو مَغْفِرَةٍ لِلنَّاسِ عَلَىٰ ظُلْمِهِمْ وَإِنَّ
رَبَّكَ لَشَدِيدُ الْعِقَابِ

“Na wanakuhimiza (ulete) mabaya kabla ya mema, hali zimekwishapita adhabu za kupigiwa mfano kabla yao. Na hakika Mola wako ni Mwenye msamaha kwa watu juu ya dhulma yao, na hakika Mola wako ni Mkali wa kuadhibu.”

[13:6]

Na:

مَا يُقَالُ لَكُ إِلَّا مَا قَدْ قِيلَ لِرَسُولٍ مِّنْ قَبْلِكَ إِنَّ رَبَّكَ لَذُو
مَغْفِرَةٍ وَذُو عِقَابٍ أَلِيمٍ

“Hukuambiwa ila ni yale waliyoambiwa Mitume wa kabla yako kwa hakika Mola wako ni Mwenye kusamehe na Mwene-nye adhabu yenyen kuumiza.” [41:43]

Haliim

Allah swt ni Mwingi wa ustahimilivu ambaye husamehe vitendo vya wakosaji. Jina hili limetajwa mara 11 ndani ya Qur`ani mojawapo ya aya inasema:

تُسَبِّحُ لَهُ السَّمَاوَاتُ السَّبْعُ وَالْأَرْضُ وَمَنْ فِيهِنَّ وَإِنْ مِنْ
شَيْءٍ إِلَّا يُسَبِّحُ بِحَمْدِهِ وَلَكُنْ لَا تَفْقَهُونَ تَسْبِيحَهُمْ قَدْ إِنَّهُ كَانَ
حَلِيمًا غَفُورًا

“Zinamtukuza mbingu saba na ardhi na vilivyomo ndani yake, na hakuna chochote isipokuwa kinamsabihi kwa sifa zake njema, lakini nyinyi hamfahamu kutukuza kwao. Hakika yeche ni Mpole, Mwingi wa kusamehe.” [17:44]

Wahhaab

Allah swt ni Mpaji mkuu, Yeye ambaye hutoa baraka nyingi. Jina hili limetajwa kama sifa ya Allah swt mara tatu ndani ya Qur`ani. Mojawapo ya aya inasema:

رَبَّنَا لَا تُزِّعْ قُلُوبَنَا بَعْدَ إِذْ هَدَيْتَنَا وَهَبْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ رَحْمَةً
إِنَّكَ أَنْتَ الْوَهَابُ

“Mola wetu! Usizipotoshe nyoyo zetu baada ya kutuon-goza na utupe rehema itokayo kwako, hakika wewe ndiye Mpaji mkuu.” [3:8]

Àfiuw

Allah swt ni Mwingi wa kusamehe. Jina hili limetajwa mara tano kama sifa ya Allah swt Kwenye mojawapo ya aya hizi , Allah swt anasema,

إِنْ تُبْدِوا خَيْرًا أَوْ تُخْفُوهُ أَوْ تَعْفُوا عَنْ سُوءٍ فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ
عَفُوًّا قَدِيرًا

“Mkidhihirisha wema au mkificha au mkiyasamehe maovu, basi hakika Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe, Muweza.” [4:149]

Zipo sifa zingine kadhaa zinazohusu rehema ya Allah swt kama vile *Mujib* - Mwenye kupokea maombi,

وَإِلَىٰ ثُمُودَ أَخَاهُمْ صَالِحًاٌ قَالَ يَا قَوْمَ اعْبُدُوا اللَّهَ مَا لَكُمْ مِنْ إِلَهٍ غَيْرُهُ هُوَ أَنْشَأَكُمْ مِنَ الْأَرْضِ وَاسْتَعْمَرَكُمْ فِيهَا فَاسْتَغْفِرُوهُ ثُمَّ تُوبُوا إِلَيْهِ إِنَّ رَبِّيَ قَرِيبٌ مُجِيبٌ

“Na kwa Thamud (tukampeleka) ndugu yao, Saleh akasema Enyi watu wangu mwabuduni Mwenyezi Mungu, nyinyi hamna Mwenyezi Mungu ila Yeye tu, Yeye ndiye aliyekuum-beni katika ardhi, na akakukalisheni humo, basi muombeni msamaha, mrejee kwake. Hakika Mola wangu yu karibu na Mwenye kupokea maombi” [11:61]

Na

Hamiid

Mwenye kustahiki sifa zote njema. Jina hili limetajwa mara kumi na saba kama vile:

يَا أَيُّهَا النَّاسُ أَنْتُمُ الْفَقَرَاءُ إِلَى اللَّهِ وَاللَّهُ هُوَ الْغَنِيُّ الْحَمِيدُ

“Enyi watu! Nyinyi ndiyo wenyewe haja kwa Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ndiye Mkwasi, Mwenye kusifiwa.”

[35:15]

Na

Khayr:

Jina hili limetajwa mara 3 ndani ya Qur`ani kama vile:

إِنَّا آمَنَّا بِرَبِّنَا لِيغْفِرَ لَنَا خَطَايَانَا وَمَا أَكْرَهْتَنَا عَلَيْهِ مِنْ
السُّحْرِ ۖ وَاللَّهُ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ

“Kwa hakika tumemwamini Mola wetu ili atusamehe mako-sa yetu na uchawi uliotulazimisha kuufanya, na Mwenyezi Mungu ndiye bora na wa kudumu.” [20:73]

Na

Barr:

إِنَّا كُنَّا مِنْ قَبْلُ نَدْعُوهُ ۖ إِنَّهُ هُوَ الْبَرُّ الرَّحِيمُ

“Hakika sisi zamani tulikuwa tukimuabudu Yeye, hakika Yeye ndiye Mwema, Mwenye kurehemu.” [52:28]

Na

Salaam:

“Yeye ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hapana aabudiwaye isipokuwa Yeye tu, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye salama, Mtoaji wa amani. Mwangaliaji, Mwenye nguvu, Jabbaari, Mkubwa, Mwenyezi Mungu yu mbali na hao wanomshirikisha.” [59:23]

Na,

Quddus:

Mtakatifu, Aya [59:23] imenukuliwa hapo juu. Aya nyingine ihusuyo jina hili ni:

يُسَبِّحُ اللَّهُ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ الْمَلِكُ الْقُدُّوسُ
الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

“Vinamtukuza Mwenyezi Mungu vilivyomo mbinguni na
vilivyomo ardhini, Mfalme, Mtakatifu, Mwenye nguvu,
Mwenye hekima.” [62:1]

Na,

Khayr al-Warithiin

وَزَكَرِيَا إِذْ نَادَى رَبَّهُ رَبَّ لَا تَذَرْنِي فَرِّدًا وَأَنْتَ خَيْرٌ
الْوَارِثِينَ

“Na Zakaria alipomwita Mola wake; Mola wangu! Usiniache
peke yangu na wewe ndiye mbora wa wanaorithi.” [21:89]

Na,

Khayr-un `Uqba:

هُنَالِكَ الْوَلَايَةُ لِلَّهِ الْحَقُّ هُوَ خَيْرٌ ثَوَابًا وَخَيْرٌ عُقَبًا

“Huko ufalme ni wa Mwenyezi Mungu, Mkweli, yeye ni Mbora kwa malipo na Mbora kwa kuleta matokeo.” [18:44]⁶

Allah swt anatuhurumia sisi na Yeye anatutarajia sisi tuhurumiane sisi kwa sisi.

Mtu anaweza akaashiria kwamba Allah swt amejaribu njia mbali mbali za kutuhakikishia sisi kuhusu Rehema Yake. Kama ambavyo ametaja rehema yake mara nyingi sana, tunapaswa sisi kuwa na uhakika kabisa kuhusu rehemha hiyo.

Msisitizo wa Allah swt juu ya rehema Yake ni kwamba pia anatuambia sisi tuwe tunahurumiana. Kwa kweli ni kama anatuambia kwamba Mimi kama Mola wenu ninakuonyesheni wingi wa rehema bila ya kudaiwa au kumhitaji ye yeyote; pia nanyi mnapaswa kuwa na huruma, hususani kwa sababu ninyi kila mmoja wenu anamhitajia mwenzake na kila mmoja wenu anayo haki juu ya kila mtu mwingine. Allah swt hamhitaji ye yeyote mionganii mwetu na bado anaturehemu. Ile hali ya kutegemeana sisi kwa sisi inatupatia sababu zaidi ya kuhurumiana sisi kwa sisi. Endapo ingefikiriwa kuwa mtu mmoja ambaye angesema, “Mimi simhitaji wala sitamhitaji mtu ye yeyote na kwa hiyo sihitaji kusumbuka kujua nini kinachokutokeeni” huyo angekuwa ni Allah swt Ni Yeye tu ndiye anayeweza kusema, “Mimi si mhitaji wa kitu chochote na bado ni Mwingi wa rehema.” Kwa hiyo, ni kitu gani kinachotufanya sisi watu wahitajiao tusiwe na huruma? Baadaye tutafikiria juu ya aya ya 12 na 54 kwenye Sura ya 6 ambapo

⁶ Kwa taarifa zaidi kuhusu kundi hili na kundi jingine la sifa za ki-Mwenyezi Mungu, tafadhalii rejelea “Taswira ya Allah swt ndani ya Qur`ani” ndani ya ‘Islamic Reference Series, Juzuuz. 1, Allah: Existence and Attributes, kilichohaririwa na M. A. Shomali.

Allah swt anasema kwamba amelifanya ni suala la wajibu juu Yake kuwa Mwenye rehema.

Rehema ya Allah swt haiwezi kuzuiwa:

Endapo Allah swt anataka kumrehemu mtu, hapana mtu anayeweza kumzuia Yeye. Hata kama watu wote watakusanyika kufanya hivyo, haitaweza kutokea. Yeye ni Mwenye uwezo wa kuhakikisha kwamba rehema Yake inakufikia wewe. Mtu anakosea kutia shaka kuhusu Allah swt kama anayetaka kutoa rehema lakini anashindwa kufanya hivyo.

Rehema ya Allah swt hukunusuru wewe na adhabu:

Mojawapo ya mafundisho ya Qur`ani ni kwamba, ni kuitia rehema Yake kwamba mtu anaweza kuokolewa asiadhibiwe hapa duniani au Akhera kama ilivyoonyeshwa kwenye kisa cha Mtume Nuhu, pale mwanae alipokataa kupanda kwenye safina:

قَالَ سَأَوِي إِلَى جَبَلٍ يَغْصِمُنِي مِنَ الْمَاءِ ۝ قَالَ لَا عَاصِمَ الْيَوْمَ
مِنْ أَمْرِ اللَّهِ إِلَّا مَنْ رَحِمَ ۝ وَحَالَ بَيْنُهُمَا الْمَوْجُ فَكَانَ مِنَ
الْمُغْرَقِينَ

**“Akasema nitaukimbia mlima utakaonilinda na maji.
Akasema leo hakuna wa kulindwa na amri ya Mwenyezi
Mungu isipokuwa yule atakayemrehemu, mara wimbi-
likaingia kati yao na akawa mionganoni mwa waliogharik-
ishwa.” [11:43]**

Mtoto mwanamume wa Mtume Nuhu, badala ya kupanda safina, akakimbilia kwenye mlima na alitarajia kunusurika kufa maji. Mtume Nuhu alimuonya mwanae kwamba haku-na wa kumlinda na adhabu ya Allah swt, yaani kufa maji, na kwamba ni wale tu watakaopokea reheme Yake ndiyo watakaonusuriwa. Kwa wale wanaookolewa ni kwa sababu tu ya rehema ya Allah swt na kama watu hawajihudhurishi wenyewe kwenye rehema Yake hawataokolewa. Allah swt anatoa rehema Yake kwa kututaka tupande safina Yake ya rehema. Watu wanapaswa kutarajia ulinzi Wake ingawa mtoto wa Nuhu alikataa.

Aya nyingine ambayo imo ndani ya sura hii hii inahu su Nabii Swaleh. Pale ambapo watu wake hawakumwamini yeye na wakamuua ngamia wake Allah swt akaamua kuwaadhibu. Hata hivyo, walioamini walinusurika kwa sababu ya rehema Yake:

فَلَمَّا جَاءَ أَمْرُنَا نَجَبَنَا صَالِحًا وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَهُ بِرَحْمَةٍ مِّنْنَا
وَمَنْ خَرْقَيْ يَوْمَئِذٍ إِنَّ رَبَّكَ هُوَ الْقَوِيُّ الْعَزِيزُ

“Basi ilipofika amri yetu, tukamuokoa Swaleh na wale walioamini pamoja naye kwa rehema yetu, na pia tukawaokoa katika fedheha ya siku hiyo. Hakika Mola wako ndiye Mwene-nye nguvu, Mwenye kushinda.” [11:66]

Kwa sababu ya rehema ya kutoka Kwake, Allah swt aliwao koa. Kwa hiyo, Swaleh na wale waaminio hawakuokolewa isipokuwa kwa rehema Yake. Hii ndiyo kazi nyingine ya rehema ya Allah swt.

MAELEZO YA ZIADA YA REHEMA YA ALLAH SWT

Mwenye rehema na Mkwasi

Kwenye sehemu ya pili, tuliona kwamba Allah swt ni Mwingi wa rehema na Mwenye uwezo.⁷ Allah swt si kama wale am-bao wanapokuwa dhaifu wanakuwa wapole na wanapokuwa na uwezo hawawi hivyo. Allah swt anajieleza Yeye Mwenyewe kuwa ni mkwasi, hayupo kabisa katika kuwa mhitaji; akiwa na sifa hizi bado Yeye ni Mwingi wa rehema:

وَرَبُّكَ الْغَنِيُّ ذُو الرَّحْمَةِ إِنْ يَشَاءُ يُذْهِبُكُمْ وَيَسْتَخْلِفُ مِنْ
بَعْدِكُمْ مَا يَشَاءُ كَمَا أَنْشَأَكُمْ مِنْ ذُرِّيَّةٍ قَوْمٍ آخَرِينَ

“Na Mola wako ndiye Mkwasi, Mwenye rehema. Kama akita-ka atakuondoeni na kuweka wengine awatakao baada yenu kama vile alivyokuumbeni katika uzazi wa watu wengine.”

[6:133]

Mola wetu anajitosheleza na Mwingi wa rehema; Yeye si mhitaji ingawaje bado yu mrehemevu. Rehema yake si kwa sababu ya udhalili au matarajio Yake ya kusaidiwa mnamo siku za uso-ni. Hapo zamani hakuwa mhitaji ili atuonee huruma sisi. Zaidi ya hayo, Yeye si kama wale wanaokuwa na huruma pale tu wanapokuwa dhalili na kwa mfano, wanapokuwa hawana kazi, na hukusahau wewe mara tu wanapokuwa wakwasi.

⁷ Shomali, M. A., “Kuelewa rehema ya Mwenyezi Mungu” kwenye jarida la The Message of Thaqalayn, Vol. 12, No. 1, Issue no. 45.

Mwingi wa Rehema na Ujuzi:

Kwa mujibu wa Qur`ani, Allah swt anavyo vyote; rehema na ujuzi. Wakati fulani watu hutufanyia sisi ukarimu mkubwa sana kwa sababu hawatujui sisi ni nani, hawajui makosa yetu, mambo mabaya ambayo tumeyasema kuhusu wao au sifa gani duni tulizonazo. Kama wangejua undani wetu, wangeondoa mapenzi yao na huruma zao. 'Abd al-'Azim Hasan anasimulia kwamba Imam Jawad (a.s.) alisimulia kupitia kwa baba zake hadithi ifuatayo kutoka kwa Imam Ali (a.s.):

لَوْ تَكَافَتْ مَا تَدَافَنْتُمْ

"Kama mngejua kuhusu siri za kila mmoja wenu wala msingezikana."⁸

Kutokana na rehema Yake, Allah swt amefunika madhaifu yetu kiasi kwamba binadamu wenzetu hawajui kuhusu sifa zetu mbaya tulizonazo na matendo yetu mabaya ambayo tu-metenda. Bila shaka, mawalii wa Allah swt hawamo katika kundi hilo kwa kuwa wao ni bora zaidi kuliko watu wanavyofikiria; vinginenyo, watu wengi zaidi wanayo matatizo mengi ambayo Allah swt ndiyе tu anayeyajua na bado, Allah swt anawahurumia wao. Watu hawajui na wanaweza au wasiweze kuwa na huruma, Allah swt anajua na kwa hakika Yeye ni mrehemevu.

Ipo aya moja nzuri sana kuhusu maombi ya malaika ambayo yanathibitisha sifa hii ya rehema ya Mwenyezi Mungu.

⁸ *Bihar al-Anwar*, Juzuuy. 74, Uk. 385.

Mwanzoni mwa kuumbwa kwa mwanadamu. Malaika walishangaa pale Allah swt aliposema anataka kumteua mwakilishi wake hapa duniani. Hawakukataa. Walichofanya ni kumuuliza tu Allah swt ili wapate kuelewa:

وَإِذْ قَالَ رَبُّكَ لِلْمَلَائِكَةِ إِنِّي جَاعِلٌ فِي الْأَرْضِ خَلِيفَةً قَالُوا
أَتَجْعَلُ فِيهَا مَنْ يُفْسِدُ فِيهَا وَيَسْفِكُ الدُّمَاءَ وَنَحْنُ نُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ
وَنُقَدِّسُ لَكَ قَالَ إِنِّي أَعْلَمُ مَا لَا تَعْلَمُونَ

“Na pindi Mola wako alipowaambia Malaika: Mimi nitamweka khalifa katika ardhi, wakasema: Je, utamuweka humo atakayefanya uharibifu humo na kumwaga damu humo, na hali sisi tunakutukuza kwa sifa zako na kukutaja kwa utukufu wako? Akasema: Hakika mimi najua msiyoyajua.” [2:30]

Wakasema unataka kumteua yule ambaye atakuja kumwaga damu na kufanya uharibifu? Hapana shaka kwamba wao ha-wakuwa wanarejelea kwa Nabii Adam (a.s.) kama yeye “ndiye atakaye mwaga damu na kufanya uharibifu.” Uharibifu huo ungetokea na kuendelea kutokea ndani ya kizazi cha Adam; walijua kwamba baadhi ya dhuria wake wangemwaga damu na kufanya uharibifu, kuanzia kwa mmojawapo wa watoto wake Adam. Hatimaye, malaika waliridhika kwamba pamoja na kwamba tatizo kama hilo lipo, wanadamu wanazo baadhi ya sifa, zaidi ya zote ni uwezo wa akili ambao ndio unaowafanya wao kuwa wanastahili kuteuliwa kama makhalifa wa Allah swt

Kama wewe ungekuwa ndio malaika je, ungelipokea vipi hili? Endapo malaika hawangekuwa safi, wangeficha hisia za chuki na uhasama kwa wanadamu kwa sababu wange-

wafikiria wanadamu kama washindani wao. Wangefikiria kwamba wapo karibu sana na Allah swt, wakichukulia zile ibada zao za wakati wote na kumtukuza Allah swt kwa mfululizo. Pamoja na kwamba binadamu huyu sasa ameteuliwa kuwa kama mwakilishi wa Allah swt juu ya ardhi, malaika hawakuendekeza chuki yoyote. Kwa kweli, yale wanayoya-fanya, kama ilivyotajwa kwenye aya zifuatazo na mahali pengine ni ziada ya kumtukuza na kumsifu Allah swt (au kwa usahihi zaidi, kama sehemu ya kumtukuza kwao Allah swt, kwa sababu 'tasbih' inajumuisha kila kitu wanachofanya malaika na wakazi wengine wa mbinguni), huwaombea msamaha wanadamu. Maombi haya ya wakati wote mfululizo kwa ajili yetu kwa kweli zinaonyesha uungwana wao wa kufikiria wengine vizuri kuliko wao wenyewe. Hakuna hisia za ushindani, chuki au uhassama. Kuhusu maombi ya malaika wanaobeba Arshi Tukufu, Qur`ani inasema:

الَّذِينَ يَحْمِلُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ
 وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا وَسَعْتَ كُلَّ شَيْءٍ
 رَحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِيمُهُمْ عَذَابَ
 الْجَحِيمِ رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتٍ عَدْنَ الَّتِي وَعَدْتُهُمْ وَمَنْ صَلَحَ
 مِنْ أَبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ

"Wale wanaokichukua kiti cha Enzi na wale wanaokizunguka, wanatukuza kwa kumsifu Mola wao, na wanamwamini na wanaowaombea msamaha walioamini, Mola wetu! Umekieneea kila kitu kwa rehema na elimu, basi wasamehe waliotubu na wakafuata njia yako na waepushe na adhabu

ya Jahannam. Mola wetu na uwaingize katika Bustani za milele ulizowaahidi, na pia waliofanya mema mionganoni mwa baba zao na wake zao na watoto wao, bila shaka wewe ndiye Mwenye nguvu Mwenye hekima” [40:7-8]

Kwa hiyo, waumini wanao malaika wengi sana ambao huwaombea kwa Allah swt awasamehe. Muhimu zaidi, kwa sababu ya usafi wao, maombi yao hayakataliwi. Kwa kweli, ni kwa sababu ya rehema Yake kwamba Allah swt amewaumba malai-ka wema kama hao na amewafundisha kuomba msamaha kwa ajili yetu. Kwa hiyo, hivi inawezekana kwamba Allah swt hatawasikiliza hao? Je, Atawavunja matumaini yao? Kwa hakika hapana. Kama sisi ni waumini wa kweli na tunarudi Kwake kwa kweli na kutubu. Hatawaangusha wao au sisi.

Zaidi ya hayo, katika aya hizo hapo juu, malaika wanassisitiza kuhusu mambo mawili: Rehema ya Allah swt inayojumuisha vitu vyote na Elimu ya Allah swt inayojumuisha vitu vyote.

Rehema ya Mwenyezi Mungu inakizingira kila kitu:

Uthibitisho wa malaika kuhusu rehema ya Allah swt kuwa unazingira vitu vyote unaonekana kwenye aya zingine. Mathalani, Qur`ani inatuambia kuhusu maombi ya Musa na jibu la Allah swt:

أَنْتَ وَلِيُّنَا فَاغْفِرْ لَنَا وَارْحَمْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الْغَافِرِينَ وَأَكْتُبْ
لَنَا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ إِنَّا هُدْنَا إِلَيْكَ قَالَ
عَذَابِي أُصِيبُ بِهِ مَنْ أَشَاءَ وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ

“Wewe ndiye kiongozi wetu, basi tusamehe na uturehemu, na wewe ndiye Mbora wa kusamehe. Na utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera, sisi tunarejea kwako. Akasema adhabu yangu nitamfikishia nimirata, na rehema yangu imeenea kila kitu,” [7:155-156]

“Yeyote ninayemtaka” inarejelea kwa wale ambao kwa mfulizmo wamekuwa wakifanya matendo maovu ambayo hayakuacha hata nafasi ndogo ya msamaha. bila shaka, hii inatumika kwa aina maalum ya watu tu, lakini inapokuja kwenye rehema ya Allah swt “inakienea kila kitu.” Kwa hiyo, katika kuwaonya watu waovu, Allah swt anazungumzia kuhusu adhabu, ambapo wakati huo huo Yeye anatuhakikishia kuhusu rehema Yake inayokienea kila kitu. Kuna kisa, huenda labda cha kubuni, kuhusu msafiri wa kiroho ambaye alifanya mazungumzo na Allah swt. Kwa kumtania tu Allah swt akamwambia, “Unaonaje nikiwaambia watu kuhusu tabia yako halisi ili kwamba asitokee mtu yoyote atakayekuheshimu?” Msafiri huyo akajibu, “Unaonaje nikiwaambia watu kuhusu tabia Yako ya kweli ili kuwe hakuna mtu atakayekuhofia Wewe na ilani za maonyo Yako na kwa hiyo wawe hawatakutii Wewe.” Hadithi hii yenye msukumo wa kiroho inaonyesha kwamba kama watu walio wengi wanetambua kwa ukweli juu ya wingi wa rehema za Allah swt, kuna wasiwasi kwamba wanaweza, bada la ya kuonyesha shukurani kwa rehema Yake, watatumia nafasi hii kwa manufaa yao na kuwa wavivu na wasijali kuhusu wajibat zao. Na ndiyo maana Imam Ali (a.s.) anasema:

الْفَقِيهُ كُلُّ الْفَقِيهِ مِنْ لَمْ يُقْنِطُ النَّاسُ مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ وَلَمْ يُوَسِّعْهُمْ
مِنْ رُوحِ اللَّهِ وَلَمْ يُؤْمِنُهُمْ مِنْ مَكْرَ اللَّهِ

“Mtu anaye washauri watu wasipoteze matumaini na kutoresa imani juu ya rehema za Allah swt na wasije wakawa na uhakika sana na wakajiamini kupita kiasi kwamba wao wanayo kinga kutokana na ghadhabu na adhabu Yake; mtu huyu ana hekima sana na utambuzi mkubwa.”

(*Nahj al-Balaghah*, Semi za hekima na. 90)

Mwanazuoni wa Uislamu anayefaa ni yule ambaye hawapi matumaini sana watu hadi wakafikia kujihi sana kwamba wao wapo salama kutokana na adhabu ya Allah swt, na wala huwa hawaogopeshi sana hivyo kwamba wakapoteza matumaini. Unapaswa kuweka uwiano wa pande zote. Mtu anatakiwa asitetereke hapa duniani, ingawaje ndani ya akhera, fikira ya watu kujinufaisha na rehema ya Allah swt na kufanya maovu bila kujali haipo. Huko, uhalisia wote utadhihirika wazi na mtu ataona rehema ya Allah swt na ukunjufu wake wote ulionao. Watu ambao ndiyo tu watakaonyimwa rehema kubwa ya Allah swt ni wale ambao walichagua kutokunufaika na rehema Yake, kama vile tu vya mtoto wa Nuhu (a.s.) ambaye alikataa mwaliko wa baba yake kupanda safina ili aokolewe na rehema ya Allah swt Katika kusisitiza kuhusu ueuneaji kwa kila kitu wa rehema ya Allah swt, Qur`ani inasema:

فَإِنْ كَذَّبُوكَ فَقُلْ رَبُّكُمْ ذُو رَحْمَةٍ وَاسِعَةٍ وَلَا يُرَدُّ بَأْسُهُ عَنِ
الْقَوْمِ الْمُجْرِمِينَ

**“Kama wakikudhalilisha, basi waambie! Mola wenu ni Mwene
nye rehema nyingi na adhabu yake haizuiliwi kwa watu
waovu.” [6:147]**

Kama ungetakiwa kumpeleka mtu mcha Mungu sana na mwaminifu kuwasilisha ujumbe wako kwa watu ambao ni wadeni wako wakubwa, na badala ya kupata kukaribishwa mjumbe huyo anakataliwa na kushutumiwa kuwa mwongo, wewe ungetoa majibu gani? Unaweza kukasirika na kutumia maneno makali au kuwagomea. Hata hivyo, mambo kama hayo hayarejelei kwa Allah swt, anamwambia mjumbe wake kwamba kama wakikudhalilisha na kukushutumu wewe kwamba ni mwongo, waambie kwamba Mola wenu ni mwingi wa rehema, kwani Allah swt anawataka warejee Kwake. Kwa maneno men-gine, Allah swt anamaanisha kwamba ingawaje mmesema haya kwa Mtume Wangu, bado mnayo fursa ya kurejea, na Yeye ana shauku kuwajumuisheni nyinyi kwenye rehema Yake.

Allah swt amefanya rehema kuwa wajibu juu Yake:

Mwelekeo mwingine wa rehema ya Allah swt ambao umesisitizwa ndani ya Qur`ani ni kwamba Allah swtamefanya lazima na wajibu kwa Yeye kuonyesha rehema. Qur`ani inasema:

قُلْ لِمَنْ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ قُلْ لِلَّهِ ۚ كَتَبَ عَلَىٰ نَفْسِهِ
 الرَّحْمَةَ ۗ لَيَجْعَلَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا رَبِّ فِيهِ ۚ الَّذِينَ
 خَسِرُوا أَنفُسَهُمْ فَهُمْ لَا يُؤْمِنُونَ

“Waulize: Ni vya nani vilivyomo mbinguni na ardhini?
Sema: Ni vya Mwenyezi Mungu. Yeye amejilazimisha (kuwafanya rehema), hakika atakukusanyeni siku ya Kiyama isiyo na shaka ndani yake, wale waliojitia khasarani, basi wao hawataamini.” [6:12]

Na,

وَإِذَا جَاءَكَ الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِآيَاتِنَا فَقُلْ سَلَامٌ عَلَيْكُمْ ۖ كَتَبَ رَبُّكُمْ
عَلَىٰ نَفْسِهِ الرَّحْمَةَ ۗ أَنَّهُ مَنْ عَمِلَ مِنْكُمْ سُوءًا بِجَهَالَةٍ ثُمَّ تَابَ
مِنْ بَعْدِهِ وَأَصْلَحَ فَإِنَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Na wanapokufikia wale wanaoamini Aya zetu, basi waambie: Amani iwe juu yenu, Mola wenu amejilazimisha rehema, kwamba atakayefanya mionganoni mwenu uovu kwa ujinga, kisha akatubu baada yake na akafanya mema, basi Yeye ndiye mwingi wa kusamehe, Mwenye kurehemu.” [6:54]

Ka-ta-ba `ala asili yake ni neno `kitabah` na maana yake ni ‘kuandika’ na **ka-ta-ba `ala nafsih** maana yake ni: ‘Amejilazimishia na kuwa wajibu juu Yake.’ Hii inafanana na aya, “Enyi mliaoamini! Imekuwa ni wajibu kwenu kufunga Saumu (*kutiba `alaykum*).”

Ndani ya sura ya 6, aya ya 12, Allah swt anamwambia Mtume (s.a.w.w.) kuwa uliza watu kuhusu vitu vilivyomo mbinguni na ardhini ni vya nani. Halafu Allah swt anamwambia Mtume awape jibu hili: “Ni vyake Allah, Yeye amefanya rehema kuwa ni wajibu juu Yake.” Watu hawapaswi kuwa na wasiwasi kwa kuwa dunia hii ni ya Allah swt na si vinginevyo. Kama dunia hii ingekuwa ya watu, tungekuwa na matatizo mengi yasiyo na idadi na migogoro mingi sana; tunashukuru kwamba dunia hii ni Yake, ambaye sisi kuwa naye tumefarijika na kuburudika kwa ukamilifu na bila shaka.

Halafu Allah swt anasema kwamba kutokana na rehema Yake atatufufua na kutukusanya pamoja kutupatia maisha ya milele. Hataturuhusu sisi tuangamie kwa kifo. Ataturudisha na kutupatia rehema zaidi. Bila shaka, tunapaswa kujaribu kufanya amali njema kwenye rekodi za matendo yetu ili tuweze kufuzu kuingia mbinguni na hata kupokea rehema nyingi zaidi. Kufuatana na Qur`ani, wapo watu ambao wameangamiza nafsi zao, au kwa usahihi zaidi, ‘wamejipoteza wenyewe.’ ‘Kujipoteza mwenyewe mtu’ ni usemi mzuri sana ambao umetajwa mara kadhaa ndani ya Qur`ani. Hawa ndiyo tu watu ambao hawaamini na hawataamini kwa sababu wamechagua kuwa mbali na Allah swt na rehema Yake. Hili ni tatizo la kujitakia wao wenyewe. Kama mimi ni mtu mwema na mkarimu, wakati wa majira ya baridi ya theluji (*winter*) nitakupa mahali pa kujihifadhi, na kuwasha kiyoyozi cha joto, nitakutengenezea supu ya moto, na kukutayarishia kitanda chenye vuguvugu. Badala yake wewe unakataa kutumia ile sehemu ya kujihifadhi am-bayo nimekupa. Allah swt anapeleka watu 120,000 kukualika wewe, lakini unaamua kukataa kwenda. Unasema, “Hapa nje nipo vizuri.” Nini kitakutokea? Na nani wa kulaumiwa? Kama wewe unataka kujinyima rehema ya Allah swt, kwa nini umlaumu Yeye swt?

Kwa hiyo, Allah swt anasema kwamba amejilazimisha juu Yake kutufanyia rehema. Ni kwa sababu tu ya huruma Yake ndio amesisitiza sana juu ya Yeye kuwa mrehemevu ili sisi tuwe wenyewe kufuzu kupokea rehema nyingi zaidi na zaidi; vinginevyo, Yeye hatuhitaji sisi. Hata kama kila mtu atakengeuka, hakuna kitu kitakachomtokea Yeye. Lakini Yeye ni Mwingi wa rehema sana hivyo kwamba anasema,

Nimejilazimisha mwenyewe kuwa mrehemevu. Hii ni kwa sababu ya rehema Yake isiyokuwa na ukomo hivyo kwamba anatutendea sisi hivi kwa sababu mtu unapokua si mhitaji kwa kawaida huwa kuna uelekeo kuwasahau wengine. Angalia, kwa mfano huu, jinsi tunavyo wafanyia mchwa. Tunahisi kwamba hatuwahitaji. Hata mtu mwenye huruma hangejua afanye nini nao (isipokuwa, bila shaka kama wanafanyiwa utafiti kwa lengo la kisayansi). Ama wawe mamia au maelfu wala hutazingatia au kujali kuhusu mchwa hao kwa sababu huhitaji chochote kutoka kwao. Kama wewe si mwenye huruma unaweza hata kuwaua. Ni watu wangapi mionganini mwetu wanajishughulisha kuhusu mchwa ambao hutambaa majumbani mwetu? Inawezekana wanayo matatizo au uhaba wa chakula. Bado hatuhangaiki au kujali. Lakini Allah swt, pamoja na ukweli kwamba Yeye hahitaji chochote kutoka kwetu na kwamba umbali uliopo baina yetu na Yeye ni zaidi kuliko ule wa baina yetu na mchwa, bado moyo Wake wa kutupenda sisi hauna ukomo.

Ndani ya sura ya 6, aya ya 54, Allah swt anamwambia Mtume Wake, "Na wanapokufikia wale wanaoamini Aya zetu, basi waambie: Amani iwe juu yenu." Maana yake ni kwamba Mtume anapaswa kuwa wa kwanza kutoa salam, na kwa hakika hakuna mtu hata mmoja ambaye angeweza kumtangulia Mtume kufanya hivyo. Wakati fulani, mtu mmoja alitaka kumtangulia Mtume kutoa 'salam'; kwa hiyo, alikwenda akajificha nyuma ya ukuta na halafu akarukia kusema salam kwa Mtume. Hata hivyo, Mtume (s.a.w.w.) alipomsogelea yeye alishikwa na butwaa na hakuweza kusema. Mtume (s) alipoanzisha salam yake, mtu huyo akatulizwa. Mtume alikuwa mpole na mnyenyekemu sana

hivyo kwamba kila mara alipenda kuwa wa kwanza kutoa salam.

Zaidi ya kumwambia Mjumbe Wake kutoa salam kwa walioamini, Allaha swt Mwenyewe atatoa salam kwa walioamini huko mbinguni. Qur`ani inasema, ‘Amani!’ (Neno la salam) kutoka kwa Mola Mwingi wa Rehema” [36:58].

Kwa vyovyothe vile, Allah anasema wanapokujia wale walioamini, sema salam kwao (ambayo inaweza kuwa na maana kwamba ‘nipelekee salam Zangu kwao’) na uwape ujumbe huu kwamba “Mola wenu amejilazimisha (kukufanyieni) rehema juu Yake.” Kwa nini? Kwa sababu “kwa kweli Yeye ni Mwingi wa msamaha Mwenye rehema.” Allah swt anatuambia sisi kwamba endapo ye yote kati yenu ametenda dhambi kwa ujinga kutokana na shinikizo la tamaa na vishawishi lakin akajuta, baadaye akawa mwema, wajue kwamba Mola wao ni Mwingi wa msamaha na rehema. Kwa hiyo, mtu asije akajifikiria kwamba kwa sababu ametenda maovu mengi mno hivyo kwamba hakuna fursa ya kurudi kwa Allah swt Kama tukijutia dhambi zetu kwa kweli na kubadilika na kuwa wema, kwa hakika Allah swt atatusamehe na amelifanya ni jambo la wajibu juu Yake kufanya hivyo. Ule ujumbe ambao Allah swt anamwambia Mjumbe Wake kuuwasilisha kwa wanadamu ni kuwa wenye kuhurumiana. Kuhusu kukubalika kwa toba hasa, tunaona ujumbe unaofanana na huo kwenye aya ifuatayo:

إِنَّمَا التَّوْبَةُ عَلَى اللَّهِ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السُّوءَ
يَجْهَالَةً ثُمَّ يَتُوبُونَ مِنْ قَرِيبٍ فَأُولَئِكَ يَتُوبُ اللَّهُ
عَلَيْهِمْ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا

“Hakika toba inayopokelewa na Mwenyezi Mungu ni ya wale tu wanaofanya uovu kwa ujinga, kisha wakatubia kwa haraka, basi hao ndiyo Mwenyezi Mungu huipokea toba yao, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye hekima.”

[4:17]

Nini maana ya ‘kutubu haraka?’ Aya ifuatayo inafafanua hili:

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ حَتَّىٰ إِذَا حَضَرَ أَحَدُهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي تُبْثُتُ الْآنَ وَلَا الَّذِينَ يَمْوَلُونَ وَهُمْ كُفَّارٌ
أُولَئِكَ أَعْنَدْنَا لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا

“Na si toba ya wale ambao hufanya maovu mpaka mauti im-emfikia mmoja wao, husema: Hakika mimi nimetubia sasa, wala ya wale ambao wanakufa hali ya kuwa wao ni makafiri, wale tumewaandikia adhabu iumizayo.” [4:18]

Hii ina maana kwamba kabla kifo hakijamfika mtu, bado uwezekano wa kutubu upo; lakini toba ya mhusika wakati yupo kwenye kitanda cha mauti, atakuwa amechelewa sana. Ni hali hiyo hiyo inawapata wale wanaokufa bila imani na hutaka kuwa waumini baada ya kifo. Kwa hiyo, almuradi wewe ungali hai na afya yako njema na unaweza kufanya jambo zuri, fursa ya toba bado ipo, na Allah swt amejiwekea wajibu juu Yake kuikubali toba hiyo.

Hitimisho:

Ikizingatiwa akilini sifa nyingi za rehema ya Allah swt ndani ya Qur`ani, Allah swt anawahakikishia watu uhalisi wake ikitarajiwa kwamba sisi kama wanadamu tunatendeana hivyo. Rehema ya Allah swt haiwezi kuzuiwa mara anapochagua kutoa na tunatarajiwa kuamini kwamba hakuna kitakachotukomboa tusiadhabiwe isipokuwa rehema Yake. Rehema Yake na uwezo Wake hutokea wakati mmoja; Yeye anao uwemo kamili na hutoa upole Wake, kinyume na wale ambao huwa wema wakati huwa dhaifu na huwa kinyume chake wanapokuwa katika hali nzuri. Rehema Yake pia inalingana kwa mambo mengine na ujuzi Wake, kwani anawajua kwa kweli waja Wake, matendo yao mema na mabaya, na bado, kwa ukarimu Wake huendelea kutoa msamaha Wake na upole, ambapo kama watu wangejua dosari za wengine wangeacha kuhurumiana wao kwa wao. Zaidi ya hayo, alishaumba malai-ka ambao hawana ubinafsi ambao kwa mfululizo hutuombea. Kama tungejua rehema ya Allah swt inayojumuisha kila kitu, tungejiingiza kwenye hatari ya kutojali wajibu wetu, ambapo ndiyo maana ni muhimu kwetu sisi kwa wakati mmoja huohuo kutambua uwepo wa adhabu Yake. Tukiangalia kila kitu kwa ujumla, watu wasijifikirie kama wamefanya dhambi nyingi sana hivyo kwamba hawana nafasi ya kupata msamaha Wake usio na ukomo. Anachotakiwa kufanya mtu ni kujutia dhambi zake kwa kweli ambapo wakati huo huo akibadilika kuwa mwema, na hii inaweza kuleta wokovu, kwani Allah swt amejilazimishia wajibu wa kutuhurumia (sisi) kuwa wajibu Wake. Mtu anatarajiwa kuangalia pande zote kati ya matumaini na khofu.

Kwenye sehemu ya Nne, tutajifunza mpango ambao Allah swt ametengeneza kutohana na rehema Yake ili tuweze kuwa na maisha ya raha katika sayari hii. Vitu vingi vinatakiwa kupatikana kwa ajili yetu ili tuweze kuendelea kuishi na kufurahia maisha yetu. Halafu tutachunguza kuhusu mpango wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya mwongozo wetu ambao msingi wake upo kwenye rehema Yake.

SEHEMU YA NNE

MAELEZO MAFUPI: Kwenye sehemu iliyotangulia ya mfululizo wa makala haya, sifa za Mwenyezi Mungu, kama vile wema, usamehevu, elimu na ukwasi Wake zimeelezewa kama ziada kwa uhakikisho wa rehema inayokie-nea kila kitu aliyoifanya kuwa ni wajibu juu Yake, hususani kwa wale wenye kufuzu kuipokea katika njia yao ya kiroho. Katika sehemu hii, tutachunguza dhima ya rehema ya Mwenyezi Mungu kama inavyoonekana ndani ya Qur`ani katika kutengeneza mipango mbali mbali kwa ajili yetu sisi kuent-delea kuishi katika hali inayofaa hapa duniani, kama vile kumba nyota, kulinda mbingu, na kutuokoa sisi kutoka kwenye mabala. Rehema ya Mwenyezi Mungu pia huchukua nafasi katika mwongozo kwa wanadamu kwani Yeye aliwatumia wanadamu wajumbe wenye sifa za umaasumu na wene-ye uwezo wa kuhisi maono ya mwingine na wapole. Kwa kweli, Mwenyezi Mungu amewapa wanadamu baraka zisizo na ukomo katika vipengele vyote vya maisha yao; ni wajibu wetu kuzitambua na kuzitumia kwa busara ili tuweze kupata radhi Zake na hatimaye tuwe makhalifa Wake.

DHIMA YA REHEMA YA MWENYEZI MUNGU KATIKA MAISHA YETU YA KIDUNIA

Ndani ya Qur`ani Mwenyezi Mungu anarejelea kwenye mipango mbali mbali ambayo Ameitengeneza katika dunia hii kwa ajili ya manufaa yetu au kwa ajili ya uhai wetu. Baadhi ya mipango hiyo ni kwa ajili tu ya kufanya maisha yawe rahisi zaidi kwetu ambapo

mipango mingine ni ya muhimu. Katika haya yafuatayo, tutarejelea baadhi ya neema hizo za Mwenyezi Mungu.

Kuhifadhi mbingu na kuumbwa kwa nyota: Ikisisitiza juu ya rehema ya Mwenyezi Mungu, Qur`ani inatuambia kwamba Mwenyezi Mungu anaihifadhi mbingu kwa ajili ya kulinda dunia:

أَلَمْ تَرَ أَنَّ اللَّهَ سَخَّرَ لَكُمْ مَا فِي الْأَرْضِ وَالْفُلُكَ تَجْرِي فِي
الْبَحْرِ بِأَمْرِهِ وَيُمْسِكُ السَّمَاءَ أَنْ تَقَعَ عَلَى الْأَرْضِ إِلَّا بِإِذْنِهِ^{٢٩}
إِنَّ اللَّهَ بِالنَّاسِ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Je, hamuoni kwamba Mwenyezi Mungu amevitiisha kwa ajili yenu vilivyo ardhini, na majahazi yanayopita baharini kwa amri yake, na ameishikilia mbingu isianguke juu ya ardhi ila kwa idhini yake. Kwa hakika Mwenyezi Mungu ni Mpole kwa watu na Mwenyezi kurehemu.” [22:65]

Kwa kusema kwamba: “Je, hamuoni kwamba Mwenyezi Mungu amevitiisha kwa ajili yenu...” Mwenyezi Mungu anatutaka tuvitalie maanani vitu vyote ambavyo amevifanya kuwa vitiifu kwetu. Ametupatia uwezo wa kudhibiti vile vilivyomo juu ya ardhi na kuzitumia meli zinazotembea baharini. Juu ya hayo, Mwenyezi Mungu anaishikilia mbingu mahali pake ilipo, huizuia isianguke juu ya ardhi isipokuwa kwa amri Yake (labda hii inarejelea kwenye matukio yanayotokea kabla ya Siku ya Hukumu ambapo ardhi na mbingu zitavunjika). Mwishoni mwa aya, Mwenyezi Mungu anatukumbusha juu ya Upole na Rehema zake za hali ya juu kabisu. Pia Ameumba nyota kwa ajili ya maelekezo ya mazingira wakati wa usiku.

وَهُوَ الَّذِي جَعَلَ لَكُمُ النُّجُومَ لِتَهَدُوا بِهَا فِي ظُلْمَاتِ الْبَرِّ
وَالْبَحْرِ قَدْ فَصَّلَنَا الْآيَاتِ لِقَوْمٍ يَعْلَمُونَ

“Na Yeye ndiye aliyekuumbieni nyota ili muongoke kwazo katika giza la bara na bahari, hakika tumezichambua dalili kwa watu wanaojua.” [6:97]⁹

Kupishana kwa mchana na usiku: Endapo pasingeku-wepo na upishanaji na wakati wote tungakuwa na mchana au usiku, basi hali hii ingeathiri vibaya sana maisha yetu ya kim-wili, kisaikolojia na kiroho. Upishanaji huu ni wa muhimu kwa ajili ya utulivu wa akili na nafsi zetu. Mwenyezi Mungu ameumba muda wa usiku kimsingi kwa ajili ya mapumziko yetu. Qur`ani inasema:

وَمِنْ رَحْمَتِهِ جَعَلَ لَكُمُ اللَّيلَ وَالنَّهَارَ لِتَسْكُنُوا فِيهِ وَلِتَبْتَغُوا
مِنْ فَضْلِهِ وَلَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ

“Na kwa rehema Zake amekufanyieni usiku na mchana ili mtulie humo na mtafute fadhili Zake na ili mpate kushukuru.” [28:73]

Wakati wa mchana na wakati wa usiku ni neema mbili za Mwenyezi Mungu na tunapaswa kushukuru zaidi kwa kila mchana na usiku unaokuja. Aya hii inamaanisha kwamba watu wamepewa pendekezo kwamba wasichague aina ya kazi ambayo itafanyika usiku kucha. Bila shaka, wapo wale wanaofanya kazi usiku tu kwa manufaa ya jamii au kwa sababu ya mahitaji yao na hakuna ubaya katika hilo, kwani hawa-

⁹ Angalia pia aya ya 16:16

na njia mbadala. Hata hivyo, kama ni jambo la kuchagua ni vema zaidi kuchagua kazi ambayo inakupa fursa ya kuweza kuwa na familia yako, kufanya ibada, au kupumzika mnamo mwisho wa siku. Wakati wa usiku bila shaka ndio muda mzuri zaidi wa kupumzika. Wakati wa mchana, hata kama utajaribu kuigiza wakati wa usiku kwa kuzima taa na kuvuta pazia ili pawepo giza chumbani, bado hutapata mapumziko kama yale yanayopatikana usiku. Hili si tu suala la mwanga au giza, mazingira yote yanakuwa tofauti. Kwa kawaida sisi tunalichukulia hili kuwa la kawaida kwa vile hatuhesabu hili kama ni mali yetu ingawaje kwa ukweli halisi hizi ni rasili-mali ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu na tunapaswa kuwa na kushukurani.

Upopo na mvua: Bila ya upopo hewa inabaki imetulia tuli na hiyo inaweza kusababisha matatizo. Allah swt aliumba upopo kwa ajili ya kuboresha hewa tunayovuta kupidia kusogea kwa dunia na kuwepo kwa upopo. Kwenye baadhi ya sehemu ambapo jiji hujengwa karibu ya milima mirefu inayozuia uvumaji wa upopo, watu hupata vipingamizi kama vile kushindwa kuondoka kwenye nyumba zao kwa siku kadhaa. Kwa hiyo, wimbi hili la upopo huleta manufaa kama vile hewa safi na husaidia kusambaza mbegu kwa ajili ya utungisho wa mimea:

وَهُوَ الَّذِي أَرْسَلَ الرِّيَاحَ بُشْرًا بَيْنَ يَدَيِ رَحْمَتِهِ وَأَنْزَلَنَا مِنَ
السَّمَاءِ مَاءً طَهُورًا لِنُحْيِي بِهِ بَلْدَةً مَيْتَانَا وَنُسْقِيْهُ مِمَّا خَلَقَنَا
أَنْعَامًا وَأَنَاسِيَّ كَثِيرًا وَلَقَدْ صَرَفْنَاهُ بَيْنَهُمْ لِيَذَكُّرُوا فَأَبْيَ أَكْثَرُ
النَّاسِ إِلَّا كُفُورًا

“Naye ndiye azitumaye pepo kuwa khabari njema kabla ya (kufika) rehema yake, na tunayateremsha kutoka mawinguni maji safi. Ili kwa hayo tuihuishe nchi iliyokufa na tuwanyweshe baadhi ya tuliowaumba katika wanyama na watu wengi. Na kwa hakika tunaigawa (mvua hii) baina yao mara kwa mara ili wakumbuke, lakini watu wengi wanakataa ila kukufuru tu.” [25:48-50]

Kwa kutuma upopo huu, pia Yeye hukupatia wewe habari njema ya uwezekano wa mvua ambayo hukusafisha wewe.

Wanyama: Kutokana na rehema Yake, Mwenyezi Mungu swt ameumba wanyama, baadhi yao hutusaidia sisi kusafirisha bidhaa zetu. Kama asingeumba wanyama kama farasi, ngamia, punda, na nyumbu basi ingekuwa vigumu sana kwetu kubeba bidhaa zetu, hususani kabla ya ugunduzi wa motokaa. Labda kama hapangekuwepo na wanyama kama hao kubeba bidhaa, fikira ya kugundua motokaa isingejitokeza, kwani kwa kawaida huwa tunaunda kwa mfano wa kile kilichopo katika maumbile, kama vile ugunduzi wa ndege ambayo imeundwa kwa mfano wa viumbe ndege. Hii imepewa jina na watafiti wa elimu viumbe (*biophysicists*) kama (*biomimetics*). Kwa vyovyyote vile, Qur`ani inasema:

وَتَحْمِلُ أَنْقَالَكُمْ إِلَى بَلْدٍ لَمْ تَكُونُوا بِالْغَيْرِ إِلَّا بِشَقِّ الْأَنْفُسِ ۝ إِنَّ رَبَّكُمْ لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ وَالْخَيْلَ وَالْبِعَالَ وَالْحَمِيرَ لِتَرْكُبُوهَا
وَزِينَةٌ وَيَخْلُقُ مَا لَا تَعْلَمُونَ

“Na hubeba mizigo yenu kupeleka kwenye mji msikokuweza kufika isipokuwa kwa kujitia tabu. Hakika Mola wenu

ni Mpole sana Mwenye kurehemu. Na (amewaumba) farasi na nyumbu na punda ili muwapande na (wawe) pambo, na ataumba (vingine) msivyovijua.” [16:7-8]

Kwa hiyo kuumbwa kwa wanyama, kwa kiasi fulani maana yake ni kwa ajili ya manufaa yetu. Bila shaka, Uislamu unatoa mapendekezo na maelekezo ya jinsi ya kuwatunza wanyama hawa. Hata hadithi zimependekeza hilo, kwa mfano, kama mtu ameketi kwenye farasi au punda na halafu akakutana na rafiki yake, ni lazima yeye asianze kusema mpaka kwanza ashuke kwenye kipando chake, kwa sababu kufanya hivyo kuna maumivu kwa mnyama huyo. Au Imam Ali (a.s.) anatuambia tusiwalaani wanyama, vinginevyo wewe mwenyewe utalaanika. Pia wanyama ni budi wapewe malisho ya kutosha, hifadhi na hata madawa.¹⁰

Usafiri ndani ya bahari ndogo na bahari kuu: Kutokana na rehema Yake, Mwenyezi Mungu ametuwezesha kutengenza meli na mashua kwa ajili ya kubeba bidhaa zetu ndani ya bahari ndogo na kuu. Kama ingekuwa si kwa uwezo wa maji kuwa chombo cha kubeba bidhaa pamoja na kuwa na sifa ya kuruhusu vitu kuelea juu ya uso wake, hatungekuwa na uw-ezo wa kubeba bidhaa hizo:

رَبُّكُمُ الَّذِي يُرْجِي لَكُمُ الْفَلَكَ فِي الْبَحْرِ لِتَتَغْوِي مِنْ فَضْلِهِ إِنَّهُ
كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا

¹⁰ Kwa taarifa zaidi, tafadhali rejea kwenye makala ya Shomali, M. A., “Aspects of Environmental Ethics” in Life, London: 2011, Taasisi ya Mafunzo ya Kiislam (Institute of Islamic Studies).

“Mola wenu ni yule anayekuendesheeni majahazi katika bahari ili mtafute fadhila zake, bila shaka ye ye ni Mwenye kurehemu kwenu..” [17:66]

Ulinzi Dhidi ya Mabalaa: Ingawaje tunaona maafa yanayotokea, hatuyaoni mengi ambayo huokolewa kutokana nayo. Mathalani, Qur`ani inasema:

وَإِنْ نَشَأْ نُعْرِقُهُمْ فَلَا صَرِيخَ لَهُمْ وَلَا هُمْ يُنْقَذُونَ إِلَّا رَحْمَةً
مِنْنَا وَمَتَاعًا إِلَىٰ حِينٍ

“Na kama tungetaka tungewagharikisha, wala wasingeokolewa. Ila kwa rehema zitokazo kwetu na kuwanufaisha kwa muda kidogo.” (36: 43-44)

Endapo Mwenyezi Mungu angetaka angetugharikisha sisi sote kwenye mafuriko. Ni kwa sababu ya rehema Yake hivyo kwamba hutuokoa na kutupatia sisi uwezekano wa kuendelea kuishi.

Tunapofikiria kwa makini kuhusu uwezekano tulionao wa kifo na kuendela kuishi tangu utotonu na kuzingatia hatari na vitisho ambavyo vimetukabili tangu kuzaliwa kwetu, tunatambua kwamba fursa yetu ya kuendelea kuishi kwa kweli ni ndogo sana. Mathalani, vitisho vingi na hatari nyingi zinaweza kutokea kila siku kwa mtoto mchanga. Hebu fikiria mtoto wako awe anachezea kisu, uma, wanasesere na nyenzo zingine ndani ya nyumba, au kugusa tu vitu vyenye joto kali. Mambo mengi yanaweza kumtokea ambapo wewe mara nyingi hutaweza kuwa na udhibiti kamilifu. Au wakati tunapovuka mtaa, na watu wen-

gi huvuka mtaa kwa msingi wa mazoea, na kama mmojawapo wa madereva wengi sio muangalifu hata kwa sekunde chache tu, tunaweza kukabiliwa na lolote lisilozuilika. Kwenye barabara yanamopita magari, kama dereva mmoja tu akizembea itatokea migongano ya kufisha. Lazima pawepo na rehema ya Mwenyezi Mungu ambayo hutuokoa sisi; vinginevyo tusingeweza kuendelea na maisha yetu, au angalau hata kubakia na afya njema. Katika kubainisha rehema hiyo, Mwenyezi Mungu anaelezea uandaaji huo ndani ya Qur`ani:

لَهُ مُعَقَّبَاتٌ مِنْ بَيْنِ يَدِيهِ وَمِنْ خَلْفِهِ يَحْفَظُونَهُ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ

“(Kila mtu) ana kundi (la Malaika) mbele yake na nyuma yake, wanamlinda kwa amri ya Mwenyezi Mungu.....” [13:11]

Mwenyezi Mungu huteua malaika hasa kwa ajili ya ulinzi wetu. Wapo malaika ambao wajibu wao ni kutulinda sisi kutokana na hatari na majanga ya wakati wote tunayokabiliana nayo kila siku. Imam Baqir (a.s.) anafafanua kuhusu hii ‘amri ya Mwenyezi Mungu’

يحفظ بأمر الله من ان يقع في ركي او يقع عليه حائط ، او
يصيبه شيء حتى اذا جاء القدر خلوا بينه ، و بينه يدفعونه
إلى المقادير ، وهما مكان يحفظانه بالليل و مكان بالنهار
يتعبانه

**“Kwa maelekezo kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mtu ana-
okolewa asitumbukie kisimani au kuangukiwa na ukuta
au mabalaa kumtokea hadi hapo amri ya Mwenyezi Mungu
itakapokuja. Kwa hiyo, inapokuja amri ya Mwenyezi Mun-**

gu ataachwa na amri hiyo na atasukumwa aelekee kwenye amri hiyo. Wapo malaika wawili ambao humlinda yeye wakati wa usiku na malaika wawili wanaokuja kushika na-fasi ya ulinzi wa mchana.”¹¹

Imam Sadiq (a.s.) pia amesema:

ما من عبد إلا ومعه ملكان يحفظانه فإذا جاء الأمر من عند الله خلياً بينه وبين أمر الله.

“Hapana mja wa Mwenyezi Mungu isipokuwa wapo malaika wawili ambao wapo naye kwa ajili ya ulinzi. Amri ya Mwenyezi Mungu itakapokuja watamwacha abakie nayo amri hiyo.”¹²

Maoni kama hayo yanaweza kuonekana kwenye Nahj al-Balaghah ambamo Imam Ali (a.s.) anasema:

إن مع كل إنسان ملكين يحفظانه فإذا جاء القدر خلياً بينه وبينه.

“Kwa hakika wapo malaika wawili kwa kila mtu wanaom-linda. Amri ya Mwenyezi Mungu inapokuja humwacha nayo amri hiyo.”¹³

Kwa ujumla zaidi, Imam Ali (a.s.) anasema wapo malaika ambao kazi yao ni kuwalinda waja wa Mwenyezi Mungu¹⁴

¹¹ Tafsir Nemuneh, Juzu. 10, Uk. 144

¹² Ibid. Dondoo kutoka Al-Burhan, Juzu. 2, Uk. 283

¹³ Ibid. dondoo kutoka Nahjul-Balaghah, Semi za Hekima Na. 201

¹⁴ Ibid. dondoo kutoka Nahjul-Balaghah, Semi Namba moja.

وَمِنْهُمْ الْحَفْظَةُ لِعِبَادِهِ

Msaada na ulinzi katika masuala maalum: Pia yapo mambo maalum ndani ya Qur`ani ambamo Mwenyezi Mungu aliwasaidia na kuwalinda watu mahususi kupitia rehema Yake. Mathalan, katika kisa cha Nabii Khidr (a.s.) na Nabii Musa (a.s.), wakati Nabii Khidr alikuwa anakarabati ukuta, Musa alishindwa kuelewa ni kwa nini Khidr kufanya hivyo. Baadaye Nabii Khidr (a.s.) alieleza kwamba chini ya ukuta huo palikuwepo na hazina kwa ajili ya mayatima wawili, na Mwenyezi Mungu kwa rehema Yake alitaka hazina hiyo iendelee kubakia imezikwa pale hadi hapo wale mayatima watakapokuwa na umri mkubwa na kuitafuta wao wenyewe:

وَأَمَّا الْجِدَارُ فَكَانَ لِغَلَامَيْنِ يَتِيمَيْنِ فِي الْمَدِينَةِ وَكَانَ تَحْتَهُ
 كَنْزٌ لَّهُمَا وَكَانَ أَبُوهُمَا صَالِحًا فَأَرَادَ رَبُّكَ أَنْ يَبْلُغَا أَشْدَهُمَا
 وَيَسْتَخِرُ جَاهَنَّمَ مِنْ رَبِّكَ وَمَا فَعَلُتُهُ عَنْ أَمْرِي
 ذَلِكَ تَأْوِيلٌ مَا لَمْ تَسْطِعْ عَلَيْهِ صَبْرًا

“Na ama ukuta,basi ulikuwa wa watoto wawili mayatima mjini, na chini yake kulikuwa khazina yao,na baba yao ali-kuwa mwema kwa hiyo Mola wako alitaka wafikie balaghe yao, waitolee khazina yao. Ni rehema kutoka kwa Mola wako, nami sikulifanya kwa amri yangu, hiyo ndiyo hakika ya yale ambayo hukuweza kuyavumilia.” [18:82]

Kwa hiyo Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa rehema hivyo kwamba alimwambia Mtume Wake kufanya kazi kama kiba-

rua wa kawaida kukarabati ukuta huu bila malipo ili kwamba hawa mayatima wawili wangeiona kwa urahisi.

Mfano mwingine unahu su Nabii Zakaria (a.s.) ambaye alipewa mtoto mwanamume, Yahya kwa rehema ya Mwenyezi Mungu:

ذُكْرُ رَحْمَتِ رَبِّكَ عَبْدُهُ زَكَرِيَا إِذْ نَادَى رَبَّهُ نِدَاءً حَفِيَّا قَالَ
رَبِّ إِنِّي وَهَنَ الْعَظُمُ مِنِّي وَاشْتَغَلَ الرَّأْسُ شَيْئًا وَلَمْ أَكُنْ
بِدُّعَائِكَ رَبِّ شَقِيقًا وَإِنِّي حَفْتُ الْمَوَالِيَ مِنْ وَرَائِي وَكَانَتِ
أَمْرَاتِي عَاقِرًا فَهَبْ لِي مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا يَرِثُنِي وَيَرِثُ مِنْ آلِ
يَعْقُوبَ وَاجْعَلْهُ رَبِّ رَضِيًّا

“(Huu) ni ukumbusho wa rehema ya Mola wako kwa mja wake Zakaria. Alipomuomba Mola wake kwa maombi ya siri. Akasema: Mola wangu! Bila shaka mfupa wangu umekuwa dhaifu na kichwa kinang`aa kwa mvi wala si-kuwa mwenye bahati mbaya, Mola wangu kwa kukuomba. Na hakika mimi nawahofia jamaa zangu baada yangu, na mke wangu ni tasa, basi nipe mrithi kutoka kwako. Atakayenirithi na awarithi ukoo wa Yaakub na umfanye Mola wangu! Mwenye kuridhisha.” [19:2-6]

Pia Mwenyezi Mungu alimpa Nabii Musa (a.s.) ndugu yake, Nabii Harun ambaye alimsaidia Musa katika ufanikishaji wake:

وَوَهْبَنَا لَهُ مِنْ رَحْمَتِنَا أَخَاهُ هَارُونَ نَبِيًّا

“Nasi tukampa katika rehema zetu nduguye Harun, Nabii.”

[19:53]

Zaidi ya hayo, kupertia na rehema Yake, Mwenyezi Mungu alimpendelea Nabii Ayub (a.s.) katika mateso na matatizo yake kwa kumrudishia watu wa familia yake na wengine kama wao:

وَوَهْبَنَا لَهُ أَهْلَهُ وَمِثْلُهُمْ مَعَهُمْ رَحْمَةٌ مِنَّا وَذِكْرٌ لِأُولَئِي
الْأَلْبَابِ

**“Na tukampa watu wake na wengine kama wao pamoja nao,
kwa rehema itokayo kwetu na mawaidha kwa watu wenye
akili.” [38:43]**

Na;

فَاسْتَجَبْنَا لَهُ فَكَشَفْنَا مَا بِهِ مِنْ ضُرٌّ وَآتَيْنَاهُ أَهْلَهُ وَمِثْلُهُمْ مَعَهُمْ
رَحْمَةً مِنْ عِنْدِنَا وَذِكْرًا لِلْعَابِدِينَ

**“Basi tukamkubalia na tukamuondolea dhara alilokuwa
nalo na tukampa watu wake na mfano wa pamoja nao. Ni
rehema kutoka kwetu, na ukumbusho kwa wafanyao iba-
da.” [21:84]**

Kwa hiyo, kwa ajili ya wanadamu wote kutokana na rehema Yake Mwenyezi Mungu ametengeneza mipango kwa ajili ya manufaa, uhai, na ulinzi pamoja na mambo maalum, kwa ajili ya kila mtu, kwani Mwenyezi Mungu anathibitisha hili ndani ya Qur`ani.

Dhima ya Rehema ya Mwenyezi Mungu katika Kumuongoza Mwanadamu.

Si tu kwamba Mwenyezi Mungu ameumba dunia pamoja na sisi na kuyafanya maisha kuwa ya manufaa kwetu, lakini pia Amejaalia rehema Yake kwa kutuandalia muongozo. Hali hii inafananishwa na kuwaalika watu waje kwetu, tuwape chakula na starehe, zaidi ya hayo kupanga shughuli ya aina fulani kwa sababu bila kufanya hivyo itakuwa sawa na kupoeteza muda wao na nguvu zao. Au hebu fikiria kujengwa kwa shule, ikiwa na sehemu zote za kumwezesha mtu ajifunze kwa wepesi pamoja na maktaba na maabara pasipo na mtaala, silabasi, au waalimu. Mwenyezi Mungu ameifanya dunia hii kama shule yenye sehemu zote za kumwezesha mtu ajifunze kwa wepesi, na pia ametupatia silabasi na walimu waliobobe. Katika kufanya hivyo, Yeye anatupima sisi kwa mtihami na mwishoni, Hutupatia rekodi zetu za utendaji kwa wale waliofuzu au waliofeli.

Kumpeleka Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kama rehema:

Kufuatana na Qur`ani, Mwenyezi Mungu amewapeleka Mtume Wake kwa wanadamu kwa sababu ya rehema Yake. Mwenyezi Mungu pia anasisitiza juu ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) kuwa amepelekwa kuwasilisha ujumbe Wake wa rehema:

وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ

“Nasi hatukukutuma ila uwe rehema kwa walimwengu.”

[21:107]

Kuna njia mbili za kutafsiri aya hii: 1) Mwenyezi Mungu amempeleka yeye ili awe rehema, au 2) Amempeleka kutokana na rehema Yake. Mtu anatakiwa achukue (*rahmah*) rehema kama sababu ya kumpeleka Mtume (*maf uul li-ajlih*); mwingine aichukue kama maelezo ya kile Mtume alichotakiwa kufanya (*haal au maf uul thaani*). Matokeo hayatofautiani sana. Kwa hali yoyote ile, Mwenyezi Mungu amefanya hivi kutokana na rehema Yake na Mtume (s.a.w.w.) alikuwa pia Mtume wa rehema, ingawaje kiufundi zipo njia mbali mbali za kufikia hitimisho hili.

Hivyo, Mtume hakupelekwa kwa ajili ya watu wa Makka na wa Mashariki ya Kati tu. Wala hakupelekwa kwa ajili ya Waislamu tu waliomo duniani kote. Alipelekwa ili awe chanzo cha rehema kwa watu wote wa hapa dunuiiani, pamoja na wanadamu na majini.¹⁵ Kiumbe chochote chenye akili na uelewa kinaweza kunufaika kutoka kwake jinni huyo, hata malaika. Kwa mujibu wa hadithi, Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alimuuliza malaika Jibril:

هل أصحابك من هذه الرحمة شيء؟

“Kuna kitu chochote kutokana na rehema hii kimekufikia wewe?”

Malaika Jibril akajibu:

¹⁵ Jinni ni kiumbe asiyonekana, wa daraja la chini kuliko malaika, am-baye anaweza kutokeza kwa umbile la mnyama au mwanadamu. Kwa pamoja, jinni, mwanadamu, na malaika vinafanya viumbe vitatu vye-nye uwezo wa kuhisi katika uumbaji wa Allah swt Kama wanadamu, jinni pia linaweza kuwa jema, uovu, au lisaidie pande zote.

نعم إني كنت أخشى عاقبـه الأـمـر فـامـنـت بـك لـما اـثـنـى اللهـ عـلـيـ بـقـوـلـه : ذـي قـوـةـ عـنـ ذـي الـعـرـشـ مـكـيـنـ.

“Ndiyo, kila mara nilikuwa na wasiwasi kuhusu kitu gani kitanitokea mwishoni. Hali hii iliendelea hadi Mwenyezi Mungu akanisifu baada yako [ndani ya Qur`ani] kwa kusema, ‘Mwenye nguvu, mwenye cheo cha heshima kwa Mwenezyi Mungu.’” [81:20]¹⁶

Kuhusu Mtume Muhammad kuwa mwenye rehema, Qur`ani inasema:

لَقَدْ جَاءَكُمْ رَسُولٌ مِّنْ أَنفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ مَا عَنْتُمْ حَرِيصٌ
عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَءُوفٌ رَّحِيمٌ

“Bila shaka amekufikieni Mtume kutoka mionganini mwenu, yanamhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni, kwa waumini ni Mpole, Mwenye kurehemu.” [9:128]

Mtume amekujieni kutoka mionganini mwenu. Yeye si mgeni. Si mtu aliyetoka kwenye sayari nyingine au dunia nyininge. Yeye ni binadamu kutoka mionganini mwenu. Wakati mnapokuwa kwenye matatizo, na yeye anakuwa kwenye matatizo. Anawasikitikieni nyinyi katika mateso yenu. Hivi ndivyo anavyowapendeni na kuwajali nyinyi. Yeye ni kama mzazi ambaye mtoto wake akiwa kwenye matatizo na yeye anakuwa kwenye matatizo. Huwa anajali sana kuhusu ny-

¹⁶ Bihar Anwar, Juzu. 16, Uk. 306.

inyi. Hutaka sana kuwaona nyinyi mkiwa katika hali yenu nzuri sana. Na anao upole wa pekee na huruma ya pekee kwa waumini.

Msikilizaji mzuri sana: Mahali pengine Qur`ani inarejelea kwenye kipengele kingine cha tabia ya urehemevu wa Mtume (s):

وَمِنْهُمُ الَّذِينَ يُؤْذِنُ النَّبِيَّ وَيَقُولُونَ هُوَ أُذْنٌ ۝ قُلْ أُذْنُ خَيْرٌ
لَكُمْ يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَيُؤْمِنُ لِلْمُؤْمِنِينَ وَرَحْمَةُ اللَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ ۝
وَالَّذِينَ يُؤْذِنُونَ رَسُولَ اللَّهِ لَهُمْ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Na mionganini mwao wako wanaomuudhi nabii na wanasema yeye ni sikio: Sema sikio la kheri kwenu, anamwamini Mwenyezi Mungu na anawaamini waumini, na ni rehema kwa wale wanaoamini mionganini mwenu. Na wale wanaomuudhi Mtume wa Mwenyezi Mungu watakuwa na adhabu iumizayo.” [9:61]

Mojawapo ya mambo ambayo baadhi ya watu wa Madina walikuwa wanamfanyia Mtume ni kumuudhi kwa kumuita yeye ‘sikio’ Ilikuwa na maana kwamba Mtume (s.a.w.w.) alikuwa na tabia ya kuwasikiliza watu. Kuwa mtu kama Mtume ambaye humsikiliza Allah swt na Jibril na halafu kuwasikiliza watu na kuwapa heshima ya hali ya juu, huo ni muujiza. Badala ya watu kufurahia tabia hii bainifu, baadhi ya watu walimshutumu, kwa kusema, “Kwa nini anatusikiliza wakati wote? Kwani hana jingine la kufanya!” “Asitusikilize sana” “Yeye huyu ni sikio” Badala ya Mtume (s.a.w.w.) kujitetea mwenyewe, Allah swt alimtetea kwa

kusema Mtume ni "sikio ambalo ni zuri kwenu." Ni kwa ajili ya manufaa yetu.

Kusikiliza ni kazi ngumu. Ni rahisi sana kuongea. Kwa upande mwingine, kusikiliza kunahitaji subira. Wakati mwingine tunakuwa hatuna hata uwezo wa kusikiliza kwa dakika tano bila ya kuingilia kati mazungumzo ya mtu mwingine, hususani kama msikilizaji ni mtu muhimu na mwenye shughuli nyingi ambaye kila mtu anataka kumuulia ili apate ushauri wake; kusikiliza kunaweza kukufanya udhanie kwamba unapoteza muda wako na nguvu zako. Mtume hakufikiri namna hii. Aliwapa watu muda na mazingatio, na alifanya hivyo kwa kuwatazama wao. Mojawapo ya mambo tunayojifunza kuhusu Mtume (s.a.w.w.) ilikuwa kwamba kila mara alikuwa anawatazama watu kwa umakini kwa ajili ya kuwapa heshima kamili. Wakati mwingine unazungumza na watu ambao badala ya kukutazama wewe, wanatazama kwingine, lakini Mtume alielekeza uso wake kwa msikilizaji.

Laini na Mpole: Allah swt pia anasema kwamba alimfanya Mtume Muhammad (s) kutokana na rehema Yake kuwa mpole na laini kwa watu:

فِيمَا رَحْمَةٌ مِّنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظًّا غَلِيلَ الْقُلُوبِ
 لَانْفَضُوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَاوِرْهُمْ
 فِي الْأَمْرِ فَإِذَا عَزَمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ
 الْمُتَوَكِّلِينَ

"Basi kwa sababu ya rehema ya Mwenyezi Mungu umekuwa laini kwao na kama ungekuwa mkali mshupavu wa moyo,

wangekukimbia. Basi wasamehe na uwaombee msamaha na ushauriane nao katika mambo, na unapoazimia basi mtegemee Mwenyezi Mungu, hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wenye kumtegemea.” [3:159]

Rehema ya Mwenyezi Mungu huwafanya watu kuwa laini. Yenyewe ni kama maji. Kama mvua kubwa ikinyesha kwenye chombo; chombo hicho hakiwezi kuhifadhi maji na maji yatamwagika nje ya chombo hicho. Kama mtu anapokea rehema kama elimu, hekima, na nuru kutoka kwa Allah swt, rehema hiyo itamwagika na kwa hakika itawafikia na kuwaathiri watu wengine pia. Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume (s.a.w.w.) kwamba Yeye amempa rehema nyingi sana hivyo kwamba amekuwa laini kwa kila mtu anayemfikia. Na bila shaka, hatimaye ilienezwa kwa “mataifa yote.”

Wakati huo watu wengi hawakuwa laini sana. Wengi wao, kama sio wote, walikuwa jeuri kama matokeo ya utamaduni wao wakati wa Zama za Jahiliya (kipindi kabla ya Uislamu). Walikuwa wanawazika watoto wao wa kike wakingali hai. Ilikuwa rahisi kwoa kuua mamia ya watu. Walikuwa wakiwafanya binadamu kama watumwa na waliwafanyia mambo kama wanyama bila ya heshima yoyote. Waliwafanya wake zao kama rasilimali zao. Mtu kuonyesha mapenzi na huruma kwa watu pamoja na watoto wake na mke wake ilikuwa kama vile ni kuonyesha udhaifu. Wakati fulani Mtume alimbusu mtoto basi mtu mmoja alishangaa sana, na akakiri kwamba kamwe aliquwa hajambusu yejote katika watoto wake. Mtume alijibu: (maneno ya Kiarabu) “Mtu asiyeonyesha huruma hataonyeshwa huruma.” Zaidi ya hayo, walipokuwa wanapigana vitani walikuwa na kawaida ya kukata sehemu kadhaa za uso wa mtu kama vile pua na masikio. Watu waliokuwa

wakiitwa “Waungwana wa Makka” walikuwa na kawaida ya kujinufaisha kwa kutumia nafasi yao na kuwalazimisha watu waliokuwa na kawaida ya kwenda Makka kwa biashara au kuhiji kuacha nguo zao na kununua nguo kutoka kwao; vinginevyo wangezunguka Ka`aba wakiwa uchi. Wakati mwiningine kama mgeni alishaamini na akawapa fedha zake na vitu vingine vya thamani walikuwa na tabia ya kutokumrudishia mwenye mali. Kwa hiyo, watu hawa hawakuwa na huruma kwa wageni au kwa wale wenyeji wasioweza kujilinda. Watu hao walivutiwa tu na pesa na vitu vya kidunia na starehe zake. Kwa upande mwiningine, Mtume (s.a.w.w.) alikuwa mvumilivu sana kwao na alishaonyesha mapenzi mazito sana na huruma hivyo kwamba katika kipindi cha miaka michache aliwabadili. Aliwafanya kuwa watu waliokuwa tayari kutoa mali zao zote kwa kaka na dada zao na kujitoa mhanga kwa ajili ya mwiningine.

Ilikuwa ni kwa sababu ya rehema ya Allah swt kwamba si tu kwamba kauli ya Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ilikuwa laini, lakini ni kwamba utu wake wote ulikuwa mpole sana. Mwenyezi Mungu alimwambia Musa na Harun (amani juu yao wote) kwenda kwa Firaun na “kuongea naye kwa ulaini,” lakini inapokuja kwa Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) Mwenyezi Mungu huthibitisha kwamba tayari amekwishakwa mtu laini. Kwa hiyo, utu wake wote ulikuwa ni laini si kauli yake tu. Halafu Mwenyezi Mungu anaongezea kwamba kama angekuwa mkali na moyo mgumu, watu wangemkimbia na kumwacha peke yake, kwa sababu watu hawa wangeweza tu kushughulikiwa kwa mapenzi na huruma ya kweli halisi tu. Halafu Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume (s.a.w.w.) kuwasamehe wanapofanya makosa. Mwenyezi Mungu pia

anamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwaombea msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu watu hao. Maana yake ni kwamba Mwenyezi Mungu swt yupo tayari kuwasamehe wao na kwa hiyo anamwambia Mtukufu Mtume, "Wasamehe na niombe mimi pia kuwasamehe wao." Hii inaonyesha kipengele kingine cha rehema ya Mwenyezi Mungu.

Kumpeleka Nabii Isa kama Rehema:

Qur`ani pia inathibitisha kwamba Nabii Isa (a.s.) alipelekwa kwa sababu ya rehema ya Mwenyezi Mungu:

قَالَ كَذَلِكَ قَالَ رَبُّكَ هُوَ عَلَيْهِ هِينٌ مُّطَّلِّعٌ وَلِنَجْعَلُهُ آيَةً لِلنَّاسِ
وَرَحْمَةً مِنَّا وَكَانَ أَمْرًا مَقْضِيًّا

"(Malaika) akasema: Ni kama hivyo, Mola wako amesema; Haya ni rahisi kwangu. Na ili tumfanye Muujiza kwa watu na rehema itokayo kwetu, na ni jambo limekwisha hukumiwa." [19:21]

Malaika Jibril alimwambia Bibi Maryam kwamba Mwenyezi Mungu alitaka kumpa mtoto wa kiume kumfanya kuwa ishara na pia kuwa rehema kutoka Kwake.

Hitimisho:

Mbali ya kufanya rehema Yake inayojumuisha kila kitu ijulikane kupitia sifa Zake kama inavyoonekana ndani ya Qur`ani, Mwenyezi Mungu anakumbusha kuhusu manufaa ya kidunia tunayoyapata kutokana nayo. Na zaidi ya ku-

umbwa kwa rasilimali za kimaada kama vile mbingu, nyota, upepo, mvua, na wanyama kwa ajili ya ulinzi wetu na/ au manufaa yetu, pia amehakikisha kwamba tunaongozwa kwa mifano iliyo bora kabisa, wale wenye rehema, uwezo wa kuhisi maono ya mwingine, na upole. Fadhila hizi za kila aina zinaonyesha kwamba tumepewaa mahitaji yote muhimu na miongozo kutuelekeza kwenye maisha yenye ustawi na kufuzu ndani ya Akhera. Kwenye sehemu ifuatayo, tutaona jinsi Mwenyezi Mungu anavyotambulisha wahyi na ujumbe Wake kuwa kwa ajili ya rehema na halafu tutaendelea kuchunguza utungaji wa sheria ambao ameufanya ndani ya dini Yake kutokana na rehema Yake.

SEHEMU YA TANO

MUKHTASARI WA YALIYOPITA: Katika sehemu zili-zotangulia, tulizungumzia majina na sifa mbali mbali zinazotumika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu ndani ya Qur`ani ambazo hurejelea moja kwa moja kwa rehema Yake. Kutoka kwenye rehema Yake, ambayo ina sifa mbali mbali, Mwenyezi Mungu aliumba dunia na hususani wanadamu. Pia tulichunguza wajibu wa rehema ya Mwenyezi Mungu katika kuandaa taratibu kwa ajili ya kuishi kwetu na manufaa juu ya Ardhini na pia wajibu wake katika kumwongoza binadamu. Katika sehemu hii, tutaendelea kujifunza rehema ya Mwenyezi Mungu katika kumwongoza binadamu ambayo inajumuisha pamoja na kuleta vitabu vyya muongozo. Rehema ya Mwenyezi Mungu pia huwaandalia wanadamu aina mbali mbali za misaada katika maisha yao ya kiroho, kama vile ulinzi dhidi ya Shetani, upotovu, na kutokana na nafsi yenye kushawishi.

Mwongozo wa Mwenyezi Mungu:

Zipo aina mbili za mwongozo: kuna mwongozo wa jumla na maalumu. Mwongozo wa Jumla (*al-hidaayah al-`ammah*) ni mwongozo unaotolewa kwa viumbe vyote, kwa kuwa kila kitu kilichoumbwa hapa duniani hupokea namna fulani ya mwongozo. Firauni alipowauliza Musa na Haruni Mola wao alikuwa nani, jibu lake lilikuwa:

قَالَ رَبُّنَا الَّذِي أَعْطَى كُلَّ شَيْءٍ خَلْقَهُ ثُمَّ هَدَى

“Akasema: Mola Wetu ni Yule aliyekipa kila kitu umbo lake kisha akakiongoza.” [Surah Twaha; 20:50]

Kila kitu hapa duniani kinajua wajibu wake kwa ajili ya kuendelea kuwepo kwake hapa duniani. Wanyama, wadudu, na mimea ni viumbe vinavyojua jinsi ya kuishi na kuendeleza spishi zao. Hata elektroni zinajua namna ya kujisonga na kufanya kazi kwa sababu ni Mwenyezi Mungu ndiye ali-yeviongoza:

سَبِّحْ اسْمَ رَبِّكَ الْأَعْلَى الَّذِي خَلَقَ فَسَوْىٰ وَالَّذِي قَدَرَ فَهَدَىٰ

“Lisabihi jina la Mola Wako aliye Mtukufu, Ambaye ameumba, na akaweka sawa, Na ambaye amekadiria na aka-ongoza,” (Surah al-Aa`la, 87:1-3)

Jibu hili linafanana sana na jibu la Musa kwa Firauni. Mwenyezi Mungu ndiye aliyeumba kila kitu, ambaye amewe-ka vipimo vyote sawa na ubunifu, na pia akaviongoza.

Mwongozo Mahususi (*al-hidayah al-khaassah*) unafunga-mana na wanadamu (na majini) viumbe vyenye hiari na kwa hiyo vinaweza kufanya maamuzi ya kimaadili. Mwongozo Mahususi wenyewe umegawanyika mara mbili: a) wa ki-maumbile (*al-takwiniyyah*), ambao ni kupitia dhamira ya ki-binadamu na akili, na b) wa kisheria (*at-tashri`iyyah*) am-bao ni kupitia wahyi na ujumbe wa Mwenyezi Mungu unao-wasilishwa na Mitume kwa wanadamu. Kama tutakavyoona baadaye, wale wanaonufaika na mwongozo unaopatikana

kwa kila mtu watapokea mwongozo wa ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Kwenye sehemu iliyotangulia, tulizungumzia kuhusu Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na Mtume Isa (a.s.), wote hawa waliteuliwa na Mwenyezi Mungu kuwa Mitume wa rehema. Ndani ya kile kinachofuata, tutajifunza utoaji ujumbe mtukufu kutoka kwenye Qur`ani uliopelekwa kupitia kwa mitume kama rehema.

Vitabu vya mwongozo na rehema:

Al-Qur`ani:

Kufuatana na mapitio yetu, zipo aya kumi na sita ndani ya Qur`ani zinazoizungumzia hii Qur`ani kama iliyoshushwa kwa sababu ya rehema Yake. Mathalani, Mwenyezi Mungu anasema:

وَلَقَدْ جِئْنَاهُمْ بِكِتَابٍ فَصَلَّنَاهُ عَلَىٰ عِلْمٍ هُدًى وَرَحْمَةً لِقَوْمٍ
يُؤْمِنُونَ

“Na hakika tumewaletea Kitabu tulichokipambanua kwa ujuzi, ambacho ni mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini.” [Surah al-A`raf, 7:52]

Qur`ani si kitabu chenye utata, wala hakiwapatii watu baadhi ya vichwa vya habari vya jumla tu. Qur`ani ni kitabu kilichochanganuliwa na kinatoa maelezo yote muhimu tunayohitaji kujua kwa ajili ya furaha zetu. Hii ni kwa sababu Mwenyezi Mungu alitaka kutupatia sisi “mwongozo na rehema;” kwa hiyo, Qur`ani ni chanzo cha mwongozo huo

na chanzo cha rehema kwa wanadamu. Mahali pengine, Mwenyezi Mungu anasema:

وَنُزِّلَ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شِفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ لَا يَزِيدُ
الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا

“Na tuliteremsha katika Qur`ani ambayo ni ponyo na rehema. Wala haiwazidishii madhalimu isipokuwa hasara.”

[17:82]

Kulingana na aya hii, Qur`ani ni ponyo na rehema kwa wale wanafuata maelekezo yake na kuyatekeleza. Ni kitabu ambacho kinaweza kuponya maradhi yetu. Bila shaka, chanzo kikuu cha maradhi yetu ni kumsahau Mwenyezi Mungu, na Qur`ani kama ukumbusho (*dhikr*) inaweza kuponya hilo. Kwenye Dua ya Kumayl, tunamuomba Mwenyezi Mungu kwa kusema:

يَا مِنْ أَسْمَهُ دَوَاءٌ وَذِكْرٌ شَفَاءٌ

“Ewe ambaye jina lako ni tiba na utajo Wake ni ponyo.”¹⁷

Kwa hiyo, kwa sababu kumsahau Mwenyezi Mungu ni maradhi, kumkumbuka Yeye ni ponyo. Kwa vyovyote vile, Qur`ani ni ponyo na rehema kwa wote wenye kujitahidi kufaidika na yale yatokanayo humo. Kwa bahati mbaya, wapo wengi ambaao hujikosesha wingi huu wa rehema na

¹⁷ Sheikh Abbas Qummi, *Mafatih al-Jinan*

ponyo. Qur`ani ni kama meza ambayo imeandaliwa na Mwenyezi Mungu na kila mtu anaalikwa kukaribia na kunufaika kutoka humo; hata hivyo, wale ambao hunufaika hasa ni wachache sana kuliko binadamu wote walioalikwa. Inapaswa kuzingatia kwamba wakati wowote Mwenyezi Mungu anapotupatia sisi neema kama vile Qur`ani, Mtume (s.a.w.w.), Ahlul Bayt (a.s.), mwalimu mzuri, rafiki, mwenza mzuri, au watoto wazuri, sisi tunawajibika kwa hayo, na kama hatuwakubali na kunufaika nao, tutaishia kwenye hali mbaya zaidi ikilinganishwa na wale ambao hawajapewa neema hizo. Ndiyo maana wapagani ndani ya Makka kabla ya kuja kwa Uisalmu hawana wajibu zaidi ya wale walioendelea kuwa wapagani hata baada ya kupelekwa Mtume (s.a.w.w.) kuwaongoza. Ni hakika kwamba mnamo Siku ya Hukumu, Mwenyezi Mungu hatawaadhibu katika namna moja. Mfano mwingine unaweza kuonekana ndani ya kisa cha wanafunzi wa Isa (a.s.). Walimda Nabii Isa kumuomba Mola Wake ateremshe meza iliyojaa vyakula na Isa akaomba:

قَالَ عِيسَى ابْنُ مَرْيَمَ اللَّهُمَّ رَبَّنَا أَنْزُلْنَا عَلَيْنَا مَائِدَةً مِنَ السَّمَاءِ
تَكُونُ لَنَا عِيدًا لِأَوْلَانَا وَآخِرِنَا وَآيَةً مِنْكَ مُظَاهِرًا وَأَنْتَ خَيْرُ
الرَّازِقِينَ

“Akasema Isa bin Maryam: Ewe Mwenyezi Mungu! Mola wetu! Tuteremshie chakula mbinguni ili kiwe sikukuu kwa ajili ya wa mwanzo wetu na wa mwisho wetu na kiwe ishara itokayo Kwako na uturuzuku, kwani Wewe ni Mbora wa wanaouruzuku.” [Surah al-Maidah, 5:114]

Waliitaka meza ile sio tu kwa ajili ya kufurahia chakula hicho, lakini kushuhudia ishara ya upendo wa Mwenyezi Mungu na msaada kwa ajili yao, na kwa hili kwa upande wao lilitegemewa kuongeza matumaini yao. Katika kujibu maombi ya Isa, Mwenyezi Mungu Muweza wa Yote alisema:

قَالَ اللَّهُ إِنِّي مُنْزَلٌهَا عَلَيْكُمْ فَمَنْ يَكْفُرُ بَعْدُ مِنْكُمْ فَإِنِّي أَعْذُبُهُ عَذَابًا لَا أَعْذُبُهُ أَحَدًا مِنَ الْعَالَمِينَ

“Mwenyezi Mungu akasema: Hakika Mimi nitakuteremshia, lakini atakayekufuru baada ya hapo basi nitamwadhibu adhabu ambayo sijamwadhibu ye yote katika walimwengu.”

[Surah al-Maidah, 5:115]

Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu anapokupa wewe neema, anatarajia zaidi kutoka kwako, na hili lina mantiki. Kwa hiyo, wale ambao wamepewa zawadi ya Qur`ani na hawaisikilizi au kutekeleza yale yaliomo humo, Qur`ani: “Wala hawazidishii madhalimu isipokuwa hasara.” [17:82] Hali yao inakuwa mbaya zaidi si kwa sababu Qur`ani ina madhara; bali ni kwamba hawatii.

Aya nyingine inayothibitisha kwamba Qur`ani inatokana na rehema ya Mwenyezi Mungu inasomeka kama ifuatavyo:

وَيَوْمَ نَبْعَثُ فِي كُلِّ أُمَّةٍ شَهِيدًا عَلَيْهِمْ مِنْ أَنفُسِهِمْ وَجِئْنَا بِكَ شَهِيدًا عَلَى هُؤُلَاءِ وَنَزَّلْنَا عَلَيْكَ الْكِتَابَ تِبْيَانًا لِكُلِّ شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً وَبُشْرَى لِلْمُسْلِمِينَ

“Na siku tutakapomwinua katika kila umma akiwashuhudi dia kutokana na wao na tukakuleta wewe kuwa shahidi juu ya hawa na tumekuteremshia Kitabu hiki kubainisha kila kitu na uongofu na bishara kwa Waislamu.”

[Surah an-Nahl, 16:89]

Aya hii inarejelea kwenye kanuni ya Ki-Qur`ani ambayo inadokeza kwamba mnamo Siku ya Hukumu, Mwenyezi Mungu ataita kutoka kila umma na kila kizazi shahidi kutoka mionganini mwao ambaye atashuhudia kuhusu imani yao na mwenendo wao. Halafu aya zinarejelea kuhusu kufunuliwa kwa Qur`ani kama maelezo kwa kila kitu ambacho binadamu wanahitaji kujua kwa ajili ya furaha yao, kama mwongozo, rehema, na bishara njema kwa wale wanaojisalimisha kwenye matakwa ya Mungu.

Ifuatayo ni aya nyingine ihusuyo tabia rehemevu ya Qur`ani:

وَإِنَّهُ لَهُدَىٰ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ

“Nayo hakika ni uongofu na rehema kwa waumini.”

[Surah al-Naml, 27:77]

Hadi sasa bado tumetaja aya nne tu kuhusu suala hili na zipo aya zingine kumi na mbili zaidi ambazo zinaonyesha Qur`ani kuwa ni kitabu cha rehema.¹⁸

¹⁸ Hizo Aya nyingine kumi na mbili ni kama zifuatazo; 6:157; 7:63 na 203; 10:57 na 58; 12:111; 16:64; 28:86; 29:51; 31:3; 44:6; 45:20. Kwa mfano mtu anaweza kurejea kwenye hadithi zifuatazo: a) *Sunan Tirmidhi*, Juz. 5, uk. 329:

Kwa hiyo imethibitishwa kwamba Qur`ani ni rehema kuto-ka kwa Mwenyezi Mungu kwa ajili yetu. Kwa hiyo, kama upo wakati ambapo unataka kupata rehema ya Mwenyezi Mungu na hakuna mtu wa kuonyesha, unaweza kushika Qur`ani na kuikumbatia. Ni kipi kinaweza kuwa bora zaidi kuliko kushikilia rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu mikononi mwako? Mwenyezi Mungu anasema:

وَاعْصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ

“Na shikamaneni na kamba ya Mwenyezi Mungu...”

[Surah al-Imran, 3:103]

إِنِي تَرَكَ فِيكُمْ مَا إِنْ تَمْسِكُتُمْ بِهِ لَنْ تَضْلُلُوا بَعْدِي ، أَحَدُهُمَا
أَعْظَمُ مِنَ الْآخَرِ : كِتَابُ اللَّهِ حَبْلٌ مَمْدُودٌ مِنَ السَّمَاءِ إِلَى
الْأَرْضِ ، وَعَنْتَرِي أَهْلَ بَيْتِي وَلَنْ يَقْرُفَا حَتَّى يَرْدَا عَلَى
الْحَوْضِ ، فَانظُرُوا كَيْفَ تَخْلُفُونِي فِيهِمَا

“Nawaachieni mionganini mwenu vitu viwili nya thamani, ambavyo kama mkishikamana navyo hamtapotea baada yangu na kimojawapo ni kikubwa zaidi kuliko kingine: Kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho ni kama kamba iliyotandawaa baina ya mbingu na ardhi, na watu wa nyumba yangu. Vitu hivi viwili havitaachana hadi vitakaponikuta karibu na chemchem ya Kawthar mnamo Siku ya Hukumu. Tazameni na kuweni waangalifu juu ya namna mtakavyoshughulika navyo baada yangu.”

b) *Musnad Ahmad, Musnad al-Ansaar*, Juz. 5, uk. 182:

إِنِي تَرَكَ فِيكُمْ خَلِيفَتَيْنِ كِتَابُ اللَّهِ حَبْلٌ مَمْدُودٌ مَا بَيْنَ السَّمَاءِ
وَالْأَرْضِ (أَوْ مَا بَيْنَ السَّمَاءِ إِلَى الْأَرْضِ) وَعَنْتَرِي أَهْلَ بَيْتِي
وَإِنَّهُمَا لَنْ يَقْرُفَا حَتَّى يَرْدَا عَلَى الْحَوْضِ

“Ninawaachieni makhaliifa wawili: kwanza Kitabu cha Mwenyezi Mungu ambacho ni kama kamba iliyotandawaa baina ya mbingu na ardhi na wa pili ni watu wa nyumba yangu. Hawa hawatatengana hadi watakapokutana na mimi karibu na chemchem (ya Kawthar).”

Kwa hakika "kamba" hii inajumuisha Qur`ani, kama inavyoonekana kwenye matini za Hadithi ya Thaqlayn, ambapo Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) aliitambulisha Qur`ani kama kamba iliyotandazwa kutoka mbinguni hadi ardhini.¹⁹

Torati:

Kufuatana na Qur`ani, aya tano zinaionyesha Torati kama chanzo ambacho pia kilipelekwa kama rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu, mojawapo inasema:

ثُمَّ آتَيْنَا مُوسَى الْكِتَابَ تَمَامًا عَلَى الَّذِي أَحْسَنَ وَتَقْصِيْلًا لِكُلِّ
شَيْءٍ وَهُدًى وَرَحْمَةً لِعَلَّهُمْ بِلِقَاءَ رَبِّهِمْ يُؤْمِنُونَ

"Kisha tulimpa Musa Kitabu, kwa kumtimizia yule aliyefanya wema; na kuwa ni ufanuzi wa kila kitu na mwongozo na rehema ili wapate kuamini kukutana na Mola wao."

[Surah al-Anam, 6:154]

Mahali pengine Qur`ani inasema:

وَلَمَّا سَكَتَ عَنْ مُوسَى الْغَضَبُ أَخَذَ الْأَلْوَاحَ ۖ وَفِي نُسْخَتِهَا
هُدًى وَرَحْمَةً لِلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ يَرْهَبُونَ

"Na ilipomtulia Musa ghadhabu, alizokota zile mbao; na katika maandiko yake mna uongozi na rehema kwa wanaomwogopa Mola Wao." [Surah al-A`raf, 7:154]

Wakati Musa alipopokea zile mbao, na akarudi kwa watu wake na akawakuta wanaabudu hilo sanamu, alikasirika na

¹⁹ Rejea ya hapo juu.

akadondosha mbao hizo. Baada ya hasira yake kutulia, alizikusanya mbao hizo. Ndani ya mbao hizo, mlikuwemo na mwongozo na rehema kwa wale wanaomwogopa Mwenyezi Mungu.

Bado kwenye aya nyingine ,Qur`ani inakichukulia Kitabu cha Musa (a.s.) kama rehema:

وَمِنْ قَبْلِهِ كِتَابٌ مُّوسَىٰ إِمَامًا وَرَحْمَةً ۚ وَهَذَا كِتَابٌ مُّصَدَّقٌ
لِسَانًا عَرَبِيًّا لِيُنذِرَ الَّذِينَ ظَلَمُوا وَبُشِّرَ إِلَيْهِ الْمُحْسِنِينَ

“Na kabla yake kulikuwako Kitabu cha Musa, kuwa kiongozi na na chenyeye rehema. Na hiki ni Kitabu chenyeye kusadikisha cha lugha ya Kiarabu, ili kiwaonye wale waliodhulumu, na kiwe bishara kwa watendao mazuri.” [Surah al-Ahqaf, 46:12]

Kwa hiyo, kufuatana na aya tatu za Qur`ani zilizotajwa hapo juu, Torati pia kilikuwa ni Kitabu cha mwongozo na rehema.²⁰

Ujumbe wa Nuhu

Inaweza kueleweka kutoka kwenye Qur`ani kwamba ujumbe aliopewa Nabii Nuhu (a.s.) pia ulihusisha rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

قَالَ يَا قَوْمَ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّنْ رَبِّي وَآتَانِي رَحْمَةً
مِنْ عِنْدِهِ فَعُمِّيَتْ عَلَيْكُمْ أَنْزِلْتُ مُكْمُوْهَا وَأَنْتُمْ لَهَا كَارِهُونَ

“Akasema: Enyi watu wangu! Mwaonaje ikiwa ninayo dalili iliyio wazi itokayo kwa Mola Wangu na amenipa rehema kutoka Kwake, ikafichikana kwenu, Je, tuwalazimishe na hali nyinyi mnaichukia?” [Surah Hud, 11:28]

²⁰ Aya zingine mbili ni kama zifuatazo: 11:17; 28:43.

Kwa hiyo, ishara alizopewa Nuhu (a.s.), zikijumuisha miujiza aliyofanya na wahyi aliopokea, zilikuwa mfano wa rehema ya Mwenyezi Mungu.

Ujumbe wa Swaleh:

Qur`ani inarejelea kwenye jambo lile lile lililofanywa na Nabii Swaleh (a.s.) ambapo alisema:

قَالَ يَا قَوْمِ أَرَأَيْتُمْ إِنْ كُنْتُ عَلَىٰ بَيِّنَةٍ مِّنْ رَبِّي وَآتَانِي مِنْهُ
رَحْمَةً فَمَنْ يَنْصُرُنِي مِنَ اللَّهِ إِنْ عَصَيْتُهُ فَمَا تَرِيدُونِي غَيْرَ
تَخْسِيرٍ

**“Akasema: Watu wangu! Mwaonaje ikiwa nina dalili ilioyo
wazi itokayo kwa Mola Wangu na akanipa rehema kutoka
Kwake, basi ni nani atakayenisaidia kwa Mwenyezi Mungu
kama nikimuasi? Basi hapo hamtanizidishia isipokuwa
hasara tu.” [Surah Hud, 11:63]**

Kwa hiyo, rehema hii inarejelea kwenye mwujiza ambao aliopewa Swaleh (a.s.) au ujumbe wa Mwenyezi Mungu al- iokuwa ameupokea.

Mwenyezi Mungu hutoa sheria kutokana na rehema Yake:

Maelezo ya Ki-Qur`ani juu ya rehema ya Mwenyezi Mungu yanatoa maelezo ya kina ya dini, yaani hukumu za Shari`ah, ambazo zinaanzia kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَأْكُلُوا أَمْوَالَكُمْ بَيْنَكُمْ بِالْبَاطِلِ إِلَّا أَنْ
تَكُونَ تِجَارَةً عَنْ تَرَاضٍ مِنْكُمْ وَلَا تَقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ إِنَّ اللَّهَ
كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا

“Enyi ambao mmeamini! Msiliane mali zenu baina yenu kwa batili; ila itakapokuwa ni biashara kwa kuridhiana baina yenu. Wala msijiue. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye rehema kwenu.” [Surah an-Nisaa, 4:29]

Kama ilivyodokezwa kwenye aya hii, sababu ya kukatazwa kitendo cha kujiua ni kwa kuwa Mwenyezi Mungu ni Mwenye rehema na huruma kwenu. Mama anayeona kwamba mtoto wake anajiumiza au anajijeruhi mwenyewe humkemea asifanye hivyo kwa sababu anampenda. Vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu anamwambia mtu anayetaka kujiua na hapendi tena kuishi kwamba Yeye bado anampenda na bado anataka aendelee kuwepo.

Mfano mwingine ni hukumu ya *lī`aan*, au ushahidi wa “wale wanaowashutumu wake zao, lakini hawana mashahidi isipokuwa wao wenyewe.” [24:6]. Hukumu imetolewa kwa njia ambayo kwamba hapana mtu asiye na hatia ambaye aneadhibiwa. Halafu Mungu anaongeza:

وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ وَأَنَّ اللَّهَ تَوَابُ حَكِيمٌ

“Na lau kama si fadhila za Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Yake, na kwamba Mwenyezi Mungu ni Mwenye kutakabali toba, Mwenye hekima.” [Surah An-Nur, 24:10]

Mwenyezi Mungu hutusaidia na kutufadhili sisi kutokana na rehema Yake:

Kipengele kingine cha rehema ya Mwenyezi Mungu ni kwamba hutufadhili sisi. Ndani ya kile kinachofuata, tutarejelea baadhi ya njia ambamo fadhila hii hutolewa kama ulinzi dhidi ya Shetani, upotofu, na nafsi yenye ushawishi.

Ulinzi dhidi ya Shetani:

Shetani anaweza kufikiriwa kuwa adui yake Mungu, pamoja na kwamba hawezi kufanya madhara yoyote kwa Mwenyezi Mungu; kwa kawaida yeye hufanya juhudzi zaidi katika kuwatosha wanadamu. Kwa kweli mwanzoni alikuwa na bidii kubwa ya kumuabudu Mwenyezi Mungu. Kulaaniwa kwake kwenye adhabu ya kudumu daima milele kulianza na Mwenyezi Mungu kumuamuru amsujudie Adam:

قَالَ يَا إِنْدِيلِيسُ مَا لَكَ أَلَا تَكُونَ مَعَ السَّاجِدِينَ قَالَ لَمْ أَكُنْ
لَا سُجْدًا لِبَشَرٍ خَلْقَتُهُ مِنْ صَلْصَالٍ مِنْ حَمَاءٍ مَسْنُونٍ قَالَ
فَأَخْرُجْ مِنْهَا فَإِنَّكَ رَجِيمٌ وَإِنَّ عَلَيْكَ اللَّعْنَةَ إِلَى يَوْمِ الدِّينِ قَالَ
رَبِّ فَأَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُبَعْثُونَ قَالَ فَإِنَّكَ مِنَ الْمُنْظَرِينَ إِلَى
يَوْمِ الْوَقْتِ الْمَعْلُومِ قَالَ رَبِّ بِمَا أَغْوَيْتَنِي لَأَزَّيْنَ لَهُمْ فِي
الْأَرْضِ وَلَا أَغْوِنَهُمْ أَجْمَعِينَ إِلَّا عِبَادَكَ مِنْهُمُ الْمُخْلَصِينَ

“Akasema (Mwenyezi Mungu): Ewe Iblisi! Una nini hata hukuwa pamoja na wale waliosujudu? Akasema (Iblisi): Haiwi mimi kumsujudia ulyemuuumba kutokana na udongo mkavu kwa matope meusi yenye kufinyangwa. Akasema

(Mwenyezi Mungu): Basi toka humo , kwani hakika wewe ni mwenye kufukuzwa. Na hakika itakuwa juu yako laana mpaka siku ya malipo. Akasema (Iblisi): Mola wangu! Nipe muda mpaka siku watakapofufuliwa. (Mwenyezi Mungu) akasema: Basi hakika wewe ni katika wliopewa muda, Mpaka siku ya wakati maalumu. Akasema (Iblisi): Kwa ulivyonipoteza, basi nitahakikisha ninawazaini hapa ardhini na nitawapoteza wote.

Isipokuwa waja wako waliosafishwa.” [Surah Hijr, 15:32-40]

Shetani alikataa kusujudia kama matokeo ya kiburi chake; kwa hiyo Qur`ani imemtambulisha yeye kama adui yetu aliye dhahiri:

اَلْمَّ اَعْهَدْ إِلَيْكُمْ يَا بَنِي آدَمَ اَنْ لَا تَعْبُدُوا الشَّيْطَانَ ۖ اِنَّهُ لَكُمْ عَدُوٌ مُّبِينٌ وَّاَنِ اَعْبُدُونِي ۚ هُذَا صِرَاطٌ مُسْتَقِيمٌ وَلَقَدْ أَضَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًا كَثِيرًا ۗ اَفَلَمْ تَكُونُوا تَعْقُلُونَ

“Je, sikuagana nanyi, enyi wanadamu, kuwa msimwabudu She`tani? Hakika yeye ni adui dhahiri kwenu. Na ya kwamba mniabudu Mimi? Hii ndiyo njia iliyonyooka. Na hakika yeye amewapoteza viumbe wengi mionganoni mwenu. Je, hamkuwa mkimtia akilini?” (36:60-62).

Kwa hiyo ahadi yetu na Mwenyezi Mungu si kumuabudu adui yetu aliye dhahiri ambaye hufanya juhudhi kubwa kutudhuru sisi; bali ni kumuabudu Yule anayetuambia tufanye yale yanayohudumia maslahi yetu halisi. Mtu ye yote mwenye hekima kwa hakika angekubalina na kuzingatia ahadi kama hii.

Shetani anazo stadi, njia na vitendea kazi mbali mbali vyta kutudanganya sisi. Huyu ni adui asiyesalimu amri na

hashindwi kwa urahisi. Bila shaka, Shetani hana mamlaka au uwezo wa kuwalazimisha watu wamfuate yeye. Mbinu yake kuu ni kusababisha machafuko na kunong` oneza matamanio maovu. Wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu na kufuata busara walizopewa na Mwenyezi Mungu na maelekezo ya kidini wataona kwamba mipango ya Shetani haina nguvu kiasi hicho: "Hakika hila za shetani ni dhaifu" [4:76] Kama tukiona ni vigumu kujizuia dhidi ya Shetani, kwa kiasi kikubwa ni kwa sababu tunamsaidia dhidi yetu wenyewe kwa kumsahau Mola Wetu na kusikiliza ushauri na ushawishi wa Shetani. Kama tukiamua kuepukia mbali na Shetani na nguvu zake, juhudhi zake hazitafaa kitu. Lakini tunapomsaidia yeye dhidi yetu wenyewe, basi huwa na nguvu, kama inavyotarajiwa kutoka kwa adui yejote.

Kwa hiyo Mwenyezi Mungu, kutokana na rehema Yake, hutusaidia sisi vita dhidi ya Shetani badala kutuacha sisi bila msaada:

وَإِذَا جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِّنَ الْأَمْنِ أَوِ الْخَوْفِ أَذَاعُوا بِهِ ۖ وَلَوْ رَدُّوهُ
إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَى أُولَئِكَ الْأَمْرِ مِنْهُمْ لَعِلَّمَهُ الَّذِينَ يَسْتَبِطُونَهُ
مِنْهُمْ ۖ وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةً لَآتَيْتُمُ الشَّيْطَانَ إِلَّا
قَلِيلًا

"Ikiwajia habari ya amani au ya hofu huitangaza. Na lau wangeirejesha kwa Mtume na kwa wenyewe mamlaka katika wao, wangejua wale wenyewe kuchunguza katika wao. Na lau si fadhila ya Mwenyezi Mungu jiu yenu na rehema Yake mngemfuata shetani isipokuwa wachache tu." (4:83).

Aya hii inaashiria kwamba unapokabiliwa na kikwazo usichokitambua, ni bora kumwachia Mtume au wale am-

ba o wamepewa mamlaka na Mwenyezi Mungu waamue. Na kama isingekuwa kwa sababu ya neema ya Mwenyezi Mungu na rehema Yake, mngemfuata Shetani isipokuwa wachache. Hivyo, Mwenyezi Mungu hutusaidia sisi katika kutuokoa dhidi ya adui yetu ambapo angeamua kutokutusaidia. Hili linafanana na wazazi amba o wanamshauri mtoto wao asiwaamini wageni amba o wanawenza kuwa hatari, pamoja na kwamba wapo watoto wanaokuwa na king`ang`anizi cha kufuata wageni. Kwa upande wa Mwenyezi Mungu (swt), kwa kadiri ahusikanavyo Yeye, upendo Wake kwetu ni mzito sana kiasi kwamba anataka kutushika na kulturudisha tusiende kwa Shetani, kutuweka salama dhidi ya adui.

Ulinzi dhidi ya Upotoshwaji:

Kazi nyingine ya rehema ya Mwenyezi Mungu ni kuwalinda waumini dhidi ya wale wanaotaka kuwapotosha:

وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكَ وَرَحْمَةُ لَهُمْ طَائِفَةٌ مِنْهُمْ أَنْ
 يُضْلُوكَ وَمَا يُضْلُونَ إِلَّا أَنفُسُهُمْ وَمَا يَضْرُونَكَ مِنْ شَيْءٍ
 وَأَنَزَلَ اللَّهُ عَلَيْكَ الْكِتَابَ وَالْحِكْمَةَ وَعَلَمَكَ مَا لَمْ تَكُنْ تَعْلَمُ
 وَكَانَ فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا

“Na lau si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yako na rehema Yake, lingedhamiria kundi katika wao kukupoteza; wala hawazipotezi ila nafsi zao; wala hawatakudhuru na lolote. Na amekuteremshia Mwenyezi Mungu Kitabu na hikima na amekufunza uliyokuwa huyajui. Na fadhila ya Mwenyezi Mungu kwako ni kubwa” [Surah An-Nisaa, 4:113]

Lau kama isingekuwa fadhila na rehema ya Mwenyezi Mungu, kundi la watu wavurugaji lingefanya kila hila na kuwapotosha waumini. Wakati mwingine Mwenyezi Mungu (swt) huwalinda wao dhidi ya njama za maadui kwa kuwafanya wawasahau waumini au kwa kuwabadili mawazo yao.

Ulinzi dhidi ya ushawishi wa nafsi:

Rehema ya Mwenyezi Mungu (swt) pia hutulinda sisi dhi-di ya ushawishi wa nafsi yenye kuamrisha maovu (*al-nafs al-ammarah*). Tunasoma kwenye kisa cha Nabii Yusuf (a.s.) kwamba Zulaykha au Yusuf (a.s.) alisema:

وَمَا أَبْرَئُ نَفْسِي ۝ إِنَّ الْفَسَادَ لَأَمَارَةٌ بِالسُّوءِ إِلَّا مَا رَحِمَ رَبِّي ۝
إِنَّ رَبِّي غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Nami sijitakasi nafsi yangu; hakika nafsi ndiyo iamrishayo mno uovu, isipokuwa ile ambayo Mola Wangu ameirehemu.

Hakika Mola Wangu ni Mwingi wa maghfira, Mwenye kurehemu.” [Surah Yusuf, 12:53]

Kama haya yalisemwa na Zulaykha au Yusuf, maana yake ni kwamba sisemi kwamba mimi ni mtu mtakatifu na sifanyi uovu wowote.²¹ Kwa nini? Kwa sababu nafsi ya binadamu humwamrisha yeye kutenda maovu; kwa hiyo, kama binadamu, upo muelekeo ndani mwangu kwenye matamanio duni, kwenye matendo ya kufedhehesha. Kama nikiachwa peke yangu, sitaweza kuthibitisha kwamba sifanyi matendo yasiyo na maadili. Kama mambo yalivyo, hii haimaanishi kwamba

²¹ Kulingana na ‘Tafsir-e Nimuunih,’ Juz. 9, uk. 434 & 435, maneno haya yalisemwa na Zulaykha. Kwa mujibu wa *Al-Mizan fi Tafsir al-Qur`an*, Juz. 11, uk. 199, maneno haya yalisemwa na Yusuf (a.s.).

kila mtu amehukumiwa kuwa mbaya au mwenye dhambi. Wale wanaopokea rehema ya Mwenyezi Mungu wanawenza kuwa salama kutokana na ushawishi huo na kubakia safi.

Angalizo: Kama mtu akiachwa bila ya rehema ya Mwenyezi Mungu, anaweza akatarajia kila kitendo kiovu kufanywa na yeye. Watu kama hao wanawenza kufanya vitendo ambavyo hata wanyama hawavifanyi. Hii ni hali ya kulaaniwa (*mal`uun*) ambayo imerejelewa ndani ya Qur`ani kama wale ambao wapo mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu. Kwa mfano, Qur`ani inasema kwamba Watu wa Siku ya Sabato (*ashaab al-Sabt*) ambao walidharau amri ya Mwenyezi Mungu ya kupiga marufuku shughuli za kibiashara mnamo siku ya Jumamosi walilaaniwa (4:47) na hatimaye walibadilishwa kuwa manyani kama matokeo yake:

قُلْ هَلْ أَنْبِئُكُمْ بِشَرٍّ مِنْ ذَلِكَ مَتُوْبَةً عِنْدَ اللَّهِ مَنْ لَعَنَهُ اللَّهُ
 وَغَضِيبٌ عَلَيْهِ وَجَعَلَ مِنْهُمُ الْقَرَدَةَ وَالخَنَازِيرَ وَأَبَدَ
 الطَّاغُوتَ إِلَيْكُمْ شَرٌّ مَكَانًا وَأَصَلَّ عَنْ سَوَاءِ السَّبِيلِ

“Sema: Je, niwaambie yule mwenye malipo mabaya kuliko haya mbele ya Mwenyezi Mungu? Ni ambaye Mwenyezi Mungu amemlaani na kumkasirikia na akawafanya miongoni mwao manyani na nguruwe na akamwabudu twaghuti.

Hao ndio wenyе mahali pabaya na wamepotea zaidi njia iliyo sawa.” [Surah al-Maida, 5:60]. – Angalia pia 2:65 na 7:166.

Qur`ani inaonyesha kwenye matokeo zaidi ya kuwa mbali na rehema ya Mwenyezi Mungu, kama vile kuwa kiziwi, kipofu, na moyo mgumu:

أُولَئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ فَأَصْمَمُهُمْ وَأَعْمَى أَبْصَارَهُمْ

“Hao ndio ambao Mwenyezi Mungu amewalaani, na akawatia uziwi, na akawapofua macho yao.”

[Surah Muhammad, 47:23]

فِيمَا نَقْضِيهِمْ مِيثَاقَهُمْ لَعَنَّا هُمْ وَجَعَلْنَا فُلُوبَهُمْ قَاسِيَةً صُدُورُهُمْ يُحرِّفُونَ
الْكَلِمَ عَنْ مَوَاضِيعِهِ وَنَسُوا حَظًّا مَمَّا نُكْرُوا بِهِ وَلَا تَزَالُ
تَطَلُّعٌ عَلَىٰ خَائِنَةٍ مِنْهُمْ إِلَّا قَلِيلًا مِنْهُمْ فَاعْفُ عَنْهُمْ وَاصْفَحْ
إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ

“Basi kwa sababu ya kuvunja kwao agano lao, Tuliwalaani tukazifanya nyoyo zao kuwa ngumu. Wanageuza maneno kutoka mahali mwake na wakaacha sehemu ya yale waliokumbushwa. Na hutaacha kugundua khiyana yao, isipokiwa wachache mionganoni mwao. Basi wasamehe na uwaache. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao wema.”

[Surh al-Maida, 5:13]

Tofauti na Watu wa Sabato, watu kama hao bado wanabakia katika maumbo na sura za wanadamu, lakini kwa sababu wamelaaniwa na matokeo yake miyo yao imefanywa kuwa migumu, na kwa nyongeza ya kufanywa vipofu na viziwi, wanaweza kufanya vitendo kama wanyama na kutenda vitendo vya kikatili. Hili linaelezea vitendo vya kishenzi vilivyofanywa na maadui wa Imam Husayn (a.s.)

mnamo Siku ya Ashura na hali hii iliendelea hata baada ya ushindi wao.²²

Ni rehema ya Mwenyezi Mungu ambayo inaweza kutuzua sisi tusipotoke, kama ilivyoonyeshwa mapema (12:53). Bila ya rehema Yake kwa kweli sisi ni dhaifu, ambapo inamaanisha kwamba rehema Yake ni chanzo cha nguvu dhidi ya ushawishi. Tunahimizwa wakati wote tumwombe Mwenyezi Mungu atusaidie katika kweka nyoyo zetu kuwa safi, kama alivyofundisha Imam Sajjad (a.s.) ndani ya *Al-Sahifah al-Sajjadiyah*:

فِإِنْ نَفْسِي هَالِكَةٌ أَوْ تَعْصِمُهَا

“Moyo wangu utaangamizwa kama Wewe hukuuokoa.”

²² Tukio la kushtusha na kuhuzunisha sana katika historia yote ya Uislamu lilikuwa tukio la Karbala lililotokea katika Siku ya Ashura (yaani tarehe 10 ya Mwezi wa Muharram) mwaka wa 61 AH. Mnamo siku hiyo Imam Husayn, mjukuu pekee wa Mtume aliyebaki, na makumi (takriban 72) mionganini mwa ndugu zake na masahaba waliuliwa kikatili, na Imam Ali b. Husayn na wanawake na watoto wa familia ya Mtume walichukuliwa kama mateka. Sababu kubwa ya tukio hili la kuhuzunisha ilikuwa ni kwamba Imam Husayn alikataa kutoa kiapo cha utii kwa Yazid, Khalifa aliyejitetangaza mwenyewe. Mwana Historia mashuhuri sana wa Sunni, Mohammad b. Jarir Tabari ndani ya kitabu chake kiitwacho ‘*Taarikh al-Umam wa al-Muluk*’ Juz. 3, uk. 307 anasimulia kutoka kwa Imam Husayn, “Enyi watu, ye yeyote anayeshuhudia mtawala dhalimu anahalalisha matendo yale yaliyoharamishwa na Mwenyezi Mungu, kuvunja maagano ya Mwenyezi Mungu, akatenda kinyume na Sunnah za Mtume na kuwatendea watu mabaya na kwa uadui; kama hakumpin ga kwa maneno au vitendo vyake; kwa hakika Mwenyezi Mungu atam-wadhibu kama ambavyo amemwadhibu dhalimu huyo.”.

Rehema ya Mwenyezi Mungu hutakasa moyo:

Mojawapo ya kazi ya rehema ya Mwenyezi Mungu ni kwamba hutusaidia sisi katika mapambano yetu ya kiroho na utakasaji wa moyo:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَبَعُوا خُطُواتِ الشَّيْطَانِ ۚ وَمَنْ يَتَّبِعْ
 خُطُواتِ الشَّيْطَانِ فَإِنَّهُ يَأْمُرُ بِالْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ ۚ وَلَوْلَا فَضْلُ
 اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُهُ مَا زَكَّىٰ مِنْكُمْ مِنْ أَحَدٍ أَبَدًا ۖ وَلَكِنَّ اللَّهَ
 يُزَكِّيٌّ مَنْ يَشَاءُ ۗ وَاللَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ

“Enyi ambao mmeamini! Msifuate nyayo za shetani. Na atakayefuata nyayo za shetani, basi ye ye huamrisha machafu na maovu. Na lau si fadhila ya Mwenyezi Mungu juu yenu na rehema Yake, asingelitakasika mionganoni mwenu ye yote kabisa. Lakini humtakasa amtakaye na Mwenyezi Mungu ni Msikizi na Mjuzi.” [24:21]

Na lau si fadhila na rehema Yake hakuna hata mmoja ambaye angeweza kuwa mtakatifu. Kwa hiyo, endapo mtu ye yote hapa duniani ameweza kuwa mtakatifu kama Mitume na pia wacha-Mungu na watu watukufu, si kwa sababu ya juhudii zao tu; juhudii zao ziliwaletea wao rehema ya Mwenyezi Mungu na halafu rehema ya Mwenyezi Mungu ikakamilisha kazi. Tunatakiwa kujitahidi ingawaje sio sisi tunaokamilisha kazi. Uwepo wetu wenyewe na mwongozo unategemea juu ya Mwenyezi Mungu, na zaidi ya hayo, tunapoelekea Kwake, Yeye hutusogelea na kutusaidia sisi.

Rehema ya Mwenyezi Mungu huwazuia watu wasikate tamaa:

Kwa kawaida watu hukabiliwa na matatizo ya nje au ya ndani wakati wa maisha yao. Kwa muumini, changamoto yake kubwa huanzia ndani mwake. Muumini kamwe hajifurahii yeye mwenyewe na wakati wote huona vigumu kufurahishwa na utendaji wake kwani anataka afanye matendo mema mengi kadiri iwezekanavyo na kujizuia kufanya aina yoyote ya maovu. Anapotazama kwa uangalifu, hutambua kwamba kwa kweli hakuna kikwazo chochote cha nje; tatizo lilikuwa ni kutokana na udhaifu wake mwenyewe na kukosa dhamira. Matokeo yake ni kwamba, inawezekana kwa muumini kuji-kasirikia mwenyewe na kuvunjika moyo. Hudhani kwamba ametenda dhambi nyingi na hakuna chochote katika matendo yake ambacho kinaweza kumpa matumaini, kwa hiyo, hisia hizi za kukata tamaa zinaweza kutokea. Katika maneno kwa Mtme Muhammad (s.a.w.w.), Mwenyezi Mungu anaseema:

قُلْ يَا عَبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

“Sema: Enyi waja wangu waliozifanyia israfu nafasi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwingi wa maghfira, Mwenye kurehemu.”

(Surah Az-Zumar; 39:53)

Mwenyezi Mungu anamwambia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kuwaambia waja wake kwamba wasiikatie tamaa rehema

Yake Mungu hata kama wamezifanyia israfu nafsi zao na wamejidhuru wenyewe kwa kufanya matendo maovu. Halafu Mwenyezi Mungu anasema kwamba kwa hakika Yeye ni Msamehevu kwa dhambi zote (na sio baadhi tu ya dhambi). Kama mtu anadhani kwamba hakuna nafasi ya kurejea tena na kwamba mtu amevunja uhusiano wote na Mwenyezi Mungu, aya hii inatufahamisha kwamba wakati wote kuna nafasi kwa wale wanaorejea Kwake kwa uaminifu.

Mojawapo ya dhambi kuu ni kukata tamaa juu ya rehema ya Mwenyezi Mungu (*al-ya`ṣ-u min rawḥillah*). Kule kusema kwamba 'Mwenyezi Mungu kamwe hatanisamehe' kwenyewe ni dhambi kubwa na kulingana na hadithi nyingi dhambi hii ni mbaya kuliko dhambi zingine zote kuu. Wale wanaodhani kwamba Mwenyezi Mungu kamwe hatawasamehe huwa windo la Shetani. Shetani anaweza kuwadanganya kwa urahisi sana wale ambao hawana matumaini na huwapotosha katika maisha yao yote, lakini wale wenyewe matumaini ya kusamehewa na kujirekebisha watatoroka kutoka kwa Shetani na kujaribu kurejea kwa Mola Wao. Njia bora kabisa ya kubaki na matumaini ni kukumbuka na kutafakari juu ya rehema ya Mwenyezi Mungu isiyo na kikomo.

Katika kitabu chake '*Tadhkirat al-Muttaqin*', Ayatullah Bahaari Hamedani, ambaye ni sufi mkubwa anazungumzia sera ya Shetani yenye sura mbili ambapo Shetani, kwa kusisitiza juu ya rehema ya Mwenyezi Mungu, huwahimiza watu kutenda dhambi na baada ya kutenda dhambi hizo, Shetani hujaribu kuwazuia watu wasitubie dhambi zao kwa kuwanong'oneza kwamba 'umechelewa sana na kamwe hutusamehewa, kwa hiyo, angalau furahia maisha ya kidunia.' Ayatollah Ayatullah Bahaari anashauri kwamba tuchukue

sera pinzani. Kabla ya kutenda dhambi, mhusika anatakiwa kusoma tena aya za Qur`ani juu ya adhabu ya kuumiza kwa madhalimu mnamo Siku ya Hukumu na kuamini kwamba mtu hataweza kutubu, lakini kama kwa sababu yoyote ile inatokea mtu anafanya dhambi, basi anapaswa kusoma aya za Qur`ani juu ya rehema na msamaha wa Mwenyezi Mungu na kuwa na uhakika kwamba Mwenyezi Mungu atawasamehe wale wanaotubia kwa ukweli halisi.

Hitimisho:

Katika kumwongoza binadamu rehema ya Mwenyezi Mungu hujumuisha kushusha Torati na Qur`ani, vitabu ambavyo hutoa maelezo muhimu ya kina kwa ajili ya furaha yetu, pamoja na kutoa ujumbe wa mwongozo kutoka Manabii Nuhu na Swaleh. Ndani ya maelezo haya ya rehema ya Mbinguni, Mwenyezi Mungu anatoa hukumu ambazo chimbuko lao ni kwenye rehema Yake, kama vile kuwakaripia watu wasijiue kwani Mwenyezi Mungu hupenda viumbe wake waendelee kuishi kwa furaha bila kukatia tamaa rehema Yake. Rehema ya Mwenyezi Mungu pia humpatia binadamu aina nyingi za fadhila katika maisha yao ya kiroho, kama vile ulinzi dhidi ya upotovu, nafsi yenye kushawishi, na Shetani. Pamoja na fadhila hizi, Yeye huwazuia watu wasikate tamaa, kwani rehema Yake ni kubwa kuliko dhambi za watu. Ndani ya makala zifuatazo, tutachunguza aina mbali mbali na viwango vyta msamaha wa mbinguni na kuelewa jinsi Mwenyezi Mungu anavyoweza hata kubadili matendo mabaya ya mtu na kuwa mema.

SEHEMU YA SITA

MUKHTASARI WA YALIYOPITA: Kwenye makala ili-yopita, tulichunguza wajibu wa rehema ya Mwenyezi Mungu katika kuwasaidia wanadamu kuitia kupeleka ujumbe wa mwongozo kutoka Manabii Nuhu na Swaleh, pamoja na ku-peleka vitabu vya mwongozo kama vile Torati na Qur`ani. Pia tulichunguza njia ambazo Mwenyezi Mungu huwasaidia wanadamu kuitia rehema Yake, ambayo inajumuisha kuwalinda watu kutokana na kumfuata Shetani,²³ dhidi ya njama za maadui za kuwapotosha wao,²⁴ na dhidi ya nafsi yenye kushawishi.²⁵ Pia tulitazama wajibu wa rehema ya Mwenyezi Mungu katika kuitakasa nafsi²⁶ na kuwazuia watu wasije wakakata tamaa²⁷ kwani rehema Yake ni kubwa mno kuliko dhambi za watu. Ndani ya makala hii, tutachunguza aina mbali mbali na viwango mbali mbali vya msamaha wa Mwenyezi Mungu na kuelewa jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu anaweza hata kubadili matendo mabaya ya mtu na kuwa mazuri. Baadaye, tutaangalia jinsi watu wanavyoipokea rehema ya Mwenyezi Mungu na hatimaye kuchunguza jinsi wale wanaokuwa na subira wanavyopokea rehema ya ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Wajibu wa rehema ya Mwenyezi Mungu katika msamaha:

Kutokana na rehema Yake, Mwenyezi Mungu huwasamehe wale wanaotubu:

²³ Qur`ani; 4:83

²⁴ Qur`ani; 4:113

²⁵ Qur`ani; 12:53

²⁶ Qur`ani; 24:21

²⁷ Qur`ani; 39:53

فَتَأْتَىٰ آدُمٌ مِّنْ رَّبِّهِ كَلِمَاتٍ فَتَابَ عَلَيْهِ ۝ إِنَّهُ هُوَ التَّوَابُ الرَّحِيمُ

“Akapokea Adam maneno kutoka kwa Mola Wake, na Mola Wake akapokea toba yake. Hakika Yeye ni Mwingi wa kukubali toba, Mwenye kurehemu. (Surah al-Baqarah, 2:37)

Kwanza Mwenyezi Mungu alimfundisha Adam maneno, na Adam alipotumia maneno hayo kutubia, Mwenyezi Mungu alikubali. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu Mwenyewe alilianza jambo hili. Ni muhimu kuzingatia kwamba hali hii haikuwekewa mpaka kwa Adam tu: Mwenyezi Mungu humsamehe yejote anayetubu kuwa ukweli na kwa uaminfu aka-jaribu kubadilika na kuwa mwema:

قُلْ يَا عِبَادِيَ الَّذِينَ أَسْرَفُوا عَلَىٰ أَنْفُسِهِمْ لَا تَقْنَطُوا مِنْ رَحْمَةِ اللَّهِ ۝ إِنَّ اللَّهَ يَغْفِرُ الذُّنُوبَ جَمِيعًا ۝ إِنَّهُ هُوَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ

“Sema: Enyi waja wangu waliozifanyia israfu nafsi zao! Msikate tamaa na rehema ya Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu husamehe dhambi zote. Hakika Yeye ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.

(Surah Az-Zumar, 39:53)

Kubadilisha matendo maovu kuwa matendo mema:

Sio tu kwamba Mwenyezi Mungu humsamehe mwenye kutubia, lakini pia anaweza kubadili matendo mabaya na kuwa mema:

إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلاً صَالِحًا فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا

“Isipokuwa atakayetubia na akatenda mema, basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.” [Surah al-Furqan, 25:70]

Hii ni zaidi ya kusamehe tu matendo maovu ya mtu. Kwa hakika watu hawana tabia hii. Watu wanapomsamehe mtu, inawezekana wasimwadhibu mkosaji kwa matendo yake maovu, lakini inawezekana wakaendelea kukumbuka matendo maovu ya mkosaji na hata kuyasema kwa wengine. Na hata kama mathalan tukiwasamehe na kusahau makosa yao kabisa, kwa kawaida hatuyachukulii matendo maovu ya watu kuwa ni matendo mazuri na kuwalipa ipasavyo. Si jambo la kawaida kwa watu kumlia wema mtu ambaye anawasaliti au kutowatii wao. Kwa kinyume chake, Mwenyezi Mungu sio tu kwamba anasamehe, lakini anaweza kubadili matendo yako mabaya na kuwa matendo mazuri, na matokeo yake, anaku-pa thawabu kwa ajili ya matendo hayo.

Tunaposoma orodha ya matendo yetu mnamo Siku ya Hukumu, tunaweza kuona kwamba tulitumia maisha yetu huku tukizikosa fursa nyingi. Juu ya hayo, rekodi yetu inao-nyesha matendo yetu mengi mazuri katika kuwasaidia watu pamoja na kwamba tunajua kwamba inawezekana hatukumsaidia yeyote. Kwa mfano, walikuwepo watu mia moja ambao walikuwa wanahitaji msaada wako, na hukuwasaidia, pamoja na kwamba inaonyeshwa ndani ya rekodi yako

kwamba uliwasaidia watu hao mia moja. Pamoja na kwamba ni vigumu kuamini, rekodi yako itasomeka, "Watuhawa mia moja ni wale ambaowewe hukuwasaidia, lakini ulipotubia kwa dhati na ukajisikia vibaya kwa kushindwa kuwasaidia, kwa kweli na kwa uaminifu ulihisi kwamba ulifanya kitendo kibaya. Wakati ulipotaka kuwasidia, hapakuwepo na fursa ya kufanya hivyo. Ama muda wako ulikwisha au watuhao hawakuwepo tena. Lakini kwa kuwa ulikwishajutia kitendo chako kwa uaminifu, sisi tumeandika kwamba uliwasaidia watuhao moja." Kwa ukarimu Wake mwingi, hii ndio njia ambayo Mwenyezi Mungu hututendea, ingawa ni kwamba hii ni kwa ajili ya hao wanaomwendea Yeye kwa uaminifu na moyo wote bila kudanganya au kuchukua fursa ya rehema ya Mwenyezi Mungu. Wao ni kweli wanatamani kubadilika na kuwa wema kwa ukweli na uaminifu.

Nafasi ya rehema ya Mwenyezi Mungu katika kurahisisha mambo yetu:

Wakati mwingine Mwenyezi Mungu, kutokana na rehema Yake, huturahisishia mambo yetu kwa kutuachia kiasi fulani au kupunguza wajibu wetu. Kwa mfano, kuhusu 'qisaas' (kulipiza kisasi), Qur`ani inaseama:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا كُتِبَ عَلَيْكُمُ الْقِصَاصُ فِي الْقَتْلَىٰ ۖ إِنَّ الْحُرُّ
بِالْحُرِّ وَالْعَبْدُ بِالْعَبْدِ وَالْأُنْثَىٰ بِالْأُنْثَىٰ ۚ فَمَنْ عُفِيَ لَهُ مِنْ أَخِيهِ
شَيْءٌ فَاتَّبَاعُ بِالْمَعْرُوفِ وَأَدَاءُ إِلَيْهِ بِإِحْسَانٍ ۗ ذَلِكَ تَخْفِيفٌ مِنْ
رَبِّكُمْ وَرَحْمَةٌ ۗ فَمَنِ اعْتَدَىٰ بَعْدَ ذَلِكَ فَلَهُ عَذَابٌ أَلِيمٌ

“Enyi mliaoamini! Mmeandikiwa kisasi kwa wenyewe kuuliwa; muungwana kwa muungwana, mtumwa kwa mtumwa, na mwanamke kwa mwanamke. Na anayesamehewa na ndugu yake chochote, basi ni kufuatana kwa wema na kulipa kwa ihsani. Hiyo ni tahafifu itokayo kwa Mola Wenu na rehema. Na atakayeruka mipaka baada ya hayo, basi ana adhabu iumizayo.” (Surah al-Baqarah; 2:178)

Kama mtu amemuua mtu mwingine, walezi wa mwathirika wanayo haki ya kudai adhabu kwa mkosaji. Lakini kama wale ambao wamepoteza mpendwa wao wakidai fedha ya fidia badala ya kulipiza kisasi, Mwenyezi Mungu analikubali hili. Hii ni aina ya wepesi Mwenyezi Mungu anayokupatia wewe, hivyo kwamba kama walezi wa mwathirika wameridhika, ni kama vile Mwenyezi Mungu anasema, “Mimi ninafurahi na kwa kweli Mwenyezi Mungu hutupenda sisi kusameheana sisi kwa sisi (ijapokuwa kama mkosaji anayo nia ya kurudia uhalifu wake hilo ni jambo jingine).” Mwenyezi Mungu anatupatia sisi haki ya kudai kuuliwa kwa mkosaji, lakini kama ukimsamehe kaka yako au dada yako katika Uislamu ambaye alitenda kosa hili na unajua kwamba anajuta, Mwenyezi Mungu hukubali hili, na hasisitizi kwamba umuue mtu huyo.

Aina ya majibu kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu:

Mwenyezi Mungu huwapa watu rehema katika njia mbali mbali. Lakini watu wanapopata rehema ya Mwenyezi Mungu hupokea katika njia mbali mbali: wapo wale wanaoridhika na kushukuru na ambao hutumia rehema hii kwa hekima, na wapo wale ambao hawana shukurani au hushindwa kuipokea. Wakati mwingine hawachukui rehema hiyo kama ni zawadi kutoka kwa Mwenyezi Mungu; badala yake, hudhani

jambo hilo limetokea kwa bahati au huamini kwa uhakika kwamba jambo hilo ni mafanikio yao wenyewe. Kama wanayo familia nzuri, watoto waadilifu, sifa stahiki, au elimu ya kufaa, huamini rehema hiyo ni matokeo ya mafanikio yao badala ya ukarimu wa Mwenyezi Mungu. Allah swt anamwambia Mtume Muhammad (s.a.w.w.):

فَإِنْ أَعْرَضُوا فَمَا أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِظًا إِنْ عَلَيْكَ إِلَّا
الْبَلَاغُ^{٤٣}

“Na wakipuuza, basi hatukukupeleka uwe mwenye kuwalinda. Si juu yako ila kufikisha tu.....” (Surah al-Fat'h, 42:48).

Kazi ya mitume ilikuwa kufikisha ujumbe wa Mwenyezi Mungu. Kama watu wakiamini au wasiamini huo si wajibu wa mitume wala hawatahojiwa kuhusu hilo. Mitume wanawajibika katika kufikisha ujumbe katika njia nzuri zaidi iwezekanavyo; hakuna mtu anayetakiwa au hata kuweza kuwalazimisha wengine kuamini. Imani inakaa ndani ya moyo na mtu pekee mwenye udhibiti juu ya moyo wake ni mhusika mwenyewe. Kwa hiyo, hakuna kiongozi au mubaligh anayepaswa kusikitika kama watu hawakikubali kile ambacho anatoa baada ya kuhakikisha kwamba ametekeleza wajibu wake inavyotakiwa. Vivyo hivyo, daktari aliye na uwezo mkubwa kabisa ambaye hubaini ugonjwa kwa usahihi na kumwandikia mgonjwa dawa nzuri ambaye kwa upande wake anachagua asitumie dawa hiyo anaweza kusikitika sana, ingawa hapaswi kulaumiwa, na wala hapaswi kujilaumu mwenyewe kwa chaguo baya la mgonjwa.

Nabii Nuhu (a.s.) ni mfano mkubwa sana. Alifanyakazi kwa bidii sana kwa miaka mia tisa na hamsini²⁸ na baada ya tabligh ya muda mrefu kiasi hicho, ni watu themanini tu ndio walioamini ujumbe wake – wastani wa mtu mmoja katika kila miaka 12 – lakini kwa vyovyyote vile hii haiwezi kuchukuliwa kama ishara ya kushindwa kwake au mapungufu. Kinyume chake, Nabii Nuhu ni mmojawapo wa manabii watano mashuhuri sana ambao huitwa ‘Mitume wenye Maazimio Makubwa’ (*ulu`l-'azm*).²⁹

Kwa hiyo, jambo la muhimu ni kufikisha ujumbe sawasawa. Kwa mfano, kama mtu akikupa bahasha yenyeye barua ndani na anakuomba uifikishe mahali, wajibu wako ni kuhakikisha kwamba barua hii inamfikia mlengwa. Hutarajiwi kumpa mtu mwingine kuifikisha barua hiyo; mtu yule anaweza kusahau. Haupaswi kuisafirisha tu kwa njia ya posta; inaweza kupotea. Kama ukiwiweka barua nje ya mlango wa nyumba yake, inaweza kupeperushwa na upemo au panaweza kuwa na watoto ambao wanaweza kuiweka mahali pengine. Wajibu wako ni kuhakikisha kwamba inafika kwenye mkono wa mwenye barua. Hata hivyo, kama ataifungua barua hiyo, akaisoma, au anaifanya kazi baada ya kuisoma huo si wajibu wako. Mhusika anaweza akaitupa barua hiyo, akaingalia juu juu, au akaisoma na asiishughulikie. Kwa jinsi unavyohusika wewe mpelekaji barua, umefanya kazi yako vema ulipochukua usumbufu wote na kuhakikisha kwamba ujumbe huu unafika kwa mhusika.

Kwa bahati mbaya, mara nyingi kinachotokea ni kwamba huwa hatuhakikishi kwamba ujumbe wa Mwenyezi Mungu

²⁸ Qur`ani; 29:14

²⁹ Qur`ani; 46:35

unafikishwa sawasawa. Kwa mfano, hata kama tunao uzoefu wa kuufahamu ujumbe wa Mwenyezi Mungu, inawezekana tusijue namna ya kuufikisha kwa njia inayofaa kwa wale wanaoishi chini ya mazingira fulani kwa namna ambayo wataupokea vema na kuuchukulia kwa makini kabisa. Wakati mwagine tunatengeneza vitabu na makala zenye manufaa kabisa, lakini havichapishwi kamwe au kama vikichapishwa inawezekana visiandikwe katika lugha na mtindo unaofaa na hata kama ikiwa hivyo, inawezekana visigawiwe vizuri. Vitabu vyetu vingi vinagawiwa kwenye makundi yetu wenewe na watu walioko nje ya makundi yetu hawajui lolote kuhusu vitabu na makala hayo. Na kwa bahati kama ikitokea wanapata kujua kuhusu vitabu hivyo, hakuna mfumo wa kuagizia kama wanavyofanya kwa vitabu vingine. Kama wakienda kwenye maduka ya vitabu au wakitembelea mikondo ya wauza vitabu kwa mtandao wa intaneti, inawezekana bado wasivione vitabu hivyo. Tunatakiwa kuhakikisha kwamba kwa njia ile ile ambayo watu hupokea marundo ya aina nyingi za ujumbe mwagine kutoka kwenye makampuni makubwa ya biashara na vyombo vya habari, na ujumbe wa Mwenyezi Mungu unawafikia wao kwa njia ya uadilifu na heshima, kwa njia ambayo wanaweza kuupokea, na sio tu, mathalani, kwa kuuweka nje ya mlango wa nyumba zao. Baadaye, uamuzi wa kuufanyia kazi ujumbe huo ni juu yao. Tunatakiwa kuhakikisha kwamba ujumbe unawafikia. Leo hii tuko nyuma sana katika suala hili. Watu wengi kwa kweli hawapati habari za kielimu nzuri ambazo zinawasilisha Uislamu kwa hekima. Badala yake wanapaswa kufanya juhudhi ya kuzitafuta.

Kwa hali yoyote ile, baada ya kutaja jambo hilo hapo juu, Qur`ani inasema:

وَإِنَّا إِذَا أَدْقَنَا الْإِنْسَانَ مِنَ رَحْمَةً فَرَحِبَ بِهَا وَإِنْ تُصِنْبُهُمْ سَيِّئَةً
بِمَا قَدَّمْتُمْ أَيْدِيهِمْ فَإِنَّ الْإِنْسَانَ كُفُورٌ

“.....Na hakika tunapomwonjesha mtu rehema kutoka Kwetu, huifurahia. Na ikisibiwa na ovu kwa sababu ya iliyotanguliza mikono yao, basi hakika mtu huyu anakufuru.” [Surah Ash-Shura, 42:48]

Binadamu huonekana kuwa na furaha kupita kiwango pale wanapopata rehema ya Mwenyezi Mungu na matokeo yake hujisahau, huhisi kujisikia, na kumsahau Mwenyezi Mungu. Kwa upande mwingine, wanapopatwa na matatizo makubwa, wanawenza kusahau neema aliyowapa Mwenyezi Mungu siku za nyuma na kulalamika juu ya hayo yanayowapata. Baada ya kuwa wamekwishapokea maelfu ya aina mbali mbali za rehema ya Mwenyezi Mungu, sasa wakiwa wakabiliane na tatizo moja tu huwafanya wao kuwa wasumbufu na walalamihi. Pale watu wanapopewa mahitaji yao muhimu ya kila siku huridhika kwa urahisi na kusahau dhima wanayotakiwa kuwajibikia; kwa upande mwingine, na inapotokea hawakupewa kitu kile kile kwa siku moja, hulalamika na kuhoji sifa nzuri za Mpaji. Majibizo haya ya kawaida kwa wanadamu ambayo hutokea mara kwa mara yanaweza kusafishwa kwa maelekezo na elimu ya kutosha.

Jinsi ya kupokea rehema nyingi zaidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

Kwa wale wanaopokea rehema ya Mwenyezi Mungu kwanza kabisa, Mwenyezi Mungu huwapa wao rehema ya ziada. Kwa

njia hii, rehema hiyo haitapotea bure wala kugeuzwa dhidi yao, kwa sababu wale wasioikubali neema ya Mwenyezi Mungu na kunufaika nayo watahojiwa na kuadhibiwa vikali zaidi ikilinganishwa na wale ambao hawakupewa rehema kabisa. Na kama watu wasio na shukurani kama hao wakipewa zaidi, matatizo yao yatazidi kuongezeka tu. Kwa mfano, kama Mwenyezi Mungu amenipa mimi mtoto na nisimtunze mtoto huyo ingekuwa ni vema zaidi kama nisipopewa zaidi ya huyo. Au kama Mwenyezi Mungu amenipa mimi fedha wakati sina ujuzi wa kutunza fedha, itakuwa ni vema kama Mwenyezi Mungu hatanipa fedha zaidi. Hata hivyo, kama mtu ni mwenye kushukuru na anajua jinsi ya kushukuru neema za Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu atamzidishia:

لَئِنْ شَكْرْتُمْ لَأَزِيدَنَّكُمْ

“....Mkishukuru nitawazidishia” [Surah Ibrahim, 14:7]

Mahali pengine, Qur`ani inasema:

يُدْخِلُ مَنْ يَشَاءُ فِي رَحْمَتِهِ وَالظَّالِمِينَ أَعْذَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا

“Humwingiza amtakaye katika rehema Yake. Na wenye kudhulumu amewawekea adhabu iliyo chungu.”

[Surah al-Insan, 76:31]

Rehema ambayo Mwenyezi Mungu huwapa watu ambao anawardhia ni rehema ya nyongeza juu ya ile ambayo kila mtu hupewa. Mwenyezi Mungu humpa rehema kila mtu, lak-

ini huwapa zaidi wale ambao wenye shukurani, na huwaruhusu waende kwenye kina kirefu zaidi cha bahari ya rehema Yake. Kwa upande mwingine, wale madhalimu na wasio na shukurani watapata hasara na kuteseka. Inazingatiwa kwamba katika Uislamu, tendo lolote baya linachukuliwa kuwa ni tendo udhalimu, iwe kama linawaathiri wengine au dhalimu mwenyewe. Hakika, hata pale ambapo mtu fulani anawafanya udhalimu wengine kwanza hujifanyia udhalimu yeye mwenyewe na kujikosea yeye mwenyewe kabla ya kuwakosea na kuwadhuru wengine. Mathalani, endapo ninatumia maneno machafu wakati wa kuzungumza, huko ni kumvunja heshima yule ninayemwambia maneno hayo, lakini kwanza kitendo hicho kinadhuru utu wangu mwenyewe na kitaniletea aibu. Watu watakaposikia mimi ninaongea kwa njia kama hiyo, watamhurumia yule nimwambiaye maneno hayo, lakini wote watakuwa dhidi yangu na watachukizwa na kitendo changu. Kwa hiyo, pamoja na kwamba nilitaka kumdhalilisha mtu, nitakuwa nimejidhalilisha mwenyewe tu. Watu waheshimiwa na wenye hadhi hawaamiliani na wengine kwa utovu wa heshima, lakini huwezi kutarajia mtu asiyejiheshimu kufanya kila kitu.³⁰ Mtu ambaye hajiheshimu yeye mwenyewe anaweza kufanya lolote. Hakuna kitakachomzuia kufanya hivyo. Imam Hadi (a.s.) amenukuliwa akisema:

³⁰ Mtu anayejiheshimu mwenyewe havai kila kitu, hata kama yuko peke yake. Inasemekana kwamba wakati fulani mmojawapo wa Ulamaa ambaye kila mara alikuwa akivaa '*aba*' (joho) na '*amamah*' (kilemba) katika namna rasmi kabisa akiwa nyumbani kwake aliambiwa na mtu fulani: "Hakuna mtu ye yote hapa. Kwa nini unavaa vazi la kikazi?" Akajibu: "Nipo mwenyewe hapa."

من هانت عليه نفسه فلا تأمن شره

“Usijihisi uko salama kutokana na vitendo vibaya vya wale wasiojiheshimu.”³¹

Kwa hiyo, wale wanaojiheshimu wenyewe hawatarajiwi kutenda dhambi na vitendo vya kidhalimu na kwa hiyo hawatanyimwa kupokea rehema ya ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Mwenye subira hupokea rehema za ziada:

Kundi moja ambalo hupokea rehema za ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni wenyе subira:

وَلَنْبُونَكُمْ بِشَيْءٍ مِّنَ الْخَوْفِ وَالْجُوعِ وَنَقْصٍ مِّنَ الْأَمْوَالِ
 وَالْأَنْفُسِ وَالثَّمَرَاتِ^{٣١} وَبَشِّرِ الصَّابِرِينَ الَّذِينَ إِذَا أَصَابَتْهُمْ
 مُصِيبَةٌ قَالُوا إِنَّا لِلَّهِ وَإِنَّا إِلَيْهِ رَاجِعُونَ أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَواتٌ
 مِّنْ رَبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ وَأُولَئِكَ هُمُ الْمُهَتَّدُونَ

“Na hakika tutawajaribu kwa chembe ya hofu na njaa na upungufu wa mali na wa nafsi na wa matunda. Na wape bishara wanaosubiri. Ambao ukiwapata msiba, husema: Hakika sisi ni wa Mwenyezi Mungu, na Kwake tutarejea. Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola Wao, na rehema, na hao ndio wenyе kuongoka.”

(Surah al-Baqarah; 2:155:157)

³¹ Bihar al-Anwar, Jz. 72, uk. 301; Hadithi ya 11 & Jz. 75, uk. 366 Hadithi ya 5; Mizan al-Hikmah, Jz. 2, uk. 982.

Kwa hakika tutajaribiwa na kupimwa katika njia mbali mbali. Wakati mwingi ipo hofu kwa ujumla au kwa sababu ya upungufu wa usalama. Panaweza kuwepo njaa, inawezekana usiwe na chakula kwa ajili yako mwenyewe, watoto wako, au marafiki zako. Au panaweza kuwepo na hasara katika matunda, fedha, au katika maisha. Tunaweza tukapoteza vitu au watu tuwapendao. Yote haya ni matukio ambayo Mwenyezi Mungu hutujaribu nayo.

Hebu tufafanue aya hizo hapo juu na zingine zifananazo nazo. Baadhi ya watu wanaweza kudhani kwamba Mwenyezi Mungu anaposema kwamba Yeye hukujaribu wewe ina maanisha kwamba Yeye anasababisha matatizo haya kwa makusudi yakutokee wewe hasa. Kinyume chake kabisa; panaweza kuwepo na mambo mengi ambayo Mwenyezi Mungu Mwenyewe hafurahishwi nayo kabisa pamoja na matukio mabaya yanayotokea kama mauaji au wizi. Kama mtu akimuua mwanangu, hiki si kitendo ambacho Mwenyezi Mungu amekipenda, lakini sasa kwa kuwa kinatokea kwa hiyo kinakuwa kama ni mtihani kwangu. Kwa hiyo, chochote kile kinachotokea kwako kwa sababu yoyote ile, kinatakiwa kitafsiriwe kama mtihani kwamba kama ukifafulu utanyanyuliwa daraja hapa duniani na akhera. Kwa mfano, tuchukulie kwamba mimi kuwa mkufunzi wa kuendesha gari ambaye huketi karibu na mwanafunzi wangu anapoendesha gari mjini. Kufumba na kufumbua, mtu mmoja kwa sababu yoyote ile anadharau taa nyekundu na anaonekana mbele yetu. Mimi kama mkufunzi, ninatarajiwu kumtazama mwanafunzi wangu ili kumjaribu yeye. Ingawa sikumwambia huyo dereva mzembe atupite kwa ghafla hivyo, tukio hili linaweza bado

kuwa kama mtihani. Kwa uangalifu mkubwa wa utendaji wa mwanafunzi wangu, ama ninaweza kumwambia alionyesha ustadi mzuri wa kuendesha gari au ninaweza kumwambia kwamba bado anahitaji mafunzo zaidi. Pamoja na kwamba uendeshaji wa kizembe wa dereva wa gari ny ingine haukutarajiwa, bado ninaweza kuchukua tukio hili kama mtihani. Hivyo, maamuzi mabaya ya watu na matokeo hasi yanayowapata wengine, yanaweza kuwa kama mitihani, ingawa Mwenyezi Mungu hajakusudia matendo hayo mabaya na matukio ya mielekeo hasi kutokea.

Kwa kufafanua, pale Mwenyezi Mungu anaposema, "Ninakujaribuni nyinyi kwa kila kitu," haimaanishi kwamba kwa makusudi Yeye huwachukua wale muwapendao, au kusababisha upungufu wa salama na kwa ufupi, kwamba yuko nyuma ya kila tatizo.³² Maana ya hili ni kwamba chochote kinachotokea, kizuri au kibaya, Yeye huangalia utendaji wako na unashughulikia vema jinsi gani hali hiyo. Pia hii yenewe ni neema kwa wale wanaotaka kuboresha kitabu chao cha amal; wakati wowote na kwa hali yoyote wanayo fursa ya kuendelea. Kwa kawaida hali sio hivyo katika rekodi na mashindano ya kidunia. Kama wewe ni muogeleaji, kwa mfano, unafan-ya mazoezi kwa bidii sana ili uweze kupata rekodi nzuri na kupanda juu zaidi, lakini kwa bahati mbaya, muda ambao waamuzi wanakubali kazi yako ni wakati unapoifanya kweenye mashindano rasmi. Kwa hiyo, kama wakati wa mazoezi yako au mashindano ya kirafiki unaweza kupandisha rekodi yako juu, waamuzi hao hawatakubali hata kama imepigwa picha na kutazamwa na watu wengi.

³² Ipo haja ya kutoa maelezo pambanuzi baina ya umoja kuhusu matendo (*tawhid-e afaali*) na kuyahusisha matendo mabaya ya watu kwa Mwenyezi Mungu. Mambo haya mawili yasichanganywe.

Kwa vyovyote vile, wale wanaothibitika kuwa na subira baada ya kupidia kwenye mitihani yote na majaribio yote, Mwenyezi Mungu anasema, **“Na wape bishara wanaosubiri!”³³** Lazima patakuwepo na thawabu nyingi kwa watu kama hao kwa Mwenyezi Mungu kumwambia Mtume Wake awape bishara watu hao. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu hatawapa watu kila kitu wanachotamani.³⁴ Bali Mwenyezi Mungu atawapa wenye kusubiri malipo zaidi sana hivyo kwamba watatosheka kikamilifu na kwa hakika itavuka mpaka wa matarajio yao, kwani itakuwa ni bila kipimo chochote:

إِنَّمَا يُؤْفَى الصَّابِرُونَ أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ

“....Hakika si mengineyo, wenye subira watapewa ujira wao bila ya hisabu.” [Surah Az-Zumar; 39:10]

³³ Qur`ani 2:155

³⁴ Ipo hadithi nzuri ambayo inaweza kutusaidia sisi kuelewa jambo hili vema. Nadir Shah Afshar (1688-1747, mtawala wa Irani ambaye alipanua himaya yake kutokea mto Indus hadi Milima ya Caucasus) wakati moja alikuwa akienda vitani na jeshi lake alipokutana na mvulana mdogo sana amebeba kitabu. Alimuuliza mvulana jina lake ni nani. Mvulana akajibu: “Nasr Allah” (Ushindi wa Mwenyezi Mungu). Mfalme akafurahi sana na akalichukulia tukio hilo kama ishara ya ushindi katika vita hiyo. Halafu mfalme alimuuliza mvulana yule alikuwa anakwenda wapi. Akajibu alikuwa anakwenda “Maktab,” ambako walijifunza masomo ya Qur`ani. Alipoulizwa na mfalme huko Maktab walijifunza nini mvulana akajibu: “Surah ya Al-Fath.” Mfalme alizidi kufurahi. Na akampa mvulana huyo dinari moja (sarafu ya dhahabu), lakini mvulana akaanza kulia. Nadir akamuuliza kwa nini alikuwa analia. Akajibu, “Ninalia kwa sababu ni-kienda nyumbani na mama yangu akiona hii mkononi mwangu, ataniuliza ‘Hii imetoka wapi?’” Nadir akasema, “Mwambie nimepewa na mfalme.” Akasema, “Hakika nitamwambia kwamba hii nimepewa na mfalme, lakini hatakubali.” Nadir akasema kwa nini. Akasema, “Mama yangu ataniambia kwamba kama mfalme akitoa kitu, hatoi dinari moja tu. Wafalme hutoa kwa wingi, kwa hiyo, hii haitoki kwa mfalme.” Nadir Shah aliamua kumpa rundo la dinari na akalichukua na akaenda nyumbani.

Si mara elfu moja zaidi, au hata mara milioni moja zaidi. Bali ni sawa na kumpa mtu hundi iliyo wazi (*blank cheque*). Kwa hiyo, kwa kadiri Mwenyezi Mungu ahusikanavyo, hakuna mpaka wowote ule ambao unaweza kuwa pale.

Mojawapo ya mambo ambayo tunayaona ndani ya Qur`ani kuhusu wenye kusubiri ni kwamba:

أُولَئِكَ عَلَيْهِمْ صَلَواتٌ مِّنْ رَبِّهِمْ وَرَحْمَةٌ

“Hao juu yao zitakuwa baraka zitokazo kwa Mola Wao, na rehema” (2:157).

Wenye kusubiri ni wale wanaopokea rehema za ziada ikiwa ni nyongeza ya neema ambazo kila mmoja hupokea kwa sababu ya mtazamo wao unaofaa kwenye ukarimu wa Mwenyezi Mungu na pia matatizo na majaribu yanayowapata.

Jambo la kupendeza zaidi ni kwamba, huwa tunasoma kwenye Ziyarah ya Ashura kwamba wale ambao wanaomboleza kweli kweli kwa ajili ya Imam Husayn (a.s.) na wakashirikiana naye katika maumivu yake na misiba yake wanaweza kutarajia kulipwa malipo ya wenye kusubiri na kupokea baraka na rehema Zake:

اللَّهُمَّ اجْعَلْنِي فِي مَقَامِي هَذَا مَمْنَنْ تَنَاهَى مِنْكَ صَلَواتٍ وَرَحْمَةٍ وَمَغْفِرَةً

“Ewe Mola Wangu! Nijaalie mionganini mwa wenye kupata baraka, rehma na maghfira kutoka Kwako.

Kwa hiyo, tatizo lolote linalokutokea linaweza kubadilika na kuwa bonasi kwako, kama ukifanya subira, na kuendelea kuwa nayo, na wakati wote uwe unatembea kwenye njia ili-yonyooka. Mnamo Siku ya Hukumu utaona kwamba kile ambacho umekipata kwa njia hii kinaweza kuwa kikubwa zaidi ya vile ulivyotegemea, kama vile matendo yako mema ya swala na saumu. Kwa hakika matendo mema ni ya muhimu sana na ya lazima, lakini kitendo kimoja kile tunachojua kuwa kinalipwa bila kipimo ni subira. Bila shaka, subira kama hiyo inawezekana tu kwa wale wanaotekeleza wajibu wao na kuomba msaada kutokana na vitendo vyao vyaa ibada na sadaka.

SEHEMU YA SABA

MUKHTASARI WA YALIYOPITA: Ndani ya makala ili-yopita, tulichunguza aina mbali mbali za miitikio kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu. Baadhi ya rehema zinapatikana kwa kila mtu, lakini wale wanaoonyesha shukurani wanajistahilisha wenyewe kupokea neema za ziada. Inafaa kutaja kwamba kuondolewa rehema kutoka kwa watu wasio na shukurani kunaweza kuwa ni rehema kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu kupokea neema za nyongeza kunahitaji wajibu mkubwa zaidi. Kwa mfano, kama mtu anakopa fedha kutoka benki na anaonyesha kwamba hana uwezo wa kuzitumia fedha hizo katika namna inayofaa, kumpa fedha ny-tingi zaidi kunaweza kuwa ni tatizo; badala yake, ni busara zaidi kuzuia kumpa fedha zaidi ili abakie na wajibu wa zile tu alizomiliki. Makala hii inalenga kwenye sifa za wale wanaostahili kupokea rehema za ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Wale wanaostahili kupokea rehema ya ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

1. Wenye Subira:

Kama tulivyosema katika sehemu iliyopita, mojawapo ya makundi yanayopokea rehema za ziada kwa wingi na zisizo na hesabu ni wale wenye subira. Maalumu tulitafakari juu ya aya (2:155-157).

2. Wenye kutenda mema:

Kundi lingine ni la ‘*Muhsinin*’ au watu wanaofanya matendo mema. Kwa Kiarabu, neno ‘*ihsan*’ au ‘kutenda mema’ linato-

kana na neno ‘*husn*’ maana yake ‘wema.’ Kwa hiyo, wanaofaidika na rehema ya Mwenyezi Mungu ni wale wanaofanya matendo mema:

وَلَا تُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ بَعْدَ إِصْلَاحِهَا وَادْعُوهُ خَوْفًا وَطَمَعًا
إِنَّ رَحْمَتَ اللَّهِ قَرِيبٌ مِنَ الْمُحْسِنِينَ

“Wala msifanye ujisadi katika ardhi baada ya kutengeneza kwake; na mwombeni kwa kuogopa na kwa kutumai. Hakika rehema ya Mwenyezi Mungu iko karibu na wanaofanya wema.” (7:56)

3 Wale wanaosikiliza Qur`ani kwa makini:

Wale wanaosikiliza Qur`ani inaposomwa wanapata rehema ya ziada. Wakati inaposomwa Qur`ani, watu hawapaswi kuzungumza, na mazungumzo yoyote yanayoendelea lazima yasitishwe. Hii ni kuonyesha heshima kwa Qur`ani na pia kunufaika kutohana na kusikiliza. Mwenyezi Mungu anase-ma:

وَإِذَا قِرَئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ وَأَنْصِثُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ

“Na isomwapo Qur`ani isikilizeni na mnyamaze ili mpage kurehemewa.” (Sura Al-A`raf, 7:204)

Mtu lazima asikilize Qur`ani huku anatafakari juu ya maneno yake badala ya kusikiliza tu. Mara nydingi huwa tunasikiliza sauti bila tafakuri juu ya maneno yake. Wakati tunapo-piga kanda ya Qur`ani majumbani mwetu au kwenye magari

yetu, tunaweza tukafanya kosa la kuzungumza na wengine wakati kanda inacheza. Qur`ani haitakiwi kutumika kama sauti nyuma ya sauti nyingine; inatakiwa kufanyiwa tafakuri kwa uangalifu wakati inasomwa. Kama kuna sababu yoyote ile inayothibitika kwamba inamzuia mtu asisikilize Qur`ani, inapendekezwa kuzima kanda hiyo.

Qur`ani inazungumza yenewe kama chimbuko la rehema (*rahmah*); kwa hiyo, si ajabu kwamba wale wanaosikiliza Qur`ani hujipatia stahili ya kupokea rehema za ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu:

وَنُنَزِّلُ مِنَ الْقُرْآنِ مَا هُوَ شَفَاءٌ وَرَحْمَةٌ لِلْمُؤْمِنِينَ لَا يَزِيدُ
الظَّالِمِينَ إِلَّا خَسَارًا

“Na tunateremsha katika Qur`ani ambayo ni ponyo na rehema. Wala haiwazidishii madhalimu isipokuwa hasara.” [Sura Bani Israil, 17:82]

Njia moja ya kufaidika na rehema hii ni mtu kutilia maa-nani kwa heshima yale yaliyomo humo na kuweka wazi moyo na akili yake kuweza kupokea nuru na mwongozo wa Qur`ani.

4. Wale wanaoswali usiku (*salatul-layl*) hupokea rehema za ziada:

Wale wanaomwomba Mwenyezi Mungu kwenye swala za usiku wa manane na kabla ya swala ya asubuhi (al-Fajri) hupokea rehema za ziada:

أَمَنْ هُوَ قَاتِنٌ آنَاءَ اللَّيْلِ سَاجِدًا وَقَائِمًا يَحْذِرُ الْآخِرَةَ وَيَرْجُو
 رَحْمَةَ رَبِّهِ قُلْ هَلْ يَسْتَوِي الَّذِينَ يَعْلَمُونَ وَالَّذِينَ لَا يَعْلَمُونَ^{٢٤}
 إِنَّمَا يَتَذَكَّرُ أُولُو الْأَلْبَابِ

“Je, Afanyaye ibada nyakati za usiku kwa kusujudu na kusimama akitahadhari na Akhera, na akitaraji rehema za Mola Wake: Sema: Je, wanalingana sawa wale ambao wanajua na wale ambao hawajui? Hakika wanaokumbuka ni wenye akili tu.” (Sura Az-Zumar, 39:9)

Mwenyezi Mungu analinganisha makundi mawili: kundi moja ni la wale wanaofanya ibada nyakati za usiku na linatahadhari kuhusu mambo ya Akhera likiwa linatarajia kupokea rehema za Mwenyezi Mungu. Kundi la pili halikutajwa. Lakini kwa ulinganishaji tunatambua kwamba ni lenye watu wenye kupuuza na hutumia muda wao mwingi wa usiku wakitenda dhambi. Ni dhahiri kwamba wale wanaomkumbuka Mwenyezi Mungu wakati wa mchana na kutenda matendo mema na halafu usiku, ambao ni wakati wa kupumzika, wanaona mapumziko yao katika kumcha Mwenyezi Mungu, wakiomba maghfira, na kusoma Qur`ani hawatapewa rehema sawa na wale wanaoshindwa kufanya hivyo.

5. Walio Wema:

Kundi lingine linalostahili rehema zaidi kutoka kwa Mwenyezi Mungu ni wale ambao ni wema (*salihin*). Mwenyezi Mungu anasema katika Surah Al-Anbiyaa, 21:75

وَأَدْخِلْنَاهُ فِي رَحْمَتِنَا إِنَّهُ مِنَ الصَّالِحِينَ

“Na Tukamwingiza yeye (Lut) katika rehema Zetu. Hakika yeye ni mionganoni mwa walio wema.”

[Sura Al-Anbiyaa, 21:75]

Kufuatana na aya hii, Nabii Lut (a.s.) hakupokea hivi hivi tu rehema maalum kutoka kwa Mwenyezi Mungu; bali hasa, aliiingizwa kwenye rehema ya Mwenyezi Mungu kwa sababu alikuwa mtenda mema. Mtu mwema anatarajiwa kufanyiwa hivyo hivyo: anawekwa katikati ya bahari ya rehema ya Mwenyezi Mungu.

6. Wale wanaoomba msamaha:

Wale wanaoomba msamaha kutoka kwa Mwenyezi Mungu wanatarajiwa kupokea rehema za ziada.

إِنَّهُ كَانَ فَرِيقٌ مِنْ عِبَادِي يَقُولُونَ رَبَّنَا آمَنَّا فَاعْفُرْ لَنَا
وَارْحَمْنَا وَأَنْتَ خَيْرُ الرَّاحِمِينَ

“Hakika lilikuwapo kundi katika waja Wangu likisema: Mola Wetu tusamehe na uturehemu, na Wewe ndiwe Mbora wa wanaorehemu.” (Sura Al-Mu`minun, 23:109).

Kama swala yao na maombi yao ya kusamehewa na kuperwa rehema ya Mwenyezi Mungu havikuleta matokeo, Mwenyezi Mungu asingetaja tukio hili ndani ya Qur`ani. Kama swala hii ilikuwa batili, Mwenyezi Mungu hangewasifu wao kwa swala hii. Kwa hiyo, tunapaswa kuamini kwamba

maombi kama haya kwa hakika huleta matokeo yanayotarajiwa; kwa hiyo, ni jambo la busara kujifunza maombi haya na kuyakariri katika kunuti zetu (*qunut* – du'a wakati wa swala za wajibu) au kwa ajili ya wakati mwingine wowote. Aya zingine ndani ya Qur`ani pia zinarejelea kwenye mapendek-ezo ya kuomba msamaha:

قَالَ يَا قَوْمِ لَمْ تَسْتَعْجِلُونَ بِالسَّيِّئَةِ قَبْلَ الْحَسَنَةِ ۖ لَوْلَا
تَسْتَغْفِرُونَ اللَّهُ لَعَلَّكُمْ تُرَحَّمُونَ

“Akasema: Enyi watu wangu! Kwa nini mnahimiza uovu kabla ya wema? Mbona hamuombi maghfira kwa Mwenyezi Mungu mpage kurehemiwa?” [Sura An-Naml, 27:46]

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَلِأَخِي وَأَدْخِنَا فِي رَحْمَتِكَ ۖ وَأَنْتَ أَرْحَمُ
الرَّاحِمِينَ

“Akasema: Mola Wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu na utuingize katika rehema Yako na Wewe ni Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.”

[Sura Al-A`raf, 7:151] 35

7. Wale wanaoombewa na malaika:

Wapo watu ambao hupokea rehema za ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu wao huombewa na malaika. Kwa nyongeza ya maombi ya jumla ya malaika ya kuwaombea waumini mfano unaoonekana ndani ya aya kama 40:7,

³⁵ Angalia pia: 2:286, 7:23; 149; 155 na 23:118

Qur`ani inarejelea kwenye mifano maalumu ambamo malai-ka wamemwomba Mwenyezi Mungu kushusha rehema Zake kwa watu fulani. Mathalani, pale ambapo malaika walimpa Nabii Ibrahim (a.s.) habari njema za kupata mtoto, mke wake alishtuka kwa sababu alikwishazeeka na mkewe alikuwa mgumba. Malaika wakasema:

قَالُوا أَتَعْجِبُنَّ مِنْ أَمْرِ اللَّهِ وَرَحْمَتُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ عَلَيْكُمْ أَهْلُ
الْبَيْتِ إِنَّهُ حَمِيدٌ مَحِيدٌ

“Wakasema: Unastaajabu amri ya Mwenyezi Mungu? Rehemha ya Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziko juu yenu enyi watu wa nyumba hii. Hakika Yeye ni Mwenye kusifiwa Mwenye kutukuzwa.” [Sura Hud, 11:73]

Fungu la maneno “Rehema na Baraka za Mwenyezi Mungu ziwe juu yenu” linaweza kuwa ni tamko, lakini linaelekea zaidi kuwa du'a inayosema , “Amani na rehema ziwe juu yenu!” Kwa hiyo, panapokuwepo na wenyenye nyumba wazuri, yaani, pale ambapo baba na mama ni watu wema, wacha Mungu na wana watoto wema, upo uwezekano mkubwa sana kwamba malaika watawaombea du'a watu wa nyumba hii; malaika wataomba dua, watamwomba Mwenyezi Mungu kuipa familia hiyo rehema za ziada na kuwapendelea zaidi.

8. Wale wanaohama na kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu:

Kundi lingine la watu linalotarajiwa kupewa rehema ya ziada ni la wale waliohama na kupambana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُولَئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ

“Hakika wale walioamini na wale waliohamma na wakapiga-na katika njia ya Mwenyezi Mungu, hao ndio wenye kuta-raji rehema ya Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kughufiria, Mwenye kurehemu.”

[Sura al-Baqarah, 2:218]

Aya nyingine ni Sura Al-Tawbah, 20:20-22:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَالَّذِينَ هَاجَرُوا وَجَاهَدُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ أُولَئِكَ يَرْجُونَ رَحْمَتَ اللَّهِ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ يُبَشِّرُهُمْ بِرَحْمَةٍ مِنْهُ وَرِضْوَانٍ وَجَنَّاتٍ لَهُمْ فِيهَا نَعِيمٌ مُقِيمٌ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا إِنَّ اللَّهَ عِنْدَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ

“Wale walioamini na wakahama na wakapigana jihadi ka-tika njia ya Mwenyezi Mungu, kwa mali zao na nafsi zao, wana cheo kikubwa mbele ya Mwenyezi Mungu, na ndio wenye kufuzu. Mola wao anawabashiria rehema kutoka Kwake na radhi na Pepo zitakazodumu. Watadumu humo milele. Hakika kwa Mwenyezi Mungu kuna malipo makub-wa.” [Sura At-Tawba, 9:20-22]

Uhamaji unaweza kutumika leo; haukuhifadhiwa kwa ajili ya wale waliohamma kutoka Makka kwenda Madina. Labda unaweza kutumika kwa mhamaji yejote anayeondoka kwe-nye makazi yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, kwa ajili ya

wale wanaohama ili kulinda imani zao, kutekeleza imani zao, au kufanya kazi ya msaada. Kwa hiyo, ye yote anayeondoka kwenye makazi aliyolelewa na kukulia na kwenda mahali pengine kwa ajili ya Mwenyezi Mungu huitwa muhajirina.

Jihaad: Maana yake ni kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Hii inaweza kuwa kwa njia ya elimu, kilimo, au tiba. Inaweza pia kuhusisha utekelezaji wa nguvu halali kulinda rasilimali ya mtu, familia, au taifa kutegemea mazingira na kuhusu nini kinachohitajika kwa ajili ya ustawi wa familia ya mtu, taifa, au wanadamu wote. Kufanya kazi kwa bidii ili kupata fedha za kutosha kwa matumizi ya familia ya mtu, kwenye hadithi inachukuliwa kuwa ni mfano wa jihadi. Imam Sadiq (a.s.) amenukuliwa akisema:

الكاف على عياله كالمجاهد في سبيل الله

“Yeyote anayejitatihidi kupata kipato kwa ajili ya familia yake ni sawa na mpiganaji anayepigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.”³⁶

Mwalimu mwenye kudhamiria kufanya kazi ya kuwaelimisha watu ni mfano wa jihadi. Mkulima anayefanya kazi sana kwa ajili ya Allah ili awapatie watu chakula ni mfano wa jihadi. Mtu anayelinda nchi yake pia ni mfano wa jihadi. Kwa hiyo, jihadi ni dhana pana sana ambayo inajumuisha mapambano yoyote kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Kufuatana na aya hizo hapo juu, wale wanaoamini na wale wanaohama na kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu wa-

³⁶ *Al-Kafi*, Jz. 5, uk. 88, hadithi ya I, Jz. 9, uk. 566, Hadithi ya 8436 & *Man La Yahdhuru hul-Faqih*, Jz. 3, uk. 168, Hadithi ya 3631

natarajiwa kupokea rehema maalumu kutoka kwa Mwenyezi Mungu, na mapungufu yoyote ambayo yamefanywa siku za nyuma yatasamehewa.

9. Watiifu:

Wale wanaomtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake wanatarajiwa kupokea rehema nyingi zaidi:

فَأَمَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ فَيُذْخَلُهُمْ رَبُّهُمْ فِي
رَحْمَتِهِ هُوَ الْفَوْزُ الْمُبِينُ

“Ama wale walioamini na wakatenda mema, Mola Wao atawaingiza katika rehema Yake. Huko ndiko kufuzu kulio wazi.” [Sura Al-Jathiyah, 45:30]

وَأَطِيعُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ تُرَحَّمُونَ

“Na Mtini Mwenyezi Mungu na Mtume ili mpate kurehemawa.” [Sura Al-Imran, 3:132]

Watu watifi ni pamoja na wale wanaoamrisha mema na kukataza mabaya, wanaosimamisha sala, wanaotoa sadaka:

وَالْمُؤْمِنُونَ وَالْمُؤْمِنَاتُ بَعْضُهُمْ أَوْلَيَاءُ بَعْضٍ يَأْمُرُونَ
بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَا عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُقِيمُونَ الصَّلَاةَ وَيُؤْتُونَ
الزَّكَاةَ وَيُطِيعُونَ اللَّهَ وَرَسُولَهُ هُنَّ أُولَئِكَ سَيِّرْ حَمْهُمُ اللَّهُ عَزِيزٌ حَكِيمٌ

“Na waumini wanaume na waumini wanawake ni marafiki wao kwa wao; huamrishana mema na hukatazana maovu, na husimamisha swala, na hutoa zaka, na humtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Hao Mwenyezi Mungu atawarehemu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu na Mwene-nye hekima.” [Sura At-Tawbah, 9:71]

Waumini wanaume na waumini wanawake waangalizi wa wao kwa wao. Matokeo yake, wanayo haki ya kuamrishana kutenda mema na kuzuiana kutenda maovu. Chochote kinachotokea kwa muumini mmoja kinaunganishwa na kwa muumini mwingine; kwa hiyo, inatarajiwu kwamba waumini wawe tayari kukubali ukosoaji wenye ujenzi na maaso bila kufikiri kwamba hapana hata mtu mmoja mwenye haki ya kuingilia mambo yao. Hapana shaka, mazingira ya kutekeleza haya yametajwa kwenye uwanja wa sheria za Kislamu, au fiqh. Kwa mfano, kama nikimuona ndugu yangu anakula kitu chenye sumu, je mimi hapa siwajibiki? Hivyo, itakuwaje nisihisi kuwajibika nikimuona, mathalani, anasikiliza muziki ulioharamishwa, yaani muziki unaowafaa makundi ya watu waovu? Hakika mimi ninawajibika. Hii ni tofauti na kuingilia mambo ya watu. Pamoja na kwamba hutaki kufanya hivyo, tunapomuona mtu anafanya uovu, tunawajibika kwa kumwambia mtu huyo kwa njia ya hekima na adabu njema inay-oweza kumzuia asiendelee na kitendo hicho.

Kwa hali yoyote ile, aya hiyo hapo juu inaonyesha kwamba kama unaamrisha mema na kukataza maovu, na unasihamisha swala, unatoa zaka, na kwa ujumla unamtii Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, ungeweza kupata rehema ya Mwenyezi Mungu baada ya muda mfupi. Mfano kama huo unaonekana kwenye aya ifuatayo:

وَأَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَأْتُوا الزَّكَاءَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ لَعَلَّكُمْ
تُرْحَمُونَ

**“Na simamisheni Swala na toeni Zaka na mtiini Mtume ili
mpate kurehemiwa.” [Sura An-Nur, 24:56]**

Kuwa mtiifu maana yake ni kuwa na ‘takua’, yaani, kumhofia Mwenyezi Mungu na kujilinda mwenyewe. Hili linatoka kwenye asili ya “wa-qa-ya” ambalo maana yake ni ‘kujinusuru’ au ‘kujilinda’ mwenyewe usifanye matendo maovu na yenyeye kudhuru, yale ambayo husababisha chukizo kwa Mwenyezi Mungu. Takua ni aina ya kinga dhidi ya vijidudu vyote na uchafu wote. Kwa nyongeza ya aya kuhusu utiifu kwa Mwenyezi Mungu, zipo aya zinazonyesha kwamba takua huongoza kwenye kupatikana rehema za ziada:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا اللَّهَ وَآمِنُوا بِرَسُولِهِ يُؤْتَكُمْ كَفَلْيَنِ مِنْ
رَّحْمَتِهِ وَيَجْعَلُ لَكُمْ نُورًا تَمْشُونَ بِهِ وَيَغْفِرُ لَكُمْ وَاللَّهُ غَفُورٌ
رَّحِيمٌ

“Enyi mliaoamini! Mcheni Mwenyezi Mungu, na mwaminini Mtume Wake, atawapa sehemu mbili katika rehema Yake, na atawajaalia muwe na nuru ya kwenda nayo, na atawa-ghufiria. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghufira, Mwenye kurehemu.” [Sura Al-Hadid, 57:28]

وَاكْتُبْ لَنَا فِي هَذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ إِنَّا هُدْنَا إِلَيْكَ ۝
 قَالَ عَذَابِي أُصِيبُ بِهِ مَنْ أَشَاءَ ۖ وَرَحْمَتِي وَسِعْتُ كُلَّ شَيْءٍ ۝
 فَسَأَكْتُبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤْمِنُونَ الزَّكَةَ وَالَّذِينَ هُمْ بِآيَاتِنَا
 يُؤْمِنُونَ

“Na utuandikie mema katika dunia hii na katika akhera. Sisi tunarejea Kwako. Akasema: Adhabu Yangu nitamsibu nayo nimtakaye; na rehema yangu imekienea kila kitu; nitaiandika kwa ajili ya wale wanaoogopa, na wanaotoa Zaka na wanaoziamini Ishara Zetu.” [Sura Al-A`raf, 7:156]

وَهَذَا كِتَابٌ أَنزَلْنَاهُ مُبَارَكٌ فَاتَّبِعُوهُ وَاتَّقُوا لَعْلَكُمْ تُرْحَمُونَ

“Na hiki ni Kitabu tulichokiteremsha kilichobarikiwa. Basi kifuateni na muwe na takua ili mrehemewe.”

[Sura Al-Anam, 6:155]

Katika nyongeza ya rehema za ziada, Mwenyezi Mungu huwapa wale wenye takua uwezo wa kutambua kwa urahisi wema na uovu:

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِنْ تَنَتَّوْا اللَّهُ يَجْعَلُ لَكُمْ فُرْقَانًا وَيُكَفِّرُ عَنْكُمْ
 سَيِّئَاتِكُمْ وَيَغْفِرُ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ

“Enyi miloamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atawajaalia upambanuzi, na atawafutia makosa yenu na atawasamehe; na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kuu.”

[Sura Al-Anfal, 8:29]

Furqaan ni kitu ambacho kwacho unaweza kutofautisha baina ya wema na uovu. Hii ni nguvu ya takua. Yule ‘Mutaqqi’, au mtu mwenye takua, kwa haraka anaweza ku-pambanua baina ya wema na uovu, kama ilivyo kinyume na wale wanaochukua muda mrefu kuamua:

إِنَّ الَّذِينَ آتَقْوَا إِذَا مَسَّهُمْ طَائِفٌ مِّنَ الشَّيْطَانِ تَذَكَّرُوا فَإِذَا هُمْ
مُبْصِرُونَ

“Hakika wale wenye takua zinapowagusa pepesi za shetani huzinduka.” [Sura Al-A`raf, 7:201]³⁷

Pia Mwenyezi Mungu huwapa wale wenye takua aina maalumu ya elimu:

وَيُعْلَمُكُمُ اللَّهُ وَاللَّهُ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمٌ

“.....Na mcheni Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu atawaelimisha; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi kwa kila kitu.” [Sura Al-Baqarah, 2:282]

Kwa hiyo tunaweza kuhitimisha kwamba matendo mema ya muumini humfanya astahili yeye kupokea rehema ya ziada. Matendo mema yanaweza kujumuisha kuomba msamaha, kuswali swala za usiku wa manane (*salat al-layl*), kutoa zaka, na kuamrisha mema na kukataza maovu (*al-amr bi-lma ruf*). Aina mbali mbali za aya zilizotajwa hapo juu zinase-

³⁷ “Nuru ya kwenda nayo” (57:28) wanayopewa wacha Mungu huwasaidia wao kuelewa vema zaidi na kwa hiyo huwasaidia kufanya uamuzi bora zaidi na kutenda matendo mema zaidi.

ma wazi kabisa kwamba watu wenye imani na ucha Mungu na wenye kutenda mema wanatarajiwa kupokea rehema za ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

ANGALIZO - 1. Kwa mujibu wa Qur`ani, waumini wanatakiwa kuusiana wao kwa wao kuwa na huruma, na Mwenyezi Mungu anawasifu wafanyao hivyo:

ثُمَّ كَانَ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ وَتَوَاصَوْا
بِالْمَرْحَمَةِ

“Kisha akawa mionganoni mwa walioamini na wakatenda mema, wakausiana kusubiri na wakausiana kuhurumiana.”

[Sura al-Balad 90:17]

Waumini huusiana wao kwa wao kuwa na subira na huruma. Endapo mtu anasahau kuwa na subira na huruma, mwenzake anapaswa kumuusia na kumkumbusha pale anaposahau. Mahali pengine Qur`ani inasisitiza haja ya kuusiana wenye kwa wenye kuzingatia haki na kuwa na subira:

إِنَّ الْإِنْسَانَ لَفِي خُسْرٍ إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ
وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ

“Hakika mtu bila shaka yumo katika hasara. Ila wale walioamini, na wakatenda mema, na wakausiana haki, na wakausiana kusubiri.” [Sura al-Asr 103: 2-3]

Kwa hiyo, waumini wanatakiwa kuusiana wao kwa wao kuzingatia huruma, haki, na subira.

ANGALIZO - 2: Kwa mujibu wa Qur`ani, Mwenyezi Mungu ameweuka huruma ndani ya nyoyo za mume na mke na ndani ya nyoyo za wafuasi wa Isa (a.s.):

وَمِنْ آيَاتِهِ أَنْ خَلَقَ لَكُمْ مِنْ أَنْفُسِكُمْ أَرْوَاجًا لِتَسْكُنُوا إِلَيْهَا
وَجَعَلَ بَيْنَكُمْ مَوَدَّةً وَرَحْمَةً إِنَّ فِي ذَلِكَ لَآيَاتٍ لِفَوْمٍ يَنَقْرُونَ

“Na hakika Ishara Zake ni kuwaumbia wake zenu kutokana na nafsi zenu ili mpate utulivu kwao, na akajaalia mapenzi na huruma baina yenu. Hakika katika haya kuna Ishara kwa watu wanaofikiri.” [Sura Ar-Rum, 30:21]

ثُمَّ قَفَّيْنَا عَلَى آثَارِهِمْ بِرُسُلِنَا وَقَفَّيْنَا بِعِيسَى ابْنِ مَرْيَمَ وَأَتَيْنَاهُ
الْإِنْجِيلَ وَجَعَلْنَا فِي قُلُوبِ الَّذِينَ اتَّبَعُوهُ رَأْفَةً وَرَحْمَةً

“Kisha tukafuatisha nyuma yao Mitume Wetu, na tukam-fuatisha Isa bin Maryam, na tukampa Injili. Na tukajaalia katika nyoyo za waliomfuata upole na rehema.....”

[Sura Al-Hadid, 57:27]

Watu wawili wanapooana, Mwenyezi Mungu hujaalia mapenzi na huruma ndani ya nyoyo zao kwa ajili ya wao kwa wao. Mapenzi yanaweza kuhitaji kuwa ya kutendeana, lakini huruma haina masharti, mmojawao anaweza kuonyesha huruma kwa mwagine bila kupokea chochote kutoka upande

wa pili, kama vile kumhudumia mwenza mgonjwa ambaye hawezi kumfanyia mwenzake lolote.

Vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu ameweka mapenzi na huruma ndani ya nyoyo za wale waliomfuata Isa (a.s.). Hili linaweza kuwa ni neno la Mwenyezi Mungu tu kwa sababu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) alileta dini mpya na aliwaita watu wengine kuamini ujumbe wake, pamoja na kwamba bado anakubali sifa za imani za jumuiya nyinginezo. Qur`ani pia inapendezewa na kazi nzuri ya wachungaji na watawa wa Ki-Kristo:

وَلَتَجِدَنَّ أَفْرَبَهُمْ مَوَدَّةً لِلَّذِينَ آمَنُوا إِنَّا نَصَارَىٰ
ذَلِكَ بِأَنَّ مِنْهُمْ قَسِيسِينَ وَرُهْبَانًا وَأَنَّهُمْ لَا يَسْتَكْبِرُونَ

“Na utawakuta walio karibu zaidi kwa mapenzi na waumini ni wale waliosema: Sisi ni manaswara (wakristo). Hayo ni kwa sababu wako mionganoni mwao makasisi na watawa na kwamba wao hawafanyi kiburi.” [Sura Al-Maidah, 5:82]

Baadhi ya watu wanaweza kutaraji kwamba Qur`ani lazima isizungumze kuwapendelea wachungaji wa dini pinzani, lakini hii si njia ambayo Qur`ani inaliendea suala hili. Qur`ani inakubaliana na kazi nzuri ambayo hufanywa na wachungaji na watawa. Pia inasifu unyenyekevu wa Wakristo hao. Hili lazima liwe neno la Mwenyezi Mungu.

Qur`ani pia inazungumzia uelekeo kwenye maisha ya utawa mionganoni mwao kitu ambacho hakikusemwa na Mwenyezi Mungu, lakini walikianzisha wao wenyewe kwa lengo la kumridhisha Mwenyezi Mungu, na baadaye wen-

gine walishindwa kuzingatia masharti yake.³⁸ Labda kila mara pamekuwepo na watawa wazuri, lakini pia unaona kwamba katika historia, hususani katika kipindi cha zama za kati, baadhi ya watawa ambao walipaswa kukana anasa za kidunia, wao wenyewe wakahusika na kutumia vibaya mamlaka na kujikusanya mali. Bila shaka, Qur`ani hailichukulii kijumla hili: inawaondoa baadhi yao (57:27) na inaongezea kwamba mwanzoni nia yao ilikuwa nzuri.

³⁸ “.....Na utawa wameuzua wao. Hatukuwaandikia hayo - ila kutafuta radhi za Mwenyezi Mungu. Lakini hawakuufuata inavyotakiwa kuufuata. Basi wale walioamini katika wao tuliwapa ujira wao. Na wengi wao ni mafasiki.” [57:27]

SEHEMU YA NANE

MUKHTASARI WA YALIYOPITA: Sehemu iliyotan-gulia ya mlolongo wa makala hizi iligusia juu ya sifa za wale wenye kufuzu kupokea rehema za ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu yaani wenye subira, wenye kutenda mema, waadilifu, wenye kutubia, watiifu, na wale wanaohama na kupigana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu. Sehemu hii ya mwisho inachunguza rehema ya Mwenyezi Mungu kama ilivyooonyeshwa katika njia ya namna ambavyo Mwenyezi Mungu hufanya malipo. Furaha yetu huko Akhera inatege-mea juu ya imani na matendo yetu, na tunahitaji maandalizi ya kutosha kwa ajili ya safari ya milele iliyoko mbele yetu. Kwa kuwa inawezekana kwamba watu huwa na muelekeo wa kutia chuku matendo yao machache, inawezekana tusi-jue umbali halisi na kudumu kwa safari hii ngumu. Mwenyezi Mungu, kutokana na rehema Zake nyingi, hutusaidia sisi kwa njia mbali mbali kutuwezesha sisi kupata maandalizi ya kutosha. Baadhi ya sifa za malipo ya Ki-Mung ni pamoja na: 1) kuwalipa watu wenye nia njema, ingawa sio kuwa-adhibu kwa matendo yao mabaya, 2) kuzidisha thawabu kwa ajili ya matendo mema, ingawa adhabu kwa ajili ya matendo mabaya haizidishwi, 3) malipo kwa ajili ya matendo yaliyopendekezwa kama ilivyosisitizwa ndani ya hadithi hata kama hadithi si thabiti. 4) kuwalipa wacha-Mungu kufuatana na utendaji wao mzuri tena bila kipimo. 5) kubadilisha dhambi kuwa matendo mema. 6) kuwasamehe watu kupitia uombezi na kwa wale wenye matumaini juu ya msamaha Wake. Kwa wakati huo huo, watu wanatakiwa kudumisha uwiano marid-hawa baina ya kukata tamaa na kuridhika na matendo yetu

ili kwamba tuwe na matumaini na tudhamirie kujitahidi katika kufanya matendo mema ili kapita juu ya njia iliyonyooka kuelekea kwa Mwenyezi Mungu wa milele.

Furaha yetu katika Akhera inategemea juu ya imani yetu, matendo yetu, na ubora ambao tumeupata kama matokeo ya matendo hayo hapa duniani. Tunayo safari ya milele mbele yetu na tunahitaji maandalizi ya kutosha kwa ajili ya safari hiyo. Jinsi safari yako ilivyozidi ndefu, ndivyo utakavyohitaji maandalizi zaidi. Kwa hiyo hatuwezi kuamua kama maandalizi yetu yanatosha au la isipokuwa tuwe tunajua umbali tutakaosafari. Hivyo, tunaweza tu kujua kama matendo yetu yanatuandalia sisi maandalizi ya kutosha kwa ajili ya safari yetu kama tunajua safari hii itadumu kwa kipindi gani. Kwa kuwa sisi hatuna ufahamu mzuri wa urefu wa safari hii na itachukua muda gani, upo uwezekani kwamba tunaweza kufikiria matendo yetu machache kama yanatosha, kwamba tumelimbikiza masurufu ya kutosha: tunazo swala nyingi sana, saumu, ziyara nyingi kuwazuru watu watakatifu (*ziyarat*), hijja, na tumetoa sadaka nyingi (*sadaqah*). Hata hivyo, wale wenye uelewa sahihi wa umbali na changamoto zinazokabiliwa hufikiria tofauti. Imam Ali (a.s.) pamoja na ucha – Mungu wake wote kwa uaminifu na huduma kubwa kwa Uislamu – alipotazama safari hii na matendo yake, yeye alisema:

آه من قلة الرزاد و بعد السفر و وحشة الطريق

“Ah! Masurufu ya safari ni machache, safari ni ndefu na njia ina upweke!”³⁹

³⁹ Sharh Nahj al-Balaghah, Ibn Abi al-Hadid, Jz. 18, uk. 226

Imam Ali (a.s.) alihisi kuhusika pale alipokumbuka masurufu yake madogo kwa upande mmoja na safari ndefu ya kusafiri kwenye upweke kwa upande mwingine. Hii ni safari ambayo kila mtu anawajibika kuisafiri yeye mwenyewe. Pamoja na kwamba mtu anaweza kuwa na wasafiri wenzake, kila mtu atabeba mzigo wake mwenyewe. Kwa kurudia mara nydingi Qur`ani inasema: “....hakuna mtu atakayebeba mzigo wa mwenzake.” Ndani ya aya nydingine, tunasoma:

قُلْ أَغِيرَ اللَّهُ أَبْغِي رَبًا وَهُوَ رَبُّ كُلِّ شَيْءٍ وَلَا تَكْسِبُ كُلُّ
نَفْسٍ إِلَّا عَلَيْهَا وَلَا تَزِرُّ وَازْرَةٌ وِزْرَ أُخْرَىٰ ثُمَّ إِلَىٰ رَبِّكُمْ
مَرْجِعُكُمْ فَيُنَبِّئُكُمْ بِمَا كُنْتُمْ فِيهِ تَخْلِفُونَ

“Sema: Je, nimtafute Mola mwingine asiyekuwa Mwenyezi Mungu; na hali Yeye ni Mola wa kila kitu? Na kila nafsi haichumii ila (unajichumia) yenyewe. Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. Kisha marejeo yenu ni kwa Mola Wenu, naye atawaambia yale mliyokuwa mkihitilafiana.”

[Surah al-Anam, 6:164]

وَلَا تَزِرُّ وَازْرَةٌ وَإِنْ تَدْعُ مُثْقَلَةً إِلَىٰ حِمْلِهَا لَا
يُحْمَلْ مِنْهُ شَيْءٌ وَلَوْ كَانَ ذَا قُرْبَىٰ إِنَّمَا تُنْذِرُ الَّذِينَ يَخْشَوْنَ
رَبَّهُمْ بِالْغَيْبِ وَأَقَامُوا الصَّلَاةَ وَمَنْ تَرَكَىٰ فَإِنَّمَا يَتَرَكَّىٰ
لِنَفْسِهِ وَإِلَى اللَّهِ الْمَصِيرُ

“Wala mbebaji hatabeba mzigo wa mwingine. Na kama aliyelemewa akiomba achukuliwe mzigo wake, hautachuku-

liwa hata kidogo, ingawa ana ujamaa. Hakika unawaonya wale tu wamchao Mola Wao kwa ghaibu na wakasimamisha swala. Na anayejitakasa, basi anajitakasa kwa ajili ya nafsi yake. Na marejeo ni kwa Mwenyezi Mungu.”

[Surah al-Fatir, 35:18]

1. Mahali pengine Imam Ali (a.s.) anasema:

آه من قلة الزاد وطول الطريق و بعد السفر و عظيم
المورد 40

“Ah! Masurufu ni machache sana, njia ni ndefu sana, safari ni ndefu sana, na mahali pa kituo ni pakubwa sana.”⁴¹

Alipofariki dunia Salman al-Farsy, Imam Ali (a.s.) aliandika juu ya kaburi lake:

وَفَدْتُ عَلَى الْكَرِيمِ بِغَيْرِ زَادٍ مِنَ الْحَسَنَاتِ وَالْقَلْبِ السَّلِيمِ
فَحَمَلَ الزَّادَ أَقْبَحَ كُلَّ شَيْءٍ إِذَا كَانَ الْوَفُودُ عَلَى الْكَرِيمِ

“Nimewaita wakarimu bila ya masurufu ya matendo mema na bila ya moyo safi.

Kubeba masurufu yako ni makosa pale am-bapo unakwenda kukaribishwa na wakarimu.”

⁴⁰ Sharh Nahj al-Balaghah, Ibn Abi al-Hadid, Jz, 18, uk. 224

⁴¹ Hii inarejelea kwenye aya ya 19:71 &72: “Hakuna mionganini mwenu ila ni mwenye kuifikia. Ni hukumu ya Mola Wako, ni lazima itimizwe. Kisha tutawaokoa wale wenye takua na tutawaacha madhalimu hapo wamepiga magoti.”

منها ج البراعة في شرح نهج البلاغة و تكلمة منها ج البراعة ج 6 ص 63

Hivyo kwa kujua kwamba safari yenyewe ni ngumu sana, Mwenyezi Mungu, kutokana na rehema Yake, hutusaidia sisi katika njia mbali mbali ili atuwezeshe kupata masurufu ya kutosha.

Tunapoelewa namna Mwenyezi Mungu anavyotulipa, wakati huo huo hatutakata tamaa kamwe wala kujivunia matendo yetu. Uelewa huu wenye kuwiana unatupa matumaini makubwa na dhamira ya kufanya matendo mema kadiri iwezekanavyo ili kuendelea na safari yetu kuelekea kwa Mwenyezi Mungu wa milele. Hata kama tanaweza kutenda tendo zuri moja zaidi, tunapaswa kulifanya, na ingawaje tunajua kwamba kitendo chetu chenyewe kinaweza kisiwe muhimu, tusingweza kupoteza matumaini wala ku-poteza fursa yoyote ya kufanya jitihada zaidi, kwa sababu hata matendo madogo, baada ya kukubaliwa na kukuzwa na Mwenyezi Mungu, yanakuwa na umuhimu. Ni sawa na pale mtu anapotuambia kwamba kama tukiweka dola moja (\$1) yeye ataongeza dola (\$999), na jumla kuwa dola (\$1000). Ingawaje dola (\$1) haina thamani, ni muhimu kui-weka kwa sababu hiyo ilikuwa ndio njia pekee ya kupata (\$1000). Tunapaswa kuleta mchango wetu mdogo, halafu Mwenyezi Mungu atauzidisha, lakini kama tukileta sifuri, hata kama ikizidishwa mara maelfu, bado itabakia ni sifuri tu.

2. Sifa za malipo ya thawabu:

Malipo ya Mwenyezi Mungu ni mapana kwa maana kwamba hapana kitendo kizuri ambacho kitapuuzwa, hata kama ni kidogo sana. Katika aya nyingi, Qur`ani inaonyesha kwamba yote yale ufanyayo yatahesabiwa. Bila shaka, kila

jema tunalofanya linatoka Kwake, kwa sababu mimi na yote yale yaliyoko chini ya mamlaka yangu ni ya Kwake na kwa hiyo mimi sistahili kupata malipo yoyote kutoka Kwake; bado, Yeye ananihakikishia mimi kwamba nital-ipwa thawabu:

وَأَنَّ اللَّهَ لَا يُضِيغُ أَجْرَ الْمُؤْمِنِينَ

“.....na kwamba Mwenyezi Mungu hapotezi ujira wa waumini.” [Surah al-Imrani, 3:171]

إِنَّا لَا نُضِيغُ أَجْرَ الْمُصْلِحِينَ

“..... Hakika Sisi hatupotezi ujira wa watendao mema.”
[Surah al-A`raf; 7:170]

Katika aya nyingi, Mwenyezi Mungu anatutaka sisi tusiwe na wasiwasi kama ujira Wake utapotea au kusahauliwa. Kwani anajua kwamba sisi tuna tabia ya kuwa na shaka haraka na labda bila kutambua kuhusu yote yale ambayo tunaahidiwa hata kama ni Mwenyezi Mungu. Wakati wote huwa anatutuliza sisi. Pamoja na kwamba inawezekana tusiyaone malipo Yake kwa sasa hivi, hili lisingebadilisha uhalsia wa mambo. Unapokuwa na uhakika kuhusu jambo fulani, kwa mfano, kwa sababu mtu mkweli amekwambia wewe kuhusu jambo hilo au hoja ya kisomi imeongozea kwenye jambo hilo, hautakiwi kuhusu ufahamu wako wa vitu vya kutamanisha ukutie shaka.

3. Malipo Yake ni mengi mno. Katika sehemu kadhaa, Qur`ani inasema:

وَنِعْمَ أَجْرُ الْعَامِلِينَ

“..... na ni ujira mwema mno wa watendao”

(3:136; 29:58; 39:74)

Aya kadhaa ndani ya Qur`ani zinataja malipo ya Mwenyezi Mungu kama *karim*, maana yake ni ‘ukarimu’ au ‘heshima’:

إِنَّمَا تُنذرُ مَنِ اتَّبَعَ الذِّكْرَ وَخَسِيَ الرَّحْمَنَ بِالْغَيْبِ فَبَشِّرْهُ
بِمَغْفِرَةٍ وَأَجْرٍ كَرِيمٍ

“Hakika unamwonya yule tu anayefuata ukumbusho na akamcha Mwingi wa rehema kwa ghaibu. Basi mbashirie maghufira na ujira wa heshima”. [Surah Yasin, 36:11] ⁴²

4. Malipo Yake ni `adhiim, au ‘makubwa’:

الَّذِينَ اسْتَجَابُوا لِلَّهِ وَالرَّسُولِ مِنْ بَعْدِ مَا أَصَابَهُمُ الْقَرْحُ^{٤٣}
الَّذِينَ أَحْسَنُوا مِنْهُمْ وَاتَّقُوا أَجْرًا عَظِيمًا

“Wale waliomwitikia Mwenyezi Mungu na Mtume baada ya majeraha yaliyowapata; kwa waliofanya wema na takua wana ujira mkubwa. [Surah al-Imrani, 3:172]⁴³

⁴² Angalia pia aya 33:44; 57:11; 57:18.

⁴³ Pia angalia aya zifuatazo: 3:179; 4:40, 67, 74, 95, 114, 146 &162; 5:9 &28; 9:22; 33:29&35; 48:10 &29; 49:3; 64:15.

5. Thawabu Zake pia ni *kabir*, au kubwa/kubwa sana':

إِلَّا الَّذِينَ صَبَرُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ أُولَئِكَ لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَأَجْرٌ كَبِيرٌ

"Isipokuwa wale waliosubiri na wakatenda mema, hao watapata msamaha na ujira mkubwa" [Surah Hud, 11:11]⁴⁴

6. Ujira Wake ni *hasan* au 'mzuri':

قَيِّمًا لِيُنْذَرَ بِأَسَا شَدِيدًا مِنْ لَدُنْهُ وَيُبَشِّرَ الْمُؤْمِنِينَ الَّذِينَ يَعْمَلُونَ الصَّالِحَاتِ أَنَّ لَهُمْ أَجْرًا حَسَنًا مَا كِتَبْنَا فِيهِ أَبَدًا

"Kimenyooka ili kitoe onyo ya adhabu kali kutoka Kwake na kiwabashirie waumini watendao mema kwamba watapata ujira mzuri. Wakae humo milele." [Surah al-Kahf, 18:2-3]⁴⁵

7. Ujira Wake ni wa kustahamilika na wa kudumu milele:

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَهُمْ أَجْرٌ غَيْرُ مَمْنُونٍ

"Hakika wale ambao wameamini na wakatenda mema wa-takuwa na ujira usio na masimango." [Surah Fussilat, 41:8]⁴⁶

⁴⁴ Pia angalia aya zifuatazo: 17:9; 35:7; 57:7; 67:12.

⁴⁵ Pia angalia aya 48:16.

⁴⁶ Pia angalia aya 68:3; 84:25; 95:6.

8. Ujira Wake uko tayari na umeandaliwa:

تَحِيَّتُهُمْ يَوْمَ يُلْقَوْنَهُ سَلَامٌ وَأَعْدَّ لَهُمْ أَجْرًا كَرِيمًا

**“Maamkuzi yao siku ya kukutana Naye yatakuwa ni Salaam.
Na amewaandalia malipo yenyenye heshima.”**

[Surah al-Ahzab, 33:44]

Hii ni sawa na wazazi wanaomuahidi mtoto wao kumpa baisedeli kama zawadi ya kufaulu mtihani vizuri; hadi hapo anapofaulu na kweli wazazi wanamnunulia baisedeli hiyo, ana wasiwasi kama kweli wazazi wake wataheshimu ahadi yao au kama wanazo fedha za kutosha. Lakini njia nyingine ya kuondosha wasi wasi huo ni kununua baisedeli kabla kabisa, na kuiweka ndani ya nyumba kumpa moyo mtoto kujifunza sawasawa ili apate maksi za juu. Vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu huandaa ujira wetu kabla ya muda, na unatungojea sisi.

وَسَارُوا إِلَى مَغْفِرَةٍ مِنْ رَبِّكُمْ وَجَنَّةٍ عَرْضُهَا السَّمَاوَاتُ
وَالْأَرْضُ أَعْدَتْ لِلْمُتَّقِينَ

**“Na harakisheni kuomba maghufira kwa Mola Wenu na
pepo ambayo upana wake ni mbingu na ardhi imeandaliwa
wenye takua.” [Surah al-Imrani, 3:133] – Tazama pia Sura ya 57:21**

Pepo ipo tayari na imekwishaumbwa pamoja na kwamba hajjawekwa mahali pake rasmi. Hilo ni bado hadi Siku ya Hukumu kwamba malipo hayo yatakuwa ya kudumu. Kwa hiyo, Pepo ipo na thawabu za watu wema zipo.

Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu watu kwa ajili ya nia zao njema na hawaadhibu kwa nia zao mbaya:

Allah hutoa thawabu kwa ajili ya nia njema, ingawa hatoi adhabu kwa ajili ya nia mbaya. Pamoja na kwamba mtu anayenuia kumkosea Mwenyezi Mungu, bado anastahili kupewa aina fulani ya adhabu, Mwenyezi Mungu hatamuadhibu al-imuradi mtu huyo hajatenda vitendo vya haramu. Hii ni kawnuni ya jumla, ingawa panaweza kuwepo na mambo ya kipekee.

Kuhusu nia njema, tuseme unataka kutengeneza njia ya kumsaidia masikini kwa kumpa fedha au chakula; unapofika tu nyumbani kwa mtu huyo unakuta amekwishapewa riziki na asingekubali kupokea msaada wako. Pamoja na kwamba unaondoka bila kutoa chochote, lakini kwa sababu ya nia yako kuwa njema, Mwenyezi Mungu anakulipa thawabu.

Au unataka kwenda msikitini kwa ajili ya swala ya jamaa yenye thawabu nyingi na wakati unapofika hapo msikitini, Imam hayupo. Hapo tena, Mwenyezi Mungu atakulipa thawabu kwa sababu ya nia yako. Hali inakuwa vivyo hivyo kwa mtu anayetamani sana kwenda kuhiji lakini hana uwezo wa kifedha. Kwa sababu ya nia yako njema, Mwenyezi Mungu atakulipa thawabu.

Kuwa na nia njema kabla ya kitendo chochote ni muhimu sana kwa maendeleo ya kiroho. Watu wanapaswa kujitahidi kuwa na nia njema kubwa kama vile kwenda maili moja zaidi kuwasaidia wengine kwa kuwa na huruma na kuwafikiria wao. Kuweka nia kama hizo pamoja na kufanya kadiri uwezavyo kukamilisha kazi hiyo kutakuchumia thawabu kwa ajili ya palipobakia.

Mwenyezi Mungu huzidisha thawabu kwa ajili ya matendo mema; adhabu kwa ajili ya matendo mabaya hazizidishwi.

Kama mtu atapewa adhabu kwa ajili ya kutenda dhambi, adhabu yake itakuwa sawa na dhambi aliyofanya. Kuna adhabu moja tu kwa kila kitendo cha haramu. Kitendo kimoja cha haramu husababisha adhabu moja, na vitendo viwili vya haramu husababisha adhabu mbili. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu hutoa thawabu kwa kadiri ya mara kumi zaidi kwa ajili ya kila tendo jema:

مَنْ جَاءَ بِالْحَسَنَةِ فَلَهُ عَشْرُ أَمْثَالِهَاٖ وَمَنْ جَاءَ بِالسَّيِّئَةِ فَلَا
يُجْزَى إِلَّا مِثْلَهَا وَهُمْ لَا يُظْلَمُونَ

“Mwenye kufanya vizuri atalipwa mfano wake mara kumi. Na mwenye kufanya vibaya hatalipwa ila sawa na hivyo tu. Nao hawatadhulumiwa.” [Surah al-Anam, 6:160]

Na utoaji Wake wa thawabu hauishii hapo, kwa kuwa kuzidisha thawabu mara kumi ni ongezeko dogo:

مَثْلُ الَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ كَمَثْلٍ حَبَّةٌ أَنْبَتَتْ
سَبْعَ سَنَابِلَ فِي كُلِّ سُبْلَةٍ مِائَةُ حَبَّةٍ وَاللَّهُ يُضَاعِفُ لِمَنْ
يَشَاءُ وَاللَّهُ وَاسِعٌ عَلِيمٌ

“Mfano wa wale wanaotoa mali zao katika njia ya Mwenyezi Mungu ni kama mfano wa punje moja iliyochipuza mashuke saba; katika kila shuke pana punje mia. Na Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa, Mjuzi.”

[Surah al-Baqarah, 2:261]

Kwa hiyo, tendo moja jema ni sawa na mbegu moja ambayo itakuwa mia saba, na bado Mwenyezi Mungu anaweza kuongeza hizi, kwani anasema: "Mwenyezi Mungu humzidishia amtakaye." Inawezekana hii inamaanisha kwamba mia saba inaweza kuwa alfu moja na mia nne, na halafu alfu mbili na mia moja.

Hadithi iliyomo kwenye *Mafatih al-Jinan* inasimulia kwamba kama mtu akiomba msamaha mara sabini kila siku ya mwezi wa Sha`ban, ni sawa na kuomba msamaha mara 70,000 katika miezi mingine. Zaidi ya hayo, Mwenyezi Mungu huishughulikia sadaka iliyotolewa katika mwezi huu kama mtoto wa ngamia; Yeye huwajibika kwa makuzi yake na humtunza. Mnamo Siku ya Hukumu, watu wataona sadaka zao zinakua sawa na ukubwa wa Mlima Uhud. Kwa hiyo, kutumia shilingi moja tu haikuchumii shilingi moja kutoka kwa Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu huwekeza katika shilingi yako moja kwa kiwango kikubwa, labda itakuchumia shilingi milioni moja mnamo Siku ya Hukumu. Na bado dhambi yetu moja inatuchumia adhabu ya kiasi cha dhambi hiyo.

Reheme ya Mwenyezi Mungu inaonekana zaidi hasa katika Mwezi wa Ramadhani. Kusoma aya moja ya Qur`ani ni sawa na kusoma Qur`ani yote. Kule kuwa muumini tu katika mwezi huu inatosha kukupa wewe thawabu. Kulala kwa ko mnamo Mwezi huu wa Ramadhani kunalipwa thawabu kama kitendo cha ibada - (نومكم فيه عبادة)⁴⁷ na kupumua kwako kunalipwa kama kitendo cha kumtukuza Mwenyezi Mungu - (أنفاسكم فيه تسبیح)⁴⁸

Inapokuja kwenye Usiku wa Kipimo, au 'Laylat al-Qadr', namna Mwenyezi Mungu anavyolipa huwezi kuamini! Ndani

⁴⁷ Wasa` ilus-Shia, Juz. 10, uk. 313

⁴⁸ Wasa` ilus-Shia, Juz. 10, uk. 313

ya hadithi nzuri kutoka kwa Imam Baqir (a.s.) kuhusu '*Laylat al-Qadr*', mtu mmoja alimuomba Imam (a.s.) amueleze kuhusu dhana ya usiku huu kuwa bora kuliko miezi elfu moja (97:3). Imam (a.s.) alijibu:

العمل الصالح فيها من الصلاة و الزكاة و أنواع الخير خير
 من العمل في ألف شهر ليس فيها ليلة القدر ، ولو لا ما
 يضاعف الله تبارك و تعالى للمؤمنين ما بلغوا و لكن الله
 يضاعف لهم الحسنات

Kitendo chochote chema unachofanya ndani ya *Laylat al-Qadr*, ama iwe swala, zaka, au matendo mengine mema, ni bora kuliko kufanya kitendo kama hicho katika kipindi cha miezi elfu moja ambamo hamtakuwa na *Laylat al-Qadr*. Kama isingekuwa hivyo kwamba Mwenyezi Mungu, Mwenye rehema na Aliye Juu, anazidisha kwa ajili ya waumini, kamwe wasingefikia kiwango cha juu. Lakini Yeye huyazidisha matendo yao mema kwa ajili yao.⁴⁹

Kuswali swala ya rakaa mbili ndani ya '*Laylat al-Qadr*' kuna thawabu zaidi ya kuswali swala ya rakaa mbili kila siku usiku kwa miezi elfu moja. Kutoa sadaka ya shilingi moja ndani ya '*Laylat al-Qadr*' ni bora kuliko kutoa sadaka ya shilingi moja kila siku usiku kwa miezi elfu moja. Baadaye, Imam Baqir (a.s.) alisema, "Kama isingekuwa kwamba Mwenyezi Mungu, Mwenye rehema na aliyeko Juu, huwazidishia waumini, kamwe wasingefikia ukamilifu wao au kuiona pepo)."⁵⁰

⁴⁹ *Al-Kafi*, Juz. 7. uk. 626, *Al-Mizan*, Juz. 20, uk. 334

⁵⁰ *Al-Kafi*, Juz. 7. uk. 626, *Al-Mizan*, Juz. 20, uk. 334

Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu, ambaye anatambua uhitaji wetu na jinsi gani maandalizi yetu yalivyo madogo kwa ajili ya safari yetu ya milele, hutupatia fursa nyingi kubwa ili tuweze kufanya vema zaidi, na mara inapofanyika, Yeye hukuzza matokeo. Kwa nyongeza ya njia ya jumla ya kuzidisha thawabu Zake kwa ajili ya matendo mema, ametufahamisha sisi muda, mahali, na mazingira ambayo yanafaa hasa. Katika kila siku, wiki, na mwaka, zipo nyakati ambamo ndani mwao fursa ya swala yako kukubaliwa ni zaidi, kupata msamaha ni rahisi zaidi, na malipo Yake ni ya ukarimu zaidi. Kutaja mifano michache ya nyakati, mahali na mazingira yenyе baraka kama hizo, mtu anaweza kurejelea kwenye wakati wa mchana (*wakati wa zawaal*: kupinduka kwa jua mchana), theluthi ya mwisho ya usiku (kabla ya mawio), usiku wa Ijumaa (Jumu'a), saa za mwanzo na za mwisho za siku ya Ijumaa, Siku ya Arafah, katikati ya Sha`ban, *Laylat Qadr*, misikitini, sehemu takatifu kama vile *Masjid al-Haraam* uliopo Makka na *Masjid al-Nabi* uliopo Madina, na baada ya swala za faradhi, hususani swala za jamaa.

Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu wale wanaofanya matendo ambayo yamependekezwa ndani ya baadhi ya hadithi, hata kama hadithi hizo haziko sahihi hasa.

Kanuni ya maafikiano kuhusu vyanzo ambavyo huonyeshi matendo yaliyopendekezwa (*Qa`idah al-Tasaamuh Fi Adillah al-Sunan*) katika elimu ya Kanuni za Sheria (*usul al-fiqh*) inamaanisha kwamba kama mtu akipokea hadithi ambamo malipo ya thawabu yameahidiwa kwa tendo fulani lililotajwa na akatekeleza kufuatana na hadithi hiyo, atapewa malipo kama hayo, hata kama hadithi hiyo si thabit. Msingi wa kanuni hii ni kundi la hadithi kutoka kwa Mtume

Muhammad (s.a.w.w.) na Maimam (a.s.) mojawapo inasomeka hivi:

**من بلغه شيء من التواب على (شيء من الخير) فعمله
كان له أخر ذلك (و إن كان رسول الله (ص) لم يقله)**

Yeyote atakayepokea hadithi kuhusu thawabu kwa ajili ya kutekeleza tendo jema na anafanya tendo hilo kweli ili aweze kupata thawabu hizo, atapewa thawabu hizo hata kama hadithi hiyo haikusemwa na Mtume wa Mwenyezi Mungu.⁵¹

Hivyo kama ukisikia au ukisoma hadithi ambayo, kwa mfano, inapendekeza du'a fulani ndani ya *Laylat al-Qadr* kwa sababu ina malipo maalumu na mtu kwa kweli akaisoma du'a hiyo, mtu huyo atalipwa thawabu hizo hata kama hadithi hiyo ilikosewa au ilighushiwa. Kama mambo yalivyo, riwaya hiyo na tendo lililopendekezwa lazima vyenyewe viwe na mantiki na vikubaliane na Qur`ani, Sunnah na akili. ⁵²

Ukarimu wa Mwenyezi Mungu upo dhahiri kabisa. Unaposikia kuhusu tendo zuri la ibada ambalo unadhani lina mantiki na ni lenye kupendeza mbele ya Mwenyezi Mungu na ukalitekeleza, Mwenyezi Mungu atalikubali na atakulipa thawabu kwa ajili ya tendo hilo hata kama halikuwa kiuhalisia ni lile Yeye alilokuagiza wewe ufanye kupitia kwa Mtume Wake. Mwenyezi Mungu analikubali hili kwa sababu umelifanya kwa

⁵¹ *Wasa'il al-Shi'ah*, Juz. 1, uk. 80 & Juz. 30, uk. 246. Ipo sura kuhusu suala hili ndani ya Juz. 1. uk. 882 ambamo mna hadithi kumi.

⁵² Bila shaka, kila mtu anatakiwa kuwa mwangalifu, na kutokukubali kila kitu, kwa sababu yapo mambo mengi ya kishirikina na maoni ambayo hayaleti maana yoyote, ambayo yapo mbali dhahiri kabisa na ukweli na mtu yeyote asizifanyie kazi riwaya kama hizo.

ajili Yake. Ni sawa na mtu ambaye anadhani wewe una kiu am-bapo kwa kweli huna kiu na matokeo yake anakuletea maji; pamoja na kwamba hukuhitaji maji hayo, bado tu utamshukuru. Bila shaka, inawezekana usimchukulie kama utakavyomchukulia yule mtu aliyekulatea maji wakati ukiwa unayahitaji hasa. Hata hivyo, Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu kwa mlingano sawa. Mwenyezi Mungu anamaanisha kutuambia sisi kwamba kwa kuwa nia yetu ilikuwa kufanya jambo jema, Yeye atatupatia thawabu kama matokeo ya huruma na ukarimu Wake.

Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu wacha-Mungu kufuatana na utendaji wao mzuri sana:

Kitengo kingine cha mfumo karimu wa upaji wa Mwenyezi Mungu ni kwamba huchukua tendo zuri zaidi kwa ajili ya hao wacha-Mungu, yaani, wale waaminio na kufanya vitendo vya uadilifu, kama kipimo ambacho kwacho hulipia thawabu mambo mengine yote wa aina hiyo ya kitendo ambacho wamekifanya katika maisha yao:

مَنْ عَمِلَ صَالِحًا مِنْ ذَكَرٍ أَوْ اُنْثَى وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَلَنْحِبِّنَّهُ حَيَاةً طَيِّبَةً وَلَنَجْزِيَنَّهُمْ أَجْرَهُمْ بِأَحْسَنِ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ

“Mwenye kutenda mema, mwanamume au mwanamke, naye akawa ni muumini, tutamhuisha maisha mema; na tutawapa ujira wao kwa mazuri zaidi waliyokuwa wakiyafanya.” [Surah al-Nahl, 16:97]

Kufuatana na aya hii, Mwenyezi Mungu huwapa wale wenye kuamini na matendo ya uadilifu maisha ya furaha (*al-hayaat al-tayyibah*) na watalipwa thawabu kulingana na

uzuri wa matendo yao. Kama umekwishafikia kiwango hiki cha ucha-Mungu, Mwenyezi Mungu huangalia matendo yao yote kama vile maelfu ya swala ambazo watakuwa wameziswali wakati wa uhai wao, huchagua iliyo bora zaidi, na halafu huzipatia thawabu swala zote ipasavyo. Inawezekana pawepo na swala moja tu mahususi ambayo uliizingatia, msafi, na iliyejiunganisha moja kwa moja kwa Mwenyezi Mungu, na bado anaifanya hiyo kuwa kigezo cha kuzipatia swala zako zote thawabu. Kama tendo moja la sadaka lilikuwa bora zaidi, Yeye atayalipa matendo yako yote ya sadaka sawa sawa.

Hili linapaswa pia kututia moyo sisi tuwe waangalifu sana kuhusu vitendo vyetu. Baadhi ya watu wengine wanaweza kuchukua fursa ya hili na kufikiria tendo lao zuri sana – kama vile swala moja nzuri sana ya zamani, kuwa inatosha kwa Mwenyezi Mungu kulipa thawabu kwa swala zao zote za siku za usoni hivyo; watakuwa hawana haja ya kujali ubora ya swala zao tena. Hata hivyo, huu ni mtazamo mbaya na wa kimakosa. Kwa kweli kama mtu anafikiri kwa namna hii, hii inadhihirisha kwamba yeye si mmoja kati ya wacha-Mungu ambao wamepewa maisha ya furaha (*al-hayat al-tayyibah*). Wale wanaostahiki hili hujaribu wakati wote kujiboresha zaidi. Huwa hawafaridhiki kabisa na matendo yao ya ibada, na hata kama wakihisi kwamba tendo mojawapo lilikuwa zuri, hujaribu kuboresha zaidi katika tendo linalofuata. Wakati wote hupandisha viwango vyao, hasa kwa sababu wanajua kwamba kuboresha kitendo kinachofuata kunaweza kuboresha matendo yao yote ya aina hiyo. Kwa mfano, Mwenyezi Mungu anatazama ni kiwango gani ambacho mtu anakuwa hadhiri na mwangalifu katika kuboresha swala zake, na kwa kila utendaji ulioboreshwaa,

Yeye anauchukua huo kama kipimo ambacho kwacho Yeye atalipia thawabu swala zake zote.

Mwenyezi Mungu huwalipa wenyewe subira bila kipimo:

Kwa mujibu wa Qur`ani, wapo watu ambao Mwenyezi Mungu huwalipa thawabu bila kipimo, ambalo hilo kwa dhahiri ni zaidi maradufu kuliko kutoa malipo yaliyozidishwa:

قُلْ يَا عِبَادَ الَّذِينَ آمَنُوا اتَّقُوا رَبَّكُمْ لِلَّذِينَ أَحْسَنُوا فِي هُذِهِ
الْدُّنْيَا حَسَنَةٌ وَأَرْضُ اللَّهِ وَاسِعَةٌ إِنَّمَا يُوَفَّى الصَّابِرُونَ
أَجْرَهُمْ بِغَيْرِ حِسَابٍ

“Sema: Enyi waja wangu ambao mmeamini! Mcheni Mola Wenu. Wale ambao wamefanya wema katika dunia hii wata-pata wema. Na ardhi ya Mwenyezi Mungu ni pana. Hakika si mengineyo, wenyewe subira watapewa ujira wao bila ya hisabu.” [Surah Azzumar, 39:10] ⁵³

⁵³ Hii ni kuhusu malipo. Pia zipo aya ambazo zinaahidi masurufu au riziki bila ukomo kwa watu fulani. Qur`ani inasema:

فِي بَيْتٍ أَنَّ اللَّهَ أَنْ تُرْفَعَ وَتُذَكَّرَ فِيهَا أَسْمَهُ يُسَبِّحُ لَهُ فِيهَا بِالشَّمْرِ وَالْأَصْنَالِ رِجَالٌ لَا تُلَهِّيهِمْ تَجَارَةٌ وَلَا بَيْتٌ عَنْ ذِكْرِ اللَّهِ وَإِقَامِ الصَّلَاةِ وَإِيتَاءِ الزَّكَاةِ يَخْافُونَ
يُوْمًا يَنْقَلِبُ فِيهِ الْقُلُوبُ وَالْأَيْمَانُ لِيَجْزِيَهُمُ اللَّهُ أَحْسَنُ مَا عَمِلُوا وَيُزَرِّعُ مِنْ فَضْلِهِ وَاللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ

“Katika nyumba ambazo Mwenyezi Mungu ameruhusu ziinuliwe na kutajwa humo jina lake, wanamtakasa humo asubuhi na jioni. Watu amabo biashara wala kuuza hakuwashughulishi na kudhukuru Mwenyezi Mungu, na kuisimamisha swala na kutoa Zaka. Wanaihofu siku ambayo nyoyo na macho yatageuka. Ili Mwenyezi Mungu awalipe mazuri ya yale waliiyoyatenda, na wazidishie katika fadhila Zake. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila ya hisabu.” [Surah an-Nur, 24:36-38]

رُبُّ الْأَنْبِيَاءِ كَفَرُوا بِالْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَيُسْخَرُونَ مِنَ الْأَنْبِيَاءِ أَمْنُوا وَالَّذِينَ أَنْفَقُوا قُرْبَةً ثُمَّ يُؤْمِنُونَ اللَّهُ يَرْزُقُ مَنْ يَشَاءُ بِغَيْرِ حِسَابٍ

Hapa malipo ya thawabu yaliyoahidiwa sio ya mara kumi zaidi, au mara 1000 zaidi, au mara milioni moja zaidi. Ni bila kipimo.

Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe:

Kwa nyongeza ya malipo Yake ya ukarimu, Mwenyezi Mungu hushughulikia dhambi au watu kwa huruma na upole. Yeye huwahakikishia wenyewe dhambi kwamba kama wakijutia dhambi zao na kutubu kwa uaminifu, Yeye atawasamehe. Watu wanapokwenda kwenye uwanda wa `Arafat mnamo siku ya 'Arafah, dhambi zao zote zitasamehewa, na wakati wanapoondoka `Arafah kwenda Mash`ar al-Haram ni lazima wasiwe na shaka yoyote kuhusu dhambi zao kusamehewa. Imesimuliwa kwamba Mwenyezi Mungu huwaacha huru watu milioni moja kutoka kwenye moto wa Jahanamu kila siku mnamo Mwezi wa Ramadhani wakati wa kufuturu. Katika usiku na mchana wa Ijumaa, Mwenyezi Mungu huwaachia huru watu milioni moja katika kipindi cha kila saa moja. Kwenye usiku na mchana mwishoni mwa mwezi,

“Wamepambiwa makafiri maisha ya duniani, na wanawafanya maskharra wale walioamini. Na wale wenye takua watakuwa juu yao Siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu humruzuku amtakaye bila hesabu.”

[Surah al-Baqarah, 2:212]

Aya hizo hapo juu, zinaonyesha kwamba Mwenyezi Mungu humruzuku yeyote amtakaye bila kipimo. Ingawa aya hizi haziwatambulishi wazi wale ambao Mwenyezi Mungu anataka kuwaruzuku bila kipimo, aya ifuatayo inadokeza kwamba hao ni waumini ambao hufanya matendo mema:

مَنْ عَيْلَ سَيِّئَةً فَلَا يُجْزَى إِلَّا مِثْلَهَا وَمَنْ عَيْلَ صَالِحًا مِنْ ذَكْرٍ أَوْ لَتْهٍ وَمَنْ مُؤْمِنٌ فَأُولَئِكَ يَنْخُلُونَ الْجَنَّةَ يُبَرَّزُونَ فِيهَا بِغَيْرِ حِسَابٍ

“Mwenye kutenda uovu hatalipwa ila sawa na huo, na mwenye kutenda wema, akiwa mwanamume au mwanamke, naye ni Muumini, basi hao wa taingia Peponi, waruzukiwe humo bila ya hesabu.” [Surah al-Mu`min, 40:40]

Mwenyezi Mungu huwaacha huru watu sawa na chochote kile Yeye alichotoa katika kipindi cha mwezi huo.

Aina mbali mbali za msamaha.

Katika kutafakari juu ya aya za Qur`ani kuhusu msamaha wa dhambi unaotolewa na Mwenyezi Mungu, msamaha wa Ki-Mungu unaweza kugawanywa katika aina nne:

- (a) **Msamaha rahisi:- aya ambazo zinarejelea kwa kawaida juu ya msamaha wa Mwenyezi Mungu kama zifuatazo:**

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرِكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ ذَلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ
وَمَنْ يُشْرِكُ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَ إِنْمَا عَظِيمًا

“Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi kufanyiwa mshirika, lakini husamehe yasiyokuwa hayo kwa amtakaye. Na mwenye kumshirikisha Mwenyezi Mungu hakika amezusha dhambi kubwa. [Surah an-Nisaa, 4:48 & 4:116].

وَمَنْ يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ اللَّهَ يَجِدُ اللَّهَ
غَفُورًا رَّحِيمًا

“Na mwenye kutenda uovu au akadhulumu nafsi yake, kisha akaomba maghfira kwa Mwenyezi Mungu atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa maghfira Mwenye kurehemu.” [Surah an-Nisaa, 4:110]

- (b) Kufunika dhambi:- Wakati mwingine dhambi haisame-hewi tu, lakini pia inafunikwa na Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo, mnamo Siku ya Hukumu, hapana mtu atakayeweza kuona dhambi ambayo mtu ameifanywa kwa sababu itakuwa imefunikwa. Hii inapendeza kwa watu wanaosoma rekodi yako ya matendo na kugundua dhambi zako, hata kama zimesamehewa. Kwa mfano, Qur`ani inasema:

إِنْ تُبْدِوا الصَّدَقَاتِ فَنِعْمًا هِيَ^١ وَإِنْ تُخْفُوهَا وَتُؤْتُوهَا
الْفُقَرَاءَ فَهُوَ خَيْرٌ لَكُمْ^٢ وَيُكَفِّرُ عَنْكُمْ مِنْ سَيِّئَاتِكُمْ^٣ وَاللَّهُ بِمَا
تَعْمَلُونَ خَيْرٌ

“Mkizidhihirisha sadaka ni vizuri; Na kama mkitoa kwa siri na kuwapa mafukara, basi hivyo ni bora zaidi kwenu, na yatawaondokea baadhi ya maovu yenu; na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa mnayoyatenda.” [Surah al-Baqarah, 2:271]⁵⁴

- (c) Kufutwa kwa dhambi: Kwa mujibu wa vyanzo vyta Kiislamu, Mwenyezi Mungu anaweza kufuta dhambi na matendo maovu ya watu fulani. Hii inaonekana kama aina ya msamaha ambayo ni zaidi ya msamaha rahisi au hata msamaha wa kufunika na kuficha dhambi, kwa sababu hapa dhambi zinafutwa kabisa bila kubaki dalili zozote. Hii ni kama kosa katika maandishi ya mtu ambayo yanepigwiwa na kisha yakasamehewa na mwalimu au yangesamehewa na kusahihishwa na mwalimu. Faida ya melezo yaliyofuata ni kwamba kosa lililosahisishwa lisingejulikana kwa wengine na

⁵⁴ Pia angalia 4:31; 8:28; 29:7; 39:35; 64:9; 65:5.

yule ambaye amesamehewa hatakumbushwa kuhusu kosa lake. Hata hivyo, upo wasi wasi kwamba kuna uwezekano wa kuondolewa kufunikwa huku kwa dhambi hizo na dhambi zilizofunikwa zinaweza zikaooneshwa. Hata pale ambapo kuna kifuniko, kama pale ambapo wino wa masahihisho umepakwa juu ya makosa, inaonyesha kwamba palikuwepo na tatizo kabla yake. Kwa hiyo muundo wa msamaha wenyewe nguvu zaidi ni kufuta kabisa kosa. Kwa mfano, Imam Sadiq (a.s.) ananukuliwa akisema:

للجمعة حقاً واجباً فلماك أن تضيع أو تقصر في شيء من
 عبادة الله تعالى والتقرب إليه بالعمل الصالح وترك المحارم
 كلها فان الله يضاعف فيه الحسنات ويحو في السينيات
 ويرفع فيه الدرجات وليلته مثل يومه قال فان استطعت أن
 تحببها بالدعاء والصلوة فافعل فان الله تعالى يضاعف فيها
 الحسنات ويمحو السيئات وإن الله واسع كريم

“Siku ya Ijumaa ina haki ya wajibu. Tahadhari usiikose au kufanya kidogo katika kumuabudu Mwenyezi Mungu na kuwa karibu na Yeye kwa kufanya matendo mema na kujizia kutenda dhambi zote. Kwa kweli, Mwenyezi Mungu huzidisha matendo mema na hufuta dhambi katika siku hii, na madaraja yatapandishwa. Usiku wake ni kama mchana. Kama unaweza kuuhuisha kwa kusoma dua na kuswali, fanya hivyo, kwa sababu Mwenyezi Mungu huzidisha ndani yake matendo mema na hufuta matendo mabaya. Kwa kwe-li Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa rehema na Mkarimu.”⁵⁵

⁵⁵ Al-Tawhid, uk.167; Al-Da`awat, uk. 37.

Pia tunasoma kwenye hadithi kutoka kwa Imam Baqir (a.s.):

التائب من الذنب كمن لا ذنب له

“Mtu anayetubu kwa uaminifu ni sawa na mtu ambaye kamwe hajafanya dhambi.”⁵⁶

- (d) Kubadilisha dhambi na kuwa matendo mema: Kulingana na Qur`ani na hadithi, sio tu kwamba Mwenyezi Mungu husamehe dhambi za wale wanaotubu, lakini pia anaweza kubadili matendo yao maovu na kuwa mema:

إِلَّا مَنْ تَابَ وَآمَنَ وَعَمِلَ عَمَلاً صَالِحًا فَأُولَئِكَ يُبَدِّلُ اللَّهُ سَيِّئَاتِهِمْ حَسَنَاتٍ ۝ وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا

“Isipokuwa atakayetubia na kutenda mema basi hao Mwenyezi Mungu atayabadilisha maovu yao yawe mema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusamehe, Mwenye kurehemu.” [Surah al-Furqan, 25:70]

Hii ni zaidi sana kuliko kusamehe dhambi na kuzifuta kabisa. Katika njia hii, kwa kweli Mwenyezi Mungu hasa anab-adilisha dhambi zao na kuwa matendo mema na anawalipa mazuri kwa ajili ya hizi dhambi. Si tu kwamba hawataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao, lakini wataweza kufidia angalau sehemu ya makosa yao. Hakika kila mtu ambaye hachumi mema katika maisha yake yuko kwenye hasara, hata kama

⁵⁶ Al-Kafi, Juz. 2, uk. 435. Bihar Al-Anwar, Juz, 6, uk. 21/41 & Juz. 90. Uk. 281.

hatafanya jambo lolote uovu. Hii ni sawa na mwanafunzi ambaye anarudisha karatasi yake ya majibu ya mtihani ikiwa haina majibu. Cha kuvutia zaidi, inaweza kueleweka kutoka kwenye riwaya ya Imam Sajjad (a.s.) kwamba matendo mema ambayo hubadilishwa na matendo maovu bado yanaweza kuzidishwa kama matendo mema ya mcha-Mungu. Imam Sajjad (a.s.) anamwambia Mwenyezi Mungu katika mojawapo ya dua zake:

يَا مَبْدُلَ السَّيِّئَاتِ بِأَضْعافِهَا مِنَ الْحَسَنَاتِ

“Ewe Unayebadilisha matendo maovu na kuwa matendo mema mengi sana!”⁵⁷

Si tu kwamba Yeye hubadilisha matendo mema na kuwa matendo maovu, lakini hubadilisha matendo maovu na kuwa matendo mema mengi sana. Kwa mfano, mtu ambaye ametumia shilingi yake kwa uovu baada ya kutubia na kushughulikiwa namna hii na Mwenyezi Mungu, angepata malipo kwa ajili ya kutumia shilingi kadhaa kwa malengo mema ndani ya rekodi ya matendo yake mnamo Siku ya Hukumu.

Kutafakari juu ya (a) aina ya watu ambao watasamehewa, (b) aina ya watu ambao watakuwa dhambi zao zimefunikwa, (c) wale ambao wana dhambi ambazo zimefutwa kabisa (d) wale ambao wangeona dhambi zao zinabadilishwa na kuwa matendo mema mengi sana, inaweza kumaanisha kwamba kama mtu ambaye amefanya dhambi na akajuta kwa uaminifu hasa na akaamua asirudie kufanya dhambi hizo tena, dhambi zake zitasamehewa. Kwa namna Mwenyezi

⁵⁷ Al-Sahifah al-Sajjadiyyah, Dua ya 24.

Mungu alivyo, hakuna shaka kuhusu hili. Ufahamu wa mwenye kutubu utaongezeka kutohana na nguvu ya majuto yake. Hujihisi aibu kwa sababu ingawa dhambi zake zimesamehewa, yeye anaendelea kutafakari juu ya hali yake mnamo Siku ya Hukumu, pale ambapo atasimama mbele ya Mwenyezi Mungu na mashahidi wakati anasomewa makosa yake. Pamoja na kwamba hatimaye yatasamehewa makosa hayo, atakuwa na wasi wasi kuhusu heshima yake na atajisemea, "Inafedhehesha na ni aibu juu yangu kwamba kabla ya msamaha wa Mwenyezi Mungu haujatangazwa, dhambi zangu zitasomwa mbele ya Mtume, Maimam, na ummah kwa ujimla." Kwa watu kama hao, Mwenyezi Mungu huficha au hata kufuta kabisa matendo yao mabaya.

Jinsi uelewa wake utakavyoongezeka akijua kwamba Mwenyezi Mungu amemsamehe na ameahidi kulinda heshima yake, vipi kuhusu nyakati na fursa alizopoteza? Angeweza kuchukua masurufu mengi wakati wa miaka hiyo kwa ajili ya safari yake ya milele. Kwa watu kama hao, Mwenyezi Mungu hubadilisha matendo yao maovu na kuwa matendo mema ili kuwazuia wasiwe na wasi sana kuhusu masurufu yao. Lakini bado ipo nafasi ya kukuza uelewa wao na kufikiri kwamba inavutia na kutia moyo kwamba matendo yao maovu yamebadilishwa na kuwa matendo mema, pamoja na kwamba bado tunaendelea kupoteza kwa sababu wale wenye matendo mema wamezidishiwa kiasi cha angalau mara kumi, lakini matendo yetu mema mapya ambayo tumepewa hayazidishwi. Inawezekana ni kwa watu kama hao ambao kwamba Mwenyezi Mungu hubadilisha matendo yao maovu na kuwa matendo mema yaliyozidishwa.

Hivyo, kutegemeana na kuongezeka kwa uelewa wako, Mwenyezi Mungu anakulipa zaidi. Bila shaka, haya ni maoni ya unyenyekevu ya mwandishi kuhusu uwezekano mmojawapo katika kuelezea njia mbali mbali za msamaha wa mbinguni. Pamoja na kwamba hii inaleta maana, isije ika-chukuliwa kama uthibitisho. Kwa hiyo kutegemeana na uelewa wako na juu ya wasi wasi wako, Mwenyezi Mungu angekusaidia, na hiki ni kipimo kingine cha radhi na ukarimu Wake.

Mwenyezi Mungu hamuadhibu yeyote kwa maovu ya mtu mwingine, lakini anaweza kumsamehe mwenye dhambi kwa tendo zuri la mtu mwingine:

Mwelekeo mwingine wa rehema ya Ki-Mungu ni kwamba wakati mwingine Mwenyezi Mungu humsamehe mtu kwa ajili ya mtu mwingine. Kwa mfano, Qur`ani inasema:

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَاتَّبَعُتْهُمْ ذُرِّيَّتُهُمْ بِإِيمَانِ الْحَقَّنَا بِهِمْ ذُرِّيَّتُهُمْ وَمَا أَنْتَاهُمْ مِنْ عَمَلِهِمْ مِنْ شَيْءٍ كُلُّ امْرٍ إِبْمَانٌ كَسَبَ رَهِينٌ

“Na walioamini na dhuriya zao wakawafuata kwa Imani tutawakutanisha nao dhuriya zao, na wala hatutawapunja kitu katika vitendo vyao. Kila mtu ni rehani wa alichokichuma.” [Surah at-Tur, 52:21]

Kwa wazazi wacha-Mungu ambao wanao watoto ambao ni waumini, pamoja na kwamba si wacha-Mungu sana au hawa-na matendo mema ya kutosha kuwawezesha wao wote kuku-sanyika mbinguni, hata hivyo, Mwenyezi Mungu ni mpole sana hivyo kwamba hutumia kutoka kwenye thawabu za wa-

zazi wacha-Mungu juu ya watoto wao bila ya punguzo lolote kwenye thawabu za wazazi. Si kwamba Mwenyezi Mungu hu-punguza yale matendo kumi mazuri ya muumini na kuwapa matano wazazi na matano kwa mtoto wake kuwanyanya wao. Kwa usahihi zaidi, atamnyanya mtoto bila kupunguza matendo mazuri na thawabu zinazoendana na za wazazi. Akisherehesha juu ya aya hiyo hapo juu, Imam Sadiq (a.s.):

قصرت الأبناء عن عمل الآباء فألحقوا الأبناء بالآباء لتقر
 بذلك أعينهم

“Wakati mwингine matendo ya watoto huwa pungufu ku-liko yale ya baba zao, lakini watoto hao wataruhusiwa ku-ungana nao ili kuwafurahisha wazazi wao.”⁵⁸

Ibn Abbas anasimulia kutoka kwa Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w.w.):

إذا دخل الرجل الجنة سأله عن أبيه وزوجته وولده ، فيقال
 لهم: إنهم لم يبلغوا درجتك و عملك فيقول: رب قد عملت لي
 ولهم، فيؤمر بالإلتحاق بهم.

“Mtu anapoingia Peponi, atauliza kuhusu wazazi wake, mke wake, na watoto. Anaweza akaambiwa kwamba wao ha-wakufikia daraja lako na matendo. Atasema: “Mola Wangu! Chochote kile nilichofanya, ilikuwa ni kwa ajili yangu na kwa ajili yao.” Hapa Mwenyezi Mungu ataamuru waruhus-we kuungana naye.⁵⁹

⁵⁸ Al-Kafi, Juz. 3, uk. 249. Al-Tawhid, uk. 394

⁵⁹ Al-Mizan, Juz. 19, 16, imesimuliwa kutoka Al-Durr al-Manthur na Jalal al-Din Suyut.

Pia Qur`ani inatutaarifu sisi kuhusu malaika kuwasalia waumini:

الَّذِينَ يَحْمِلُونَ الْعَرْشَ وَمَنْ حَوْلَهُ يُسَبِّحُونَ بِحَمْدِ رَبِّهِمْ
 وَيُؤْمِنُونَ بِهِ وَيَسْتَغْفِرُونَ لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا وَسِعْتَ كُلَّ شَيْءٍ
 رَحْمَةً وَعِلْمًا فَاغْفِرْ لِلَّذِينَ تَابُوا وَاتَّبَعُوا سَبِيلَكَ وَقِيمُ عَذَابَ
 الْجَحِيمِ رَبَّنَا وَأَدْخِلْهُمْ جَنَّاتٍ عَدْنَ الَّتِي وَعَذَّثُمْ وَمَنْ صَلَحَ
 مِنْ أَبَائِهِمْ وَأَزْوَاجِهِمْ وَذُرِّيَّاتِهِمْ إِنَّكَ أَنْتَ الْعَزِيزُ الْحَكِيمُ
 وَقِيمُ السَّيِّئَاتِ وَمَنْ تَقِ السَّيِّئَاتِ يَوْمَئِذٍ فَقَدْ رَحِمْتَهُ وَذَلِكَ
 هُوَ الْفَوْزُ الْعَظِيمُ

“Wale wanaobeba Arshi, na wanaoizunguka, wanamsabihi kwa kuhimidi Mola Wao, na wanamwamini na wanawaombea msamaha walioamini. Mola Wetu! Umekienea kila kitu kwa rehema na ujuzi. Basi wasamehe ambao wametubu na wakaifuata Njia Yako, na waepushe na adhabu ya Jahan-nam. Mola Wetu! Na waingize katika Bustani za Milele ulizowaahidi. Na pia waliofanya mema mionganoni mwa wazee wao na wake zao na dhuriya zao. Hakika Wewe ni Mwenye nguvu, Mwenye hekima. Na waepushe na maovu; kwani umwepushaye maovu siku hiyo, hakika umemrehemu; na huko ndiko kufuzu kukubwa.” [Surah al-Mu`min, 40:7-9]

Akisherehesha juu ya aya hizo hapo juu, Allamah Tabataba`i anashikilia kwamba zinarejelea makundi mawili ya waumini: Kundi moja ni lile la waliokamilika (*al-kaamilu-un*) katika imani na mienendo yao; kundi lingine linarejelea kwa baadhi ya ndugu wa kundi la kwanza ambao ni wa chini

kwa daraja, kwa vile imani na matendo yao hayako kamili. Malaika wanamuomba Mwenyezi Mungu kuwapa lile kundi la mwanzo pepo ambayo alikuwa amewaaahidi wao. Pia hu-muomba Yeye kuwaruhusu kundi la pili kuungana na kundi la kwanza ili kuwaokoa kutokana na maovu.⁶⁰

Haielekei kukubalika kufikiri kwamba Mwenyezi Mungu atawasikitisha malaika hawa wakubwa kwa kuwakatalia maombi yao. Kwa kweli, ni Mwenyezi Mungu Mwenyewe ambaye aliwahimiza malaika hao kumuomba Yeye kwa njia hii.

Vivyo hivyo, Mwenyezi Mungu anamwambia Mtume Muhammad (s.a.w.w.) awaombee watu msamaha.⁶¹

Mwenyezi Mungu husamehe kupitia uombezi:

Mwenyezi Mungu husamehe dhambi kuu za wale wanao wanamuomba Yeye kupitia uombezi (*shafa'ah*). Qur`ani in-a-sema:

⁶⁰ Angalia *Al-Mizan*, Juz. 17, uk. 310.

⁶¹

فِيمَا رَحْمَةٌ مِّنَ اللَّهِ لَيْتَ لَهُمْ وَلُوْ كُنْتَ فَطَّا غَلِيلَ الْأَلْبَابِ لَأَنْفَضُوا مِنْ حَوْلِكَ فَاعْفُ عَنْهُمْ
وَاسْتَغْفِرْ لَهُمْ وَشَارُونَهُمْ فِي الْأَمْرِ فَإِذَا عَزَّمْتَ فَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُتَوَكِّلِينَ

"Kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu, umekuwa laini kwao. Lau kama ungekuwa mkali mwenye moyo mgumu bila shaka wangelikukimbia. Basi wasamehe na uwaombee maghfira na ushauriane nao katika mambo. Utakapoazimia, basi mtegemee Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wamtege-meao." [Surah al-Imran, 3:159]

وَلَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ عِنْدُهُ إِلَّا لِمَنْ أَذِنَ لَهُ حَتَّىٰ إِذَا فُرِّغَ عَنْ قُلُوبِهِمْ
قَالُوا مَاذَا قَالَ رَبُّكُمْ قَالُوا الْحَقُّ وَهُوَ الْعَلِيُّ الْكَبِيرُ

“Wala hautafaa uombezi mbele Yake ila kwa yule aliyempa idhini. Hata itakapoondolewa fazaa kwenye nyoyo zao, watasema: Kasema nini Mola Wenu? Watasema: Haki, Nayé Ndiye aliye juu, Mkubwa.” [Surah as-Sabaa, 34:23]

كُلُّ نَفْسٍ بِمَا كَسَبَتْ رَهِينَةٌ إِلَّا أَصْحَابَ الْيَمِينِ فِي جَنَّاتٍ يَتَسَاءَلُونَ
عَنِ الْمُجْرِمِينَ مَا سَلَكُوكُمْ فِي سَقَرَ قَالُوا لَمْ نَكُ مِنَ الْمُصَلِّينَ
وَلَمْ نَكُ نُطْعُمُ الْمِسْكِينَ وَكُنَّا نَخُوضُ مَعَ الْخَاضِينَ
وَكُنَّا نُكَذِّبُ بِيَوْمِ الدِّينِ حَتَّىٰ أَتَانَا الْيَقِينُ
فَمَا تَنْفَعُهُمْ شَفَاعَةُ الشَّافِعِينَ

“Kila nafsi iko kwenye rehani kwa iliyoyachuma. Isipokuwa watu wa kuliani. Watakuwa kwenye mabustani wakiulizana. Kuhusiana na wakosefu. Ni kipi kilichowapeleka Motoni? Watasema: Hatukuwa mionganini mwa waliokuwa wakiswali. Wala hatukuwa tukiwalisha masikini. Na tulikuwa tukijiingiza pamoja na wanaojiingiza. Na tulikuwa tukikadhibisha Siku ya Hukumu. Mpaka ikatujia yakini. Basi hautawafaa uombezi wa waombezi.” [Surah al-Muddathir, 74:38-48]

Akifafanua aya hii, Allamah Tabataba`i anajadili kwamba watu wenyewe dhambi ama wanastahili kupata uombezi ili kwamba waweze kusamehewa au wanajiondolea wenyewe haki ya kupokea uombezi na kwa hiyo watabaki mate-

ka wa dhambi zao na watateseka ndani ya Jahannam. Pia Allamah anarejelea hadithi mashuhuri ya Mtukufu Mtume Muhammad (s.a.w.w.) ambamo amenukuliwa akisema:

ادخرت شفاعتي لأهل الكبار من أمتى

**“Nimehifadhi uombezi wangu kwa ajili ya watu wa umma
wangu ambao wametenda madhambi makubwa.”**

Wale watakaopewa haki ya kuombea pia kwa hakika wan-amfurahisha Yeye. Qurani inasema:

يَوْمَئِذٍ لَا تَنْفَعُ الشَّفَاعَةُ إِلَّا مَنْ أَذْنَ لَهُ الرَّحْمَنُ وَرَضِيَ لَهُ
قَوْلًا

**“Siku hiyo uombezi hautafaa ila wa aliyemruhusu Mwingi
wa Rehema na akamridhia kusema.” [surah Twaha, 20:109].**

Tazama pia Sura ya 43:86.

Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu na kwa hiyo anaweza kuwasamehe hata wale wenye dhambi nyingi na kuhukumiwa kuingia Jahannam.

Mwenyezi Mungu huwasamehe wale wenye matumaini katika msamaha Wake:

Kulingana na hadithi nyingi, Mwenyezi Mungu huwatendea watu katika njia ambayo wao wanatarajia Yeye kuwatendea wao. Bila shaka, hili ni jambo moja ambalo linatakiwa liwek-

we katika ulinganifu na mambo mengine pia; hakuna jambo moja linalopaswa kifikiriwa katika kuelewa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyowashughulikia watu. Hivyo, ipo nafasi kubwa sana kwamba kwa kweli Mwenyezi Mungu atawasamehe wale wenye matarajio katika rehema Yake na wanaamini kwamba atawasamehe. Ndani ya hadithi nzuri kutoka kwa Imam Sadiq (a.s.) tunasoma:

آخر عبد يؤمن به إلى النار، يلقيت، فيقول الله عزوجل:
اعجلوه، فإذا أتي به قال له: يا عبدي لم التفت؟ فيقول:
يارب ما كان ظني بك هذا، فيقول الله عزوجل: عبدي وما
كان ظنك بي؟ فيقول: يا رب كان ظني بك أن تغفر لي
خطيئتي و تسكنني جنتك، فيقول الله: ملائكتي وعزتي و
آلائي وبلائي وارتفاع مكاني ما ظن بي هذا ساعة من
حياته يراقط، ولو ظن بي ساعة من حياته خيراً ما روعته
بالنار، أجيروا له كذبه وأدخلوه الجنة. ثم قال أبو عبد الله
عليه السلام: ما ظن عبد بالله خيراً، الا كان الله عند ظنه
به، ولا ظن به سوءاً إلا كان الله عند ظنه به، وذلك قوله
عزوجل: وذلكم ظنكم الذي ظنتم بربكم أرداكم فأصبختم
من الخاسرين (فصلت: 16:23)

“Mja wa mwisho anayetakiwa kupelekwa Jahannam ata-geuza uso na kutazama nyuma. Mwenyezi Mungu (Azza wa jallah), atataka asimamishwe, na atakaporudishwa,

Yeye atamuuliza mja: "Mja wangu! Kwa nini uligeuka nyuma?" Mtu huyo atajibu: "Mola Wangu! Hivi sivyo nilivy-otarajia kutoka Kwako." Mwenyezi Mungu (*jalla jalaluhu*), atamuuliza: Ulikuwa unatarajia nini kutoka Kwangu? Mtu huyo atajibu: "Mola Wangu! Matarajio yangu kutoka Kwako ilikuwa kwamba Wewe ungesamehe dhambi zangu na kunipa makazi kwenye Pepo Yako." Hapo ndipo, Mwenyezi Mungu atasema: "Malaika Wangu! Kwa hadhi Yangu, neema Zangu, Mitihani Yangu na Cheo Changu cha Juu, mtu huyu kamwe hajawahi katika maisha yake kuwa na fikira nzuri kuhusu Mimi. Kama angekuwa amefanya hivyo nisingemuogopesha kwa (kumuelekeza) Jahannam. Kubalini uongo wake na mruhusuni aingie Peponi."

Halafu Imam Sadiq (a.s.) akasema: "Hapana mja wa Mwenyezi Mungu anayekuwa na dhana nzuri kuhusu Mwenyezi Mungu isipokuwa kwamba mtu huyo atam-kuta Mwenyezi Mungu anamshughulikia kama al-ivyokuwa anafikiri. Hivi ndivyo inavyoweza kueleweka kutoka kwenye aya:

وَذِلِكُمْ طَبِّقُوكُمْ الَّذِي ظَنَنتُمْ بِرَبِّكُمْ أَرْدَأْكُمْ
فَاصْبَحْتُمْ مِنَ الْخَاسِرِينَ

"Na hiyo dhana yenu mliyokuwa mkimdhania Mola Wenu, imewaaangamiza; na mmekuwa mionganoni mwa waliopata hasara ."⁶²

⁶² *Bihar al-Anwar*, Juz. 7. uk. 287. Kuna sura juu ya nini kitadhihiri mnamo Siku ya Hukumu kutoka kwenye rehema Yake. Hadithi hiyo hapo juu ni hadithi ya tatu ya sura hii. Hadithi zote tisa ndani ya sura hii zinatafakuri kufanyiwa kwa ajili ya uelewa bora zaidi wa rehema ya Ki-Mungu na baadhi ya fikira ambazo zimezungumziwa hapo juu kama vile kusamehewa kwa dhambi, kufuta dhambi kutoka kwenye rekodi ya

Hii ni rehema na ukarimu Wake na hii ndio maana pale Imam Sajjad (a.s.) alipoambiwa kuhusu kauli ya Hasan al-Basri: "Si jambo la kustajabisha jinsi watu wengine wanavyoangamizwa; ni jambo la kushangaza jinsi mtu ye yeyote ana-vyoweza kuokolewa," Imam (a.s.) akasema: "Mimi nasema, 'Si ajabu jinsi baadhi ya watu wanavyoookolewa. Ni jambo la kushangaza jinsi baadhi ya watu wanavyoangamia licha ya rehema ya jumla ya Mwenyezi Mungu.'"⁶³

Hivyo, wale wanaokwenda Jahannam ni wale ambao wamejiondolea ustahili wao wao wenyewe, na hatimaye hawafaidiki na rehema Yake kubwa. Wanahukumiwa kwenda Jahannam, na kwa kweli Jahannam itateseka kutokana na wao. Inawezekana umepata uzoefu kwamba wakati mwingine unapaswa kushughulika na baadhi ya watu ambao huku-umiza kama moto unavyounguza au hata kwa ukali zaidi; moto huunguza ngozi yako, lakini watu hawa wanaunguza moyo wako, akili na kila kitu ulichonacho. Labda hii ndio sababu kwamba wanaweza kuwa kuni za Moto wa Jahannam (2:24; 3:10; 66:6) ambao unaweza kuunguza hata moyo wa mtu (104:6 &7). Kwa hiyo, kile kinachofanya moto wa Jahannam uendelee kuwaka inaonyesha ni watu kama hao tu.

Kauli ya mwisho:

Pamoja na kwamba dunia hii na Siku ya Hukumu yote ni udhihirisho wa rehema Yake kubwa, itakuwa ni ndani ya Pepo tu ambamo rehema Yake inaweza kudhihirini katika njia iliyo bora kadiri iwezekanavyo, kwani hakuna kizuizi au mpaka uliopo. Dunia hii ni finyu mno hivyo kwamba haina fursa

matendo ya mja na ubadilishwaji wa dhambi na kuwa matendo mema.

⁶³ Ibid. Juz. 75. uk. 154.

ya kuwa na kila kitu: pepo haina mpaka. Chochote unachotaka Mwenyezi Mungu atakupa (39:34; 42:22) na hata zaidi (50:35). Kwa uelewa wetu mdogo na tamaa ya vitu vidogo ikilinganishwa na ukarimu Wake mwangi, Mwenyezi Mungu hatupatii sisi kile tunachotaka tu: kwanza anakupa kile una-chotamani na halafu anakupatia thawabu za ziada ambazo amezitayarisha na amezificha kama kitu cha kushtukiza:

فَلَا تَعْلَمُ نَفْسٌ مَا أَخْفِيَ لَهُمْ مِنْ قُرَّةِ أَعْيُنٍ جَزَاءً بِمَا كَانُوا
يَعْمَلُونَ

“Nafsi yoyote haijui waliyofichiwa katika yanayo furahisha maisha; ni malipo ya yale waliyokuwa wakiyatenda.”

[Surah as-Sajda, 32:17]

Mwenyezi Mungu na atuwezeshe sisi kuelewa vema zaidi na kunufaika zaidi kutokana na rehema Yake, na tunaomba sisi tupokee zaidi na tuwe mkondo wa rehema Yake kuwafikia watu. Mwenyezi Mungu hutafuta mawakala wa kueneza rehema Yake. Nani yupo tayari kuwa wakala Wake? Kama uki-wa wakala wake, atakupa wewe kwa wingi sana hivyo kwamba rehema Yake itabubujika kutoka kwako kwenda kwa wen-gine, kama Mtume Mtukufu Muhammad (s.a.w.w.) (3:159; 21:107). Tunamuomba Mwenyezi Mungu atusamehe dhambi zetu zote na makosa yetu yote na tunamuomba Yeye wakati wote atuweke sisi kwenye njia iliyonyooka.

Hitimisho:

Ndani ya mfululizo huu wa makala nane, tulichunguza baadhi ya mielekeo ya uelewa wa Kislamu juu ya rehema ya

Mwenyezi Mungu. Tumejifunza majina na sifa mbali mbali za Mwenyezi Mungu na kuonyesha kwamba majina na sifa ambazo zinahusiana na rehema Yake ndizo ambazo zimesisitizwa sana. Halafu tukajifunza baadhi ya sifa za rehema za Ki-Mungu na kujadili kwamba rehema Yake ndio sababu ya kuumba dunia. Kutokana na rehema Yake, Mwenyezi Mungu ametuumba sisi na yote yale tunayoyahitaji kwa ajili ya mai-sha na manufaa yetu na na akatuletea Mitume na ujumbe wa Ki-Mungu kwa ajili ya muongozo. Pia tulirejelea aina mbali mbali za rehema ambazo Mwenyezi Mungu amempatia binadamu kwa utaratibu wa kumwezesha kutembea kwenye njia iliyonyooka. Baadhi ya watu wanashukuru na baadhi ya watu hawashukuru. Wale wasioshukuru hujinyima wao wenyewe rehema za ziada; wale wenye kushukuru Mwenyezi Mungu atawapa rehema zaidi na za nyongeza. Mwisho kabisa, tulijifunza jinsi Mwenyezi Mungu anavyowafanyia watu kwa rehema Zake mnamo Siku ya Hukumu kuhusiana na malipo yenye ukarimu mwangi ambamo ataonyesha usamehevu Wake mkubwa.

Kwa hiyo, mambo kadhaa ya rehema za Mwenyezi Mungu yalipitiwa katika mfululizo huu ufuatao: (1) rehema ya Mungu kama ile inayofanya kazi katika mambo ya kiroho na kimaadili ya Kislamu, (2) maana kamili za sifa za Mwenyezi Mungu, kama vile *al-Rahman* na *al-Rahim*, pamoja na sifa Zake zinazoambatana pamoja za rehema na uwezo kuhusiana na lengo la Mwenyezi Mungu katika uumbaji Wake, (3) sifa kama vile ukarimu Wake, usamehevu Wake, na upole Wake pamoja na maelezo zaidi ya rehema Zake zilizounganishwa na elimu na ujuzi Wake na ukwasi Wake, 4) rehema ya Mwenyezi Mungu katika kutayarisha mipango mbali mbali kwa ajili ya uhai na manufaa yetu hapa duniani, kama vile

kuumba nyota, kuzishikilia mbingu, na kutuokoa na majanga; na rehema ya Mwenyezi Mungu katika kumuongoza binadamu kwani aliwapelekea wanadamu mitume wenye sifa za kutokosea (umaasum) za uwezo wa kutambua hidia za wengine na upole, (5) Mpango wa Mwenyezi Mungu kwa ajili ya aina mbali mbali za msaada katika maisha ya kiroho ya watu, kama vile, ulinzi dhidi ya Shetani, upotovu, na dhidi ya nafsi yenye kushawishi, (6) aina na viwango mbali mbali vya msamaha wa Mwenyezi Mungu, jinsi anavyoweza hata kubadilisha matendo mabaya ya mtu na kuwa mazuri, jinsi watu wanavyoathirika na rehema ya Ki-Mungu na nyongeza ya rehema kwa wale wanye subira, (7) watu wanaojipatia wenyewe haki ya kupokea rehema ya ziada kutoka kwa Mwenyezi Mungu, baadhi ya sifa hizo zikiwa ni subira, watenda mema, waadilifu, wenye kutubia, watiifu, na wale wanaohama na kupambana kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na 8) msamaha wa Mwenyezi Mungu na malipo ya ukarimu mwingi.

MWISHO

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Thelathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swalaa

16. Misingi ya Maarifa
17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu
35. Mwenyezezi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)

38. Adhana.
- 39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusherehekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii
53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata

60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzuu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita
70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam 'Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-lлаah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)

81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja'a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini
88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgongwa
97. Sadaka yenye kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenye Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi

103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Kwanza)
106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqualain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenyе hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru
123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa

125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vya kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vya kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vya furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?
140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Kuhuzunika na Kuomboleza - (Azadari)
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah

146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 1
- 153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.
157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.

168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah
174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas'ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur'ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya 'Alaa Khayri'l-Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein ('as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye

189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)
192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Upotoshaji Dhahiri katika Turathi (Hazina) ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwanendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

MUHTASARI

MUHTASARI

MUHTASARI

MUHTASARI
